Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 8 JULAI, 2003

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):**

Hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa mwaka 2003/2004.

**MHE. HAMISI J. NGULI (k.n.y. MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 180

**Hospitali za Wilaya Kuwa Chini ya Halmashauri**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa mapato ya Halmashauri ni madogo sana kiasi cha kufanya Zahanati na vituo vya afya vilivyoko chini ya Halmashauri hizo zihudumiwe kwa shida sana:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizoifanya Serikali iamue kuziweka hospitali za Wilaya chini ya Halmashauri za Wilaya wakati inatambua kuwa Halmashauri hizo hazina uwezo wa kutosha kuzihudumia hospitali hizo kwa ufanisi?

(b) Kwa kuwa hospitali ya Wilaya ya Mufindi iliyopo Mafinga ni ya zamani na ni chakavu sana, je, Serikali ina mpango gani wa kuikarabati kwanza kabla haijaikabidhi kwa Halmashauri?

(c) Kwa kuwa hospitali za Wilaya zimekuwa chini ya Serikali Kuu kwa muda mrefu, je, Halmashauri za Wilaya na Miji kupitia umoja wao *ALAT* zimekubali jukumu la kuziendesha Hospitali hizo au ni agizo la Serikali Kuu tu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizofanya Serikali kuziweka hospitali za Wilaya chini ya Halmashauri ni kuzipa Halmashauri au wananchi kwa ujumla uwezo na madaraka zaidi ya kumiliki na kuamua juu ya maendeleo ya afya katika Wilaya. Chini ya utaratibu huu, Bodi za Afya za Wilaya na Kamati za Uendeshaji za Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati zitaundwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu inatambua Halmashauri zetu hazina uwezo wa kutosha wa kuzihudumia Hospitali za Wilaya na ndiyo maana hivi sasa inatoa na inaendelea kutoa ruzuku kwa huduma za jamii katika Wilaya. Halmashauri nazo zinashauriwa kuchangia na kuanzisha vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya kuboresha huduma za Afya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Mufindi ipo tayari chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi tangu mwaka 2001 ilipoanza kugharamia shughuli za uendeshaji wake. Kuhusu uchakavu wa majengo ya hospitali hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi itaweka makisio ya ukarabati katika mpango wake wa maendeleo wa mwaka 2004/2005. Mpango huo utaonyesha mchango wa Halmashauri na Serikali Kuu au Wahisani wengine mbalimbali wa ndani na nje ya Wilaya. Serikali Kuu itachangia fedha kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali hiyo ya Wilaya ya Mufindi kulingana na uwezo wa Serikali utakaokuwepo wa mwaka 2002/2003. Ukarabati wa chumba cha upasuaji na chumba cha kuhifadhia maiti umefanyika. Kwa mwaka 2003/2004 Halmashauri inaendelea na ukarabati wa *OPD Ward* na *Maternity Waiting Home.*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Halmashauri kuziendesha Hospitali za Wilaya ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 1999 chini ya Sheria ya *The Local Government Laws – Miscellaneous Amendment Act, 1999,* katika Sehemu II, III, V na VII.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria yanaenda sambamba na mapendekezo ya siku nyingi ya Halmashauri kupitia umoja wao wa *ALAT* wa kuzifanya Halmashauri kuwa na mamlaka zaidi ya maamuzi, kumiliki, kuendesha na kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi wake.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wakati Serikali Kuu inazimiliki Hospitali hizi za Wilaya, imethibitika kwamba hali yake ilikuwa mbaya na iliendelea kuwa mbaya na kwa kuwa sasa hivi imeamua kuzipeleka Hospitali hizi katika Halmashauri jambo ambalo linatarajiwa kwamba labda hospitali hizi zinaweza kuwa bora zaidi. Lakini haziwezi kuwa bora zaidi kama hakuna mkakati wa dhati wa kuziongezea fedha.

Je, mabadiliko haya yanaweka mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hospitali hizi sasa zitakuwa na fedha zaidi ili hivyo vikatoa huduma nzuri zaidi kwa wananchi ili uamzi huu uwe na maana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza katika majibu hapa kwamba suala la Serikali kuchangia, kuboresha huduma ya Sekta ya Afya kwa kiasi kikubwa inategemea uwezo wa kifedha ambao Serikali inao kwa wakati huo. Kwa hiyo, ninaloweza kusisitiza tu hapa ni kwamba juhudi ambazo hivi sasa zipo zitaendelea kuwepo ili mradi fedha inapatikana. Hatutachelea kuzisaidia hata kidogo Halmashauri zetu katika kuboresha huduma si za Afya tu lakini hata nyinginezo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba ili kuboresha huduma za tiba katika hospitali zetu za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati, iko haja ya kupeleka wataalam wa kutosha hasa Madaktari na ma-*nurse?*

Kwa mfano, katika Vituo vya Afya kunatakiwa kuwe na Daktari Msaidizi ambaye atasaidia *minor surgeries.* Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba suala la wataalam katika sekta ya Afya, katika ngazi mbalimbali ni suala la msingi kabisa na tumekuwa muda wote tunasema hivyo na hata Wizara ya Afya imekuwa ikisema hivyo. Lakini wote ni mashahidi kwamba juhudi tunazozifanya sasa bado hazijaleta matunda mazuri.

Tumekuwa tukitangaza nafasi hasa kwenye ngazi za Vituo vya Afya na Zahanati kujaribu kupata Waganga Wasaidizi na Wahudumu wengine mbalimbali.

Lakini mara zote imeshindikana kwa sababu bado wataalam wa ngazi hizo hatuna wa kutosha. Kwa hiyo, juhudi zilizopo sasa za ku-*train* zitaendelea ili kuweza kuboresha hiyo hali ambayo sasa hivi ni tatizo kubwa.

**MHE. CHIFU ABDALLAH S. FUNDIKIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Serikali ina nia kubwa ya kupeleka madaraka katika sehemu zile ambapo wanakaa watu wengi yaani kama Wilayani na Vijiji na kila mahala. Nadhani hiyo ndiyo sababu pia wanapeleka hata jukumu la kuhudumia hospitali kwa Halmashauri.

Je, kwa nini iwe upande huo mmoja tu wa kuwapa Halmashauri madaraka zaidi bila fedha, lakini upande mwingine wanawaondoshea madaraka ambayo wanayostahili kabisa, kwa sababu kwa mfano haya mabadiliko ya Sheria ya juzi yamenyang'anya Halmashauri uwezo wa kusimamia watumishi wao? *(Makofi)*

Je, Waziri anatuambia kwamba hii haja ya kupeleka majukumu ya Hospitali katika Halmashauri inaendana vipi na upande mwingine wanawanyang'anya madaraka na upande mwingine wanawapelekea madaraka bila kuwapa fedha za kuendeshea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali, Sera ya Serikali na kwa kweli mwelekeo mzima wa shughuli za Serikali ni kupeleka madaraka katika ngazi za chini, ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji na ndiyo maana shughuli zote sasa, sekta zote sasa zinasimamiwa kwa ujumla na Halmashauri zetu.

Kwa hiyo, hakuna tena suala la kurudi nyuma kwamba tutawapokonya tena madaraka. Labda tu ni katika kutekeleza maamzi fulani fulani inaweza ikaonekana hivyo. Lakini dhamira yetu bado iko pale pale.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla swali lingine halijaulizwa. Ningependa tu kuwaarifu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, amemteua Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kuwa Kaimu wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Na. 181

**Gari kwa Ajili ya Ubalozi wetu Marekani**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna habari kwamba kwa muda mrefu ubalozi wetu huko Marekani hauna gari la kumhudumia balozi wetu aliopo huko kwa kuwa gari lililokuwepo ni moja tu kwa ajili ya kuwahudumia wafanyakazi:-

(a)Je, ni tatizo gani lililosababisha ubalozi wetu nchini humo kutokuwa na gari lenye hadhi ya kibalozi kwa matumizi ya kikazi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kitendo hicho kinamdhoofisha balozi huyo?

(c) Kama Serikali inakiri kutokuwepo kwa gari kwa ajili ya matumizi hayo niliyotaja, je, ni lini Serikali itaupatia ubalozi huo gari kwa ajili ya balozi wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inazo Ofisi mbili za Ubalozi nchini Marekani, *Washington D.C.* kwa ajili ya uwakilishi wetu kwa Taifa la Marekani na Mjini *New York* kwa ajili ya uwakilishi wa kudumu, kwenye makao makuu ya Umoja wa Mataifa. Kati ya balozi zetu zote 28 nchi za nje, ni balozi hizi mbili tu *Washington* na *New York* ndizo zinazotumia utaratibu wa magari ya kukodi kwa muhula maalum yaani *lease,* kwa gari la uwakilishi yaani gari rasmi la balozi kutoka kampuni ya kukodisha magari ya kibalozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilitoa kibali cha kutonunua magari ya Serikali kwa balozi hizi mbili, baada ya balozi husika kuomba na kujenga hoja waruhusiwe kutumia utaratibu huo kwa magari ya uwakilishi, kwani ni wa unafuu zaidi na pia ni wa uhakika wa kupata gari mpya kila mwaka isiyo na matatizo, kulinganisha na gharama kubwa za ununuzi, utunzaji pamoja na gharama za bima kwa gari kama hilo, inapokuwa mali ya Serikali.

Kufuatia utaratibu huo, gari linakuwa kama mali ya ubalozi, kwa muhula wote wa Mkataba ambao ni kati ya mwaka mmoja hadi mitatu. Hivyo, gari hilo huwa mikononi mwa ubalozi kwa kipindi chote hicho, linaendeshwa na dreva wa ubalozi na halina gharama yoyote zaidi, isipokuwa mafuta tu na kuisafisha. Zaidi, kama nilivyoelezea hapo awali, kila baada ya miezi 12 kampuni husika hutoa gari mpya nyingine inayofanana “shilingi kwa ya pili” na gari ya awali. Faida kubwa inayopata kampuni husika ni *free publicity* yaani matangazo ya bure, kwamba gari la aina hiyo ni gari linalotumiwa na Mabalozi wa Mataifa mbalimbali, kwa vile linaaminika na lina hadhi na heshima ya kibalozi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ukodishaji wa magari, kwa mtindo niliuoelezea hapo juu, ni utamaduni unaokubalika na unatumiwa na Mataifa mengi duniani, kwa hoja na sababu nilizozitaja, hivyo hakuna hisia za udhalilishaji wala unyanyasaji wa nchi au balozi husika. Huko Marekani, kwa mfano, nchi nyingi sana zinatumia utaratibu huo, hadi hii leo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hali ya uchumi duniani kubadilika na wakati huo huo hali ya usalama nchini Marekani kuwa ya wasiwasi zaidi, hasa baada ya matukio ya ugaidi wa Septemba 11, 2001, Serikali iliamua, tokea mwaka wa fedha wa 2002-2003, kuondokana na utaratibu huo, huko Marekani, kwa balozi zetu zote mbili.

Katika mwaka huo huo wa fedha, Wizara yangu imeshaanza kupeleka fedha huko *New York,* ambako ubalozi ulifikia mwisho wa kumaliza mkataba wa kukodi, ili wanunue gari la uwakilishi na ambalo ni mali ya Serikali. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, Wizara yangu imenuia kununua gari la uwakilishi kwa ubalozi wetu wa *Washington,* ambao mkataba wao wa kukodi gari la uwakilishi unamalizika mwezi wa Oktoba 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, kwamba Serikali haiwezi hata siku moja kufanya vitendo vya kumdhoofisha balozi au Maafisa wake. Serikali inahakikisha kuwa inawapatia mabalozi wake mahitaji yao yote rasmi *(Official)* kulingana na uwezo wa kifedha unaokuwepo wakati husika.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri toka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba mjini *New York* na *Washington* na balozi za huko zilikuwa zinakodi gari za makampuni husika. Je, mbona balozi wa mjini *New York* kuanzia mwezi Januari hadi hivi sasa hana gari, sasa ni jambo gani linalosababisha kama umesitishwa mkataba wa kukodi wakati ambapo fedha hazikutumwa kwa ajili ya ununuzi wa gari mpya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli fedha kwanza zilitumwa kwa ubalozi wetu katika tarehe 29 Oktoba, 2002, zilitumwa dola 49,991, kuweka kama *advance* ya kununua gari jipya. Lakini kwa matatizo waliyokuwa nayo au kwa sababu ambazo wao wenyewe ubalozini sababu ambazo wanazijua, ilibidi fedha hizo wazitumie kwa mambo mengine. Lakini kama nilivyosema, tunahakikisha tutapeleka pesa nyingine zaidi ili litafutwe gari la kununua. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matumizi ya fedha za Serikali hupitishwa na Bunge hili na hakuna mamlaka nyingine yoyote inayoweza kubadilisha matumizi hayo bila ya idhini ya Bunge na Mheshimiwa Naibu Waziri, ametueleza kwamba pesa zilizopelekwa ni kwa ajili ya kununulia gari badala yake zikatumika kwa shughuli nyingine ambazo hazikuidhinishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kutueleza idhini ilipatikana wapi ya kubadilisha matumizi ya fedha za Serikali bila utaratibu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sio kweli kwamba kila *Vote* inayokwenda Ubalozini matumizi yake lazima yapitishwe katika Bunge hili. *(Makofi)*

Jumla ya fedha zinazopelekwa Wizarani au kupelekwa Balozini, sisi kule ndiyo tunaamua kwamba kifungu hiki kitumike vipi na kwa ajili gani. Vipo vifungu vya jumla ambavyo Wabunge wanavipitisha lakini katika vifungu vile mna mafungu madogo madogo mengi ndani yake na sisi Wizarani ndiyo tunaamua. *(Makofi)*

Na. 182

**Kero Wanayopata Watanzania wakati Wanapoomba *Visa***

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN (k.n.y. MHE. MBARUK K. MWANDORO)** aliuliza:-

Kwa kuwa yako malalamiko mengi kuhusu ugumu na adha kubwa wanayopata Watanzania walio wengi wakati wanapoomba *Visa* za kuingia
kero hii umekuwa ukiongezeka siku hadi siku na kufanya Watanzania wengi kuchelewa au kukosa kabisa nafasi za masomo, matibabu au biashara:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani hadi sasa kurekebisha kero hiyo kwa ushirikiano na nchi husika?

(b) Je, ni kwa nini Serikali yetu isichukue hatua za kulipiza *(reciprocation)* kwa raia wa nchi husika mbali ya wale ambao ni muhimu sana kwa biashara, uwekezaji au ushirikiano wa kiufundi?

(c) Je, Serikali inakusudia kuchukua hatua gani kuwadhibiti Watanzania ambao kwa namna fulani wanahusika na vitendo vinavyochangia kulipatia Taifa sifa mbaya na kusababisha hata wale wasiokuwa na hatia kufikiriwa kuwa waovu na hivyo kunyimwa kabisa Visa au kupata Visa baada ya usumbufu mkubwa mno?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikifuatilia baadhi ya maombi ya Watanzania waliokataliwa *Visa* na Balozi za nje ambao wamefika Wizarani kwangu kuomba msaada. Kwa vile aghalabu, pale mwombaji anaponyimwa visa huelezwa kwa maandishi na ubalozi husika sababu za kunyimwa *Visa,* Wizara yangu huchambua kwa makini maelezo hayo na inapoona kuweko kasoro ya kiutaratibu tu basi humshauri mhusika akamilishe taratibu zinazotakiwa na baadaye aombe *Visa* upya, kama alivyoshauriwa na balozi husika. Balozi husika nazo, huwapa visa walizoomba baada ya kutimiza na kukamilisha masharti waliyowekewa.

Lakini kwa maombi yenye utata, Wizara yangu imekuwa ikiwaomba na kuwashauri wahusika kufuata na kutimiza masharti na kanuni za kupata *Visa,* kama walivyoelezwa na maafisa wa balozi zinazohusika. Sina budi kusisitiza kwamba uamuzi wa kutoa *Visa* ni wa nchi husika na hivyo Wizara yangu haiwezi kutengua uamuzi wa kuwapa au kutowapa *Visa* waombaji, bali hutoa ushauri wa kufuata taratibu zinazotakiwa.

Kwa ajili hiyo, Wizara yangu imeziomba ofisi za balozi husika zitayarishe taarifa kamili zinazotoa mwongozo bayana kwa maandishi kuhusu masharti, taratibu, kanuni na mahitaji yote mengine ya lazima (kama vile vyeti, chanjo, uwezo wa kujikimu na viwango vya ada ambayo yanahitajika kukamilishwa na waombaji wa aina mbalimbali za *Visa* ili waombaji hao waepuke kufanya makosa, wasiyokusudia na hivyo kuonekana kuwa wakiukaji wa masharti, taratibu na kanuni husika.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya Balozi husika zimefanya hivyo na balozi nyingine kama vile ubalozi wa Uingereza umekwenda hatua moja mbele zaidi, kwa kuchapisha magazetini mwongozo huo. Nawashauri waombaji wote wa *Visa* za aina zote waombe balozi zote husika nakala za miongozo yao ya kuomba *Visa* na wasome kwa makini kabisa miongozo hiyo kabla, narudia, kabla ya kujaza fomu ya kuomba *Visa* na kuiwasilisha kwenye balozi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Serikali haioni sababu ya kumnyima *Visa* mwombaji kwa kulipiza kisasi tu kwa sababu kila nchi ina haki yake ya kujiwekea utaratibu wa kutoa *Visa* ili kulinda maslahi yake ya Taifa. Hata nchi yetu ina utaratibu wa kuwahoji na kuchambua maombi ya wananchi wa nchi mbalimbali, zikiwemo za Magharibi, wanaotaka kuja nchini kwetu, kama wanavyofanya wao, ili kuhakikisha kuwa wametimiza na kufuata taratibu husika. Sidhani kwamba itakuwa ni jambo zuri na busara kumnyima mtu *Visa* kwa hoja ya nipe, nikupe *(reciprocity)* bila kujali ukweli na uhalali wa maombi ya *Visa* husika. Hata kwa nchi hizo za Magharibi wale wenye maombi yanayotimiza masharti na taratibu wamekuwa wakipewa *Visa* hata kama awali walikataliwa!

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina taratibu mbalimbali za kulinda na kutunza heshima ya Taifa, ikiwa pamoja na heshima ya Pasi ya Tanzania. Miongoni mwa taratibu hizo ni pamoja na uwezekano wa kumnyang'anya au kumkatalia mtu kupewa Pasi ya kusafiria endapo itabainika kwamba amekiuka sheria na kanuni za kuhodhi na kusafiria Pasi ya Tanzania.

Aidha, wanaomiliki Pasi za kughushi au Pasi za wizi hufikishwa Mahakamani. Hata hivyo, hatua za kudhibiti watu wanaochafua jina zuri la Tanzania na kusababisha hata wale wasiokuwa na hatia kufikiriwa kuwa waovu ni jukumu letu sote, si Serikali peke yake! Ni jukumu la kila mmoja wetu, tukiwemo sisi Wabunge.

Kwa kuwa watu hao wanaokiuka masharti, taratibu na kanuni za kuomba *Visa* au kuishi nchi za nje kinyume na mujibu wa *Visa* zao ni watoto, wazazi, ndugu, majirani, jamaa na marafiki wetu, basi hatuna budi kushirikiana kuhimiza kuendelea kuheshimu taratibu na masharti yanayotolewa pindi tunapoomba au kupata visa kwa ajili ya kwenda nje. Zaidi tusisite kuwatahadharisha na kuwaonya wale wachache wanaovuruga kwa

makusudi heshima ya Mtanzania na jina la Pasi ya Tanzania na ikibidi wafichuliwe! *(Makofi)*

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania wamekata rufaa yaani *appeal* kwa maombi ya *Visa* ya kuingia nchini Uingereza wanatakiwa kulipa takriban shilingi laki tano ambazo hawarejeshewi hata pale ambao rufaa zao hazifanikiwi. Je, Serikali haioni kwamba huo ni unyang'anyi kwa wahusika na upotevu wa fedha za kigeni kwa Taifa letu, kwa ujumla bila sababu za msingi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwanza sidhani kwamba kuna ada ya laki tano, sijui. Ninavyojua ni kwamba kuna ada ya shilingi 50,000/=.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba tulizungumza na Serikali ya Uingereza na nilipata swali hili kulijibu hapa Bungeni kwamba Waingereza wanasema hivi, anapoomba mtu *Visa* hatua ya mwanzo baada ya kuangaliwa fomu zake hushauriwa kama hazikukamilika, usiendelee kuomba *Visa* kwa sababu hutapata. Akisisitiza kwamba bado nataka kuomba, Serikali inamwambia, Ofisi ya Uingereza na ndani ya ile *Visa* imeandikwa, kwamba tukianza ku-*process* kama hutafanikiwa pesa hutarudishiwa na Serikali ya Uingereza inatoa hoja tatu, ya kwanza inasema kwamba wanapokea karibu maombi 70 kwa siku na kwa ajili hiyo inabidi waajiri watu wa ziada kuchambua fomu hizi. Wao hawawezi kutoa, wakalipa watu hawa wa ziada. Kwa hiyo, wanatoa katika malipo yale ya *Visa.*

Pili, kila mwombaji wanasema lazima aje binafsi kusailiwa. Wanaokuja kusaili ni watu ambao wanatakiwa walipwe katika gharama hizo hizo. Tatu, wanasema wana vifaa chungu mzima ambavyo vinabidi vilipiwe katika kuchunguza taratibu za *Visa* kati ya Dar es Salaam na Uingereza.

Kwa ajili hiyo, wanabainisha wazi wazi katika fomu zao kwamba iwapo utasisitiza kwamba unaitaka *Visa* yako, pamoja na kwamba wametushauri u-*with draw* ukisisitiza kwamba ikianza ile *process* tu lazima gharama hizi utazibeba, ufanikiwe au usifanikiwe. Sasa hapo inakuwa ni hiari ya mtu mwenyewe.

Na. 183

**Tatizo la Watu Kujiua Wenyewe**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa siku hizi imezuka tabia ya baadhi ya watu kujiua wenyewe lakini kabla ya kufanya hivyo baadhi yao huwa wanaacha barua zinazoelezea visa na sababu mbalimbali zinazosababisha uamuzi huo:-

(a) Je, Serikali imefanya uchunguzi gani wa kina na wa makusudi juu ya sababu zinazotolewa kufuatia uamuzi wa vifo hivyo ili kubaini tatizo sugu linalosababisha watu wengi sasa kujiua ovyo?

(b) Je, Serikali imeweka mikakati gani na ya haraka ya kuelimisha wananchi ili wasichukue uamuzi wa kujiua wanapofikwa na matatizo mbalimbali magumu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haijafanya uchunguzi wa kina ili kufahamu sababu zinazowafanya wahusika kufikia uamuzi wa kujiua.

Hata hivyo sababu za jumla zinazopelekea watu kujiua ambazo zimetolewa na watafiti wa sayansi ya jamii ni pamoja na kushindwa kufikia malengo ambayo binadamu anajiwekea, kukata tamaa ya maisha kutokana na hali ngumu ya kiuchumi, kuugua kwa muda mrefu kusiko na dalili ya kupona, migogoro ya kifamilia, kutetereka kwa mahusiano ya kimapenzi, Magonjwa ya akili, msongamano wa mawazo na imani kali za kidini *(religious fundamentalism).*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikisimamia mazingira mazuri kwa asasi na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo hutoa ushauri nasaha kwa vijana na masuala ya kifamilia. Tunaziomba Taasisi za dini zote zitoe ushirikiano mkubwa kupitia mafundisho ya kiroho ili kupunguza tatizo hili linaloongezeka.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya wazazi wa kambo ambao wana tabia ya kuwatesa sana watoto wa kufikia na baadhi ya watoto hao hujiua wenyewe kwa kukimbia mateso yanayowapata, je, Serikali inawachukulia hatua gani wazee kama hao endapo mtoto ameamua kujiua na ukapatikana ushahidi kamili?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa baadhi ya watu wanaoamua kujiua wenyewe ni wale waliothirika kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri mwenyewe, hao wenye matatizo kama hayo na uamua kujiua kwa kukimbia mateso na kutengwa yaani stigma na jamii na vile vile kukosa dawa za kuwatibu, je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuwahifadhi na kuwatunza wagonjwa kama hao ili kuepusha vifo kama hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hali ya kuonekana kwamba kila mzazi wa kambo anakuwa na roho mbaya kwa watoto wa kufikia. Lakini nataka kusema kwamba haya ni

mawazo ya ujumla mno, wapo wazazi wa kambo ambao wanawatunza watoto wa kufikia vizuri zaidi.

Kwa hiyo, yule mzazi mwenye roho mbaya kwa mtoto awe wa kufikia au wa ndugu yake au wa kwake mwenyewe, ni tabia ya ubinafsi na pengine ni jukumu letu jamii yote, kuhakikisha kwamba tunapoona hali kama hiyo inatokea kwa jirani yako basi ni vema wakaarifiwa hata wazee mtaani au viongozi wa dini ili huyo bwana aweze kupewa ushauri nasaha. Ni vigumu kwa kweli kwa Serikali kuona kila kinachotokea katika mtaa, lakini ni rahisi zaidi kwa kila mwananchi kuona linatokea kwa jirani yake.

Kwa hiyo, tunaomba ushirikiano wa wananchi ili watoto wetu wasindelee kuteseka kiasi hata cha kuamua kujinyonga. Pale unapopatikana ushahidi watu kama hao wakipelekwa Mahakamani hatua za Kisheria huchukuliwa dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wale waathirika kwamba kwa nini Serikali isiwasaidie kwa kuwapa ushauri nasaha pengine na matibabu ili wasijinyonge?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba kwa wale ambao wanayaweka wazi matatizo yao wakaripoti katika mahospitali yetu huwa wanapewa ushauri nasaha na kwa Muhimbili ni kila Ijumaa, kila Mkoa una taratibu zake. Lakini bahati mbaya hao wanaofikia kujinyonga ni wale ambao hawataki hata kueleza ukweli mfano kwamba kuugua kwa muda mrefu, kupungua kilo na madonda pengine sababu ni hii hata kama anajua, kwa hiyo, anaona bora aondoke mapema kabla siku yake haijafika. Sasa hawa hatuna njia nao lakini wale ambao wanajitokeza hupata ushauri nasaha.

Na. 184

**Sekta ya Kilimo Kuhusishwa na Mpango wa *NSSF***

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa shughuli za Shirika la *NSSF* zinahusika na kupanua mipango ya hifadhi ya jamii na kukinga jamii isiyo sekta maalum katika matatizo ya kiuchumi; na kwa kuwa sekta isiyo maalum ni kundi kubwa la wakulima ambao ni sawa na asilimia 85 na inaliingizia Taifa pato la karibu asilimia 70:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuliwezesha Shirika la *NSSF* kuhusisha sekta ya kilimo na sekta nyingine zisizo rasmi katika mipango yao ya kukinga jamii na matatizo ya kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mbunge wa Kilosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi nyingi hasa zile zinazoendelea na mipango ya hifadhi ya jamii imekuwa ikielekezwa zaidi kwa wafanyakazi walio katika sekta rasmi

na kuziacha sekta zisizo rasmi ikiwemo sekta ya kilimo bila kinga zinazotolewa na mifumo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti mbalimbali zilizofanyika duniani kuhusiana na mpango wa hifadhi ya jamii zinaonyesha kwamba mipango ya hifadhi ya jamii katika nchi zilizoendelea tayari imefikia zaidi ya asilimia 80 ya watu wake wakati nchi zinazoendelea ni asilimia kumi tu ya watu wake ndio wako kwenye mipango ya hifadhi ya jamii.

Katika kipindi cha mwaka 2000/2001 Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* lilifanya utafiti wenye nia na lengo la kuangalia namna ambavyo sekta isiyo rasmi inaweza kuingizwa katika mpango wa hifadhi ya jamii wa *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huu ulifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Tabora, Shinyanga, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa. Mikoa hii ilichaguliwa kutokana na michango yake mikubwa kwenye uchumi wa Taifa. Sekta zilizohusishwa kwenye utafiti huu ni kilimo, madini, uvuvi na biashara ndogo ndogo *(petty trade)*.

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa, asilimia kubwa ya walihojiwa yaani asilimia 56 wana uwezo wa kuchangia *NSSF* kiasi cha kati ya shilingi 1,000 hadi 3,000 kwa mwezi. Njia zinazoweza kutumika katika uchangiaji pia ziliangaliwa na kuonyesha kuwa wengi wanaweza kuchangia kupitia vikundi vyao au vyama vyao vya ushirika.

Hata hivyo kulingana na utafiti huo vipato vya wakulima walio wengi vilionekana kuwa vidogo na wengi wao hawana uwezo wa kuchangia viwango vya michango kulingana na Sheria ya *NSSF* bila kupata msaada kutoka vyanzo vingine.

Hivyo *NSSF* bado wanaangalia uwezekano wa kuanzisha mpango maalum *(complementary scheme)* kwa ajili ya wakulima.

Pia taarifa za tafiti kutoka katika nchi kama vile Philippines, India, China na Srilanka zinaonyesha kuwa nchi hizi zilipata matatizo katika kuingiza mpango wa hifadhi ya jamii katika sekta ya kilimo bila maandalizi ya kutosha. Baadhi ya matatizo hayo ni kama vile kushindwa kukusanya michango kutoka kwa wakulima, viwango vya michango vilivyochangwa kutotimiza masharti ya kupata pensheni na kukosekana utaratibu wa kusimamia utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa kuwa sekta isiyo rasmi na hasa kilimo inaliingizia Taifa pato la zaidi ya asilimia 70 na kwa kuwa wafanyakazi wengi ambao wanaweza kuwa wanachama wa *NSSF* kutoka katika sekta hii, *NSSF* inaendelea na jitihada zaidi ya kuangalia uwezekano wa kuiingiza sekta hii katika mpango wa hifadhi ya jamii. Hii ni pamoja na kuangalia umuhimu wa kuanzisha mfumo maalum utakaokidhi matakwa ya sekta hii.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa baada ya marekebisho ya *PPF* yamejitokeza matatizo kadhaa na mwingiliano kati ya vyombo hivi viwili vya *NSSF* na *PPF;* na kwa kuwa Serikali ilisema kwamba wataleta sera ya hifadhi ya jamii ambayo pamoja na mambo mengine ingetatua matatizo hayo na mwingiliano huo; je, Serikali imefikia wapi katika suala zima la kuleta au kutayarisha sera ya hifadhi ya jamii?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baada ya kuhuishwa kwa Sheria ile ya *PPF* kumejitokeza aina fulani ya mgongano katika utendaji kati ya *NSSF* na *PPF* lakini tatizo hili ni la muda tu kwa sababu sera anayoizungumzia Mheshimiwa Mohamed Missanga, imekamilika na ilihusisha mifuko yote ya hifadhi ya jamii pamoja na Chama cha Waajiri na Chama cha Wafanyakazi. Hivi sasa Wizara iko katika hatua za mwisho za kukabidhi sera hiyo kwenye Baraza la Mawaziri ili iweze kuandaliwa, kusahihishwa na hatimaye kufikishwa hapa Bungeni.

Na. 185

**Kupitisha Mabomba ya Maji Kwenye Mipaka ya Viwanja**

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wanapoomba kuunganishiwa maji safi kutoka kwenye bomba kubwa kupeleka nyumbani, mtaro wa kupitisha bomba la maji hupitishwa kwenye mipaka ya viwanja vya nyumba baada ya wafanyakazi wa Idara ya Maji kupima na kumwonyesha mwombaji; na kwa kuwa utaratibu huo ni kero kwa mwenye kiwanja na mwenye bomba kwa kukatiana mabomba ya maji:-

(a) Je, ni kwa nini mitaro hiyo ya kupitishia bomba la maji safi isipitishwe barabarani badala ya kwenye mipaka ya viwanja vya nyumba?

(b) Je, ni nani atakayehusika na fidia ya kukatwa kwa mabomba ama kumsumbua mwenye kiwanja?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mtandao wa usambazaji wa maji safi na uondoaji majitaka Mijini kwenye sehemu zilizopimwa chini ya taratibu za Mipango Miji umegawanyika katika sehemu kuu tatu.

Kwanza, kuna bomba kuu *(trunk-main)* linalotoa maji kutoka vyanzo, hupitishwa katika mashamba ama porini na kandokando ya barabara kuu katikati ya eneo la huduma

na pili, yapo mabomba ya usambazaji *(distribution mains)* ambayo hulazwa kando kando ya barabara kuu ya Mji katika eneo la huduma na siyo katika viwanja.

Tatu, yapo mabomba ya wateja *(service pipes)* yanayopeleka huduma katika viwanja na majumba ambayo hulazwa kando kando ya barabara kuu katika Miji katika viwanja na majumba ambayo hulazwa katika eneo la meta 3 kati ya jengo na jengo. Eneo hili huachwa wazi kutokana na Sheria ya Mipango Miji ambapo meta 1.50 zinaachwa kati ya jengo na jengo. Eneo hili pia hupitishwa huduma nyingine kama vile majitaka, simu, umeme na zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba kuu, mabomba ya usambazaji na yale ya wateja hupitishwa katika maeneo ya wazi ya huduma ambayo huachwa kandokando ya barabara Kisheria.

(b) Kulingana na Sheria ya Maji Na. 8 ya 1997, kifungu cha IV ni kosa mteja au mtu mwingine kuingilia au kukata huduma ya miundombinu ya majisafi na majitaka popote ilipowekwa Kisheria. Hivyo kwa yeyote atakayekata, kuharibu au kufanya usumbufu kwa wateja wengine atawajibishwa kwa Sheria iliyotajwa ikiwa ni pamoja na kulipa fidia.

Hata hivyo, Sheria zinaruhusu mamlaka zilizoidhinishwa Kisheria kufanyakazi katika eneo la wazi kama ilivyoelezwa hapo juu.

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa swali langu la msingi lilikuwa linahusu mabomba ya wateja au ya mtu mmoja mmoja; je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu au iweke ramani ambayo itasaidia kuondoa kero hizi za wateja za kukatiana mabomba?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kwamba mabomba haya au mitaro hii hupitishwa na watu wa Idara ya Maji, maana yake kwamba mteja anapokwenda kuomba kuwekewa bomba watumishi wa Idara ya Maji ndio wanaokuja kuonyesha bomba hilo lipite wapi. Kwa maana hiyo basi, Serikali ndiyo inayosababisha watu hawa kupata kero, mwenye kiwanja na mwenye bomba; je, Serikali iko tayari kuwachukulia hatua watumishi hawa wanaosababisha kupitisha mabomba katika eneo ambalo halihusiki kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kama nilivyoeleza ni kuwa sehemu zote zilizopangwa Kisheria kulingana na *town planning* huwa zina ramani zinazoonyesha ni wapi viwanja vitakuwepo na wapi *service* kama nilizozitaja zitapita. Kwa hiyo, nina hakika maeneo anayoyaelezea Mheshimiwa Mbunge inawezekana kabisa ni maeneo ambayo yalijengwa mwanzoni kama *squatter* halafu baadaye ndio wananchi wa sehemu hiyo kwa sababu wana haki ya kuomba service wakapatiwa *service.* Sasa kwenye maeneo kama hayo

lazima utapata matatizo kama hayo kwa sababu unajenga nyumba inaangalia choo cha mwenzako na nyumba nyingine inaangalia upande mwingine. Kwa hiyo, matatizo kama hayo ni lazima yatakuwepo. Lakini kwenye sehemu zote ambazo zimewekewa ramani kabla ya ujenzi kuanza, matatizo kama hayo hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, watumishi wa Idara husika zinazosambaza maji Mijini ndio uhusika katika matatizo kama haya. Hapo siwezi kusema ni kweli kwa sababu sina ushahidi lakini kwa maeneo yote yaliyopimwa kama nilivyoeleza, sioni kama mfanyakazi yeyote wa mamlaka yoyote atakiuka taratibu na masharti ya kazi ambayo anaielewa na ni lazima ukaguzi unafanyika mara kwa mara ili kuangalia usalama wa mita zetu kwenye sehemu ambazo kuna mita na kuangalia usalama wa bomba. Hivyo masharti yote huwa yanafuatwa.

Na. 186

**Huduma ya Simu kwa Tarafa za Mwembe-Mbaga, Gonja na Mamba-Vunta**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi walio wengi Wilayani Same wanaishi Ukanda wa Milimani ambapo usafiri wa barabara ni wa kubahatisha tu; na kwa kuwa huduma ya simu ingesaidia sana kunusuru matatizo ya wananchi kama vile ajali, ugonjwa, ujambazi na usalama wa raia na mali zao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya simu kwa maeneo yaliyoathirika ya Tarafa za Mwembe-Mbaga, Gonja, Mamba-Vunta na Vijiji vya Vumari, Didokwamomo na Bonde la Kilimo la Mto Ruvu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* ina mpango wa uboreshaji wa mawasiliano ya simu Vijijini *(Rural Automation Plan)*. Katika mpango huu Kijiji cha Mwembe kitapatiwa simu za vibandani. *(Makofi)*

Pia Vijiji vya Gonja, Ruvu Mferejini, Mamba Vunta na Vumari navyo vitapatiwa mawasiliano kwa kutumia simu za vibandani. Utekelezaji wa mpango huu utaanza baada ya hali ya kifedha ya kampuni kuimarika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa John Singo, anafuatilia sana masuala ya miundombinu ya kiuchumi katika Jimbo lake. Napenda kumhakikishia ushirikiano mkubwa kutoka Wizara yangu.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na ahadi nzuri alizozitoa, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mheshimiwa Waziri anatuahidi kwamba uwezo wa fedha utakapokuwepo basi wananchi watapata huduma ambayo nimeiomba; je, uwezo huu wa fedha utakuwepo lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Mheshimiwa Waziri atakubali kuja kutembelea katika Jimbo la Same Magharibi na kuona hali ya wananchi ilivyo na jinsi walivyoathirika kwa kukosa mawasiliano? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezo wa fedha wa kampuni utakuwepo lini au utapatikana lini? Napenda kumhakikishia kwamba Serikali pamoja na kampuni tunafanya juu chini ili uwezo wa shirika uweze ukaimarika mapema iwezekanavyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutembelea Wilaya ya Same. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa John Singo, kwamba tumwombe Mwenyezi Mungu kuwa na afya njema, nitafika Same hivi karibuni. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri kwa mantiki ya swali la msingi ya kwamba kuna maeneo ambayo hayafikiki.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami ya kwamba atakapomaliza kuitembelea Same, aje aitembelee Ukerewe katika visiwa 27 ambavyo havina mawasiliano na achukulie kama suala la dharura kabisa kuleta mawasiliano katika visiwa hivi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwamba nitajitahidi kutembelea Wilaya ya Ukerewe. Sina uhakika kama nitapitia visiwa vyote 27 lakini baadhi ya visiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukerewe ni kisiwa na kama vilivyo visiwa vingine Serikali inatilia maanani sana mawasiliano Ukerewe na ndiyo maana katika Bajeti yetu ya mwaka 2003/2004 ambayo Bunge lako Tukufu limeidhinisha tunaanzia na kutengeneza gati la Nansio. *(Makofi)*

187

**Mawasiliano ya Simu - Liwale**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa kabla ya kubinafsisha *TTCL* Serikali ilitoa ahadi ya kupeleka/kuanzisha huduma za mawasiliano ya simu Wilaya ya Liwale; na kwa kuwa baada ya kubinafsisha *TTCL* ahadi hiyo haijatekelezwa hadi sasa:-

(a) Je, ubinafsishaji wa *TTCL* ndio uliokwamisha au kuchelewesha upatikanaji wa mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Liwale; kama siyo/ndiyo ni lini Liwale itapata mawasiliano hayo ya simu na hatua gani imefikiwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kukosekana kwa mawasiliano ya simu katika baadhi ya Wilaya nchini ikiwemo ya Liwale kunaathiri juhudi za Serikali za kupeleka maendeleo karibu na wananchi kupitia Halmashauri zao?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu kikamilifu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya pili ya mpango wa maendeleo wa Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* ambao utekelezaji wake utaanza mwaka 2004 na ambao utategemea upatikanaji wa fedha, Mji wa Liwale umepangiwa kupata mtambo wa simu za kisasa wenye uwezo wa kuunganisha jumla ya wateja 300 kabla au ifikapo mwisho wa mwaka 2004. Katika awamu ya pili ya mpango huo, njia ya kisasa aina ya *digital* itaunganisha Miji ya Masasi, Nachingwea na Liwale. Ifikapo Desemba, 2003 njia inayounganisha Miji ya Masasi, Newala na Mtwara itabadilishwa kuwa aina ya *digital* na hivyo kuweza kuupatia Mji wa Tandahimba simu za kisasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa kukosekana kwa mawasiliano ya simu ya uhakika katika baadhi ya Wilaya nchini kunaathiri sana juhudi za Serikali za kupeleka maendeleo karibu na wananchi kupitia Halmashauri zao. Hii ndio sababu ya kubuni mpango wa kuboresha huduma za mawasiliano ya simu katika Makao Makuu ya Wilaya nchini kote pamoja na kuondoa simu zote za kukoroga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, amelisimamia kidete suala la simu Liwale kwa niaba ya wananchi wa Liwale. Namwomba yeye na Waheshimiwa Wabunge wengine tusichoke tuendelee kushirikiana mpaka Liwale na Miji mingine kama vile Kilwa, Mafia, Bukombe, Kandete, Ruangwa, Itigi na mingine ipate mawasiliano ya kisasa.

Na. 188

**Mradi wa Gesi *Mnazi Bay***

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME** aliuliza:-

Kwa kuwa Benki ya Dunia ilitoa fedha *USD* 15,000,000 kwa ajili ya uendelezaji wa gesi ya *Mnazi Bay;* na kwa kuwa fedha hizo hazikutumika kama ilivyokuwa imepangwa:-

(a) Je, Serikali ina maelezo gani ya sababu zilizofanya fedha hizo zisitumike katika mradi husika?

(b) Je, ni taratibu zipi za haraka zilizoandaliwa za kuendeleza mradi huo wa gesi ya *Mnazi Bay?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, swali lake lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1992 wakati wa kuandaa mradi wa umeme wa sita *(Sixth Power Project)* kwa ajili ya Mradi wa Umeme wa Kihansi, Benki ya Dunia iliweka Bajeti ya jumla ya Dola milioni 15 kwa ajili ya kuendeleza gesi ya *Mnazi Bay,* hususan kuipatia Miji ya Mtwara na Lindi umeme wa uhakika. Hata hivyo, Benki ya Dunia ilitoa masharti yafuatayo:-

(i) Fedha zingetolewa iwapo taarifa ya wataalam kuhusu upembuzi yakinifu ingethibitishwa kuwa kiuchumi ni vyema mradi huo kutekelezwa.

(ii) Upembuzi wa masuala ya mazingira uthibitishe kuwa hakutakuwepo na athari mbaya kwa mazingira na jamii; na

(iii) Endapo gharama za utekelezaji ingekuwa kubwa zaidi ya Dola milioni 15, ingebidi basi kiasi kilichobaki kipatikane kwanza kabla ya kupata idhini ya kutumia fedha za kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zote za upembuzi yakinifu kifedha, kiuchumi na athari za mazingira na jamii zilipatikana katikati ya mwaka 1994. Taarifa ya upembuzi yakinifu kifedha ilibainisha kuwa mradi wa kuendeleza gesi ya *Mnazi Bay* kuzalisha umeme utatekelezwa kwa Dola za Marekani milioni 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hiki ni mara mbili ya makisio ya Bajeti. Wizara ya Nishati na Madini ilitafuta wabia mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kampuni ya *Santa Fe, Tullow Oil, Tomado Resources, Deepak* na hivi sasa *Artumas Group* ya Canada. Benki ya Dunia iliamua kufuta Bajeti ya Mradi wa *Mnazi Bay* kwenye *Sixth Power Project* kuzihamishia kwenye maandalizi ya mradi wa kuendeleza Gesi ya Songo Songo. Badala yake kiasi chote cha Dola milioni 15 na kiasi kingine kilichopatikana katika mradi wa *TANESCO,* kilitumika kununulia mitambo ya umeme wakati wa dharura ya umeme ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maandalizi ya Mradi wa Songo Songo kuchelewa na gharama kuongezeka na mwekezaji mwenye nia ya kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha (Dola milioni 17) na kuuza umeme wa bei sawa au chini ya senti za Kimarekani 18 kwa *unit* moja, Benki ya Dunia ilijitoa kabisa katika mradi wa kuendeleza Gesi ya *Mnazi Bay.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini hivi sasa inafanya majadiliano na *Artumas Group* ya Canada. Vile vile Wizara imefanya mazungumzo na Benki ya Dunia, ambayo imekubali kujihusisha tena na mradi wa kutumia Gesi ya Songo Songo. Mpango huu wa sasa ni wa kukiwezesha Kitengo cha Umeme wa Vijijini ya Shirika la Umeme la Tanzania *TANESCO* kuwa na uwezo wa kujenga na kuendeleza mfumo wa umeme wa Somanga Funga - Lindi na Mtwara. *TANESCO* imekubali changamoto hii na itakamilisha kazi ya kuandaa upya mradi huo ifikapo Desemba, 2003. Lengo la Serikali ni kuipatia Miji na Vijiji vya Mikoa ya Lindi na Mtwara umeme wa uhakika na bei nafuu na kama mradi huu utafanikiwa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2004.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa kukamilika kwa mpango wa maendeleo wa Kanda ya Mtwara kunategemea sana kuwepo kwa umeme wa uhakika; na kwa kuwa matumaini makubwa ya kupatiwa umeme katika Kanda ya Kusini ilitegemewa Gesi ya *Mnazi Bay;* je, Serikali haioni kwamba kucheleweshwa kwa mradi huo pia kutachangia kuchelewesha kwa mpango wa maendeleo wa Kanda ya Mtwara?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa walikuwepo wawekezaji kama ilivyo kwa Kampuni ya *Deepak* ya India, ilikubali kabisa kuwekeza Mradi wa *Mnazi Bay* na ilikuwa na kamilifu lakini Serikali ilisuasua kutoa mpango wa kuendeleza Gesi ya *Mnazi Bay* kwa hiyo, Kampuni ya *Deepak;* je, sasa Serikali iko tayari kuiarifu Kampuni ya *Deepak* kuja kuiendeleza Gesi ya *Mnazi Bay?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, kwamba umeme wa uhakika ni nguzo muhimu sana kwa maendeleo si ya Mtwara na Ukanda wake tu lakini kwa hakika ni mahali popote pale katika nchi yetu. Ndio maana basi, Serikali imekuwa ikishughulika ili kuhakikisha kwamba kuna njia mbalimbali ambapo yoyote itakayofanikiwa kwa haraka na ambayo itawezesha kupatikana umeme kwa bei nafuu, basi umeme huu ufikishwe Mtwara, maeneo mengine ya Lindi na maeneo mengine ya Kusini haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatambua matatizo makubwa ya nishati yanayoikabili Mikoa hii ya Kusini na hususan Mtwara Mjini kwenyewe na ndio maana hata hivi sasa kuna *generator* mpya ambayo imenunuliwa kwa ajili ya Mtwara Mjini

yenye megawati 1.5 kwa juhudi kubwa za ufuatiliaji pia wa Mheshimiwa Mbunge. Lakini hii ni hatua ya awali tu au hatua ya muda mfupi. Hatua ya muda mrefu ni kama hii ya kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unafika ama kupitia Mradi wa Gesi ya Songo Songo au wa *Mnazi Bay* endapo majadiliano yatakamilika au hata ule wa Mchuchuma, itategemea upi ambao utaanza na utakuwa na unafuu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kweli Serikali haisuisui katika kukaribisha na kufanya majadiliano na wawekezaji mbalimbali lakini lazima Serikali iwe na uangalifu mkubwa ili isije ikalibebesha Taifa mzigo mkubwa unaotokana na mikataba ya nishati ambayo gharama zake baadaye zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakizungumzia sana juu ya gharama kubwa za mradi wa *IPTL* na ndio maana basi ni muhimu tuwe makini sana katika kuhakikisha kwamba mkataba wowote tunaoingia wa uzalishaji umeme ni ule unaoendana na dhamira kubwa ya Serikali kuhakikisha kwamba nishati hii inapatikana kwa bei nafuu.

Na. 189

**Makampuni ya Uchimbaji Madini**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imejaaliwa kuwa na madini ya aina mbalimbali; na kwa kuwa migodi na machimbo ya madini hayo yapo katika maeneo ya Halmashauri zetu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa upo umuhimu wa makampuni yanayochimba madini hayo kuchangia maendeleo ya wananchi kwa kulipa asilimia fulani kama ilivyo kwenye vitalu vya uwindaji wa wanyama ambapo Halmashauri husika hulipwa asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa wanyama kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya wananchi wa Halmashauri husika?

(b) Je, Serikali inadhibiti na kuthibitisha vipi kuhusu kiasi cha madini yanayopatikana kila siku kutokana na uchimbaji unaofanywa na Makampuni ya Uchimbaji wa madini katika machimbo na migodi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyojibu maswali Na.32; 342 na 343 katika Bunge hili katika nyakati tofauti, fedha zitokanazo na madini huingizwa katika Bajeti ya Serikali kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ya Taifa zima ambapo hata maeneo yenye madini pia hufaidika. Ni vema basi mapato yatokanayo na madini yakaendelea kuwa ni mapato ya Taifa kwa manufaa ya wananchi wote.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na uzalishaji wa madini unafanyika chini ya Kifungu cha 99 na 100 na sehemu ya kwanza ya Jedewali la tatu la sheria ya madini ya mwaka 1998. Ukaguzi unafanywa na Maofisa Madini kutoka katika Ofisi ya Madini ambayo imepewa dhamana ya usimamizi wa mgodi husika. Madini yoyote yanayozalishwa na makampuni ya uchimbaji hayawezi kusafirishwa nje ya nchi bila kukaguliwa na kupimwa uzito wake na Maofisa wa Madini na kisha vifurushi vya madini hayo kufungwa kwa lakiri *(seal).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa dhahabu, dhahabu husafirishwa nje ya nchi na wasafirishaji wa dhahabu wanaotambulika Kimataifa. Kabla ya kusafirishwa, huchukuliwa sampuli na taarifa zake kuhifadhiwa na baada ya dhahabu iliyosafirishwa kusafishwa, taarifa huletwa katika Idara ya Madini ambapo hulinganishwa na taarifa za sampuli za awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyotangaza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wakati akilihutubia Bunge wakati wa Bajeti ya Serikali, hivi karibuni Serikali itaanzisha ukaguzi *(Auditing and Assaying)* kwa dhahabu inayochimbwa na kuuzwa nchi za nje ili kuhakikisha kwamba nchi hii inapata mapato kulingana na uzalishaji unaoendelea.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

(a) Kwa kuwa wawekezaji hawa wametengeneza viwanja vya ndege sehemu zao za migodi na ndege hizo zinakuja usiku na mchana na kuondoka, je, kuna udhibiti gani ambao unafanyika kwa usiku huo ambao unatuthibitishia sisi kwamba madini yetu hayatoroshwi? *(Makofi)*

(b) Kwa nini wasiwekwe Maafisa wetu ambao wanawekwa kama kwenye viwanja vingine vya ndege ambao wanakagua ndege hizo zinapoingia na kutoka, je, Serikali haioni kuwa kutokukagua ndege hizo kunaweza kusababisha madini yetu kuondoka kuleta mengine ambayo yanaathiri vijana wetu kwa wingi hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa wasiwasi ambao Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaweza kuwa nao katika masuala ya usafirishaji madini nje ya nchi. Kwa hakika ni haki yao kuwa na wasiwasi. Lakini napenda kuchukua nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba nchi hii ina taratibu mbalimbali zinazotawala au zinazosimamia usafiri wa anga na mwingineo na pia kama nilivyosema awali zinazotawala usafirishaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najibu swali la msingi nilisema kwamba katika kila eneo la mgodi tunao Maafisa pale wa Serikali wanaohusika na udhibiti au ukaguzi wa madini. Sasa basi endapo kuna taarifa ambazo Mheshimiwa Mbunge au Waheshimiwa Wabunge wengine wanaweza wakawa nazo kinyume na ambavyo Serikali inafahamu, napenda nichukue nafasi hii kuwakaribisha Waheshimiwa hawa tushirikiane ndani ya Serikali ili kuhakikisha kwamba kama kuna matatizo ambayo sisi tunadhani kwamba hatuyafahamu basi tuweze kushirikiana nao katika kudhibiti mali hii ya Taifa.

Lakini napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kwa mujibu wa taratibu wa uendeshaji wa nchi hii zilivyo hivi sasa, tunazo taratibu za kuhakikisha kwamba mtu haingii na kutoka tu kama anavyojitakia. Hii ni nchi yenye ulinzi na usalama wa kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha. Kabla hatujaendelea kuna tangazo. Mheshimiwa Benito Malangalila, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 8 Julai, 2003 kutakuwa na kikao pamoja na mambo mengine kitajadili Mkataba wa Umoja wa Afrika dhidi ya Ugaidi. Kikao hicho kitafanyika chumba namba 54 kuanzia saa 5.00 asubuhi baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri anayewasilisha leo.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata vi-*note* vingi sana kuhusu utaratibu wa maswali ya nyongeza. Kila nikipata ki-*note* ananiambia hakuna ruksa ya kusoma, mwambie asisome, vi-*note* vya namna hiyo.

Sasa nimesema ni vizuri niwakumbushe Kanuni ya 36(3) inasema: “Isipokuwa kama Spika ataelekeza vinginevyo, Wabunge watakaouliza maswali ya nyongeza hawatazidi watatu kwa swali moja la msingi na Mbunge hataruhusiwa kusoma swali lake.”

Sasa ukikaa hapa unapomwona Mbunge ameinama unajua anataka sauti yake isikike kwenye *Microphone* sasa namna ya ku-*check* kama anasoma inakuwa ngumu kidogo. Kwa hiyo, jirani kama umekerwa kidogo basi utasimama kuhusu utaratibu, utasema kanuni ili kunisaidia.

Baada ya matangazo hayo, Katibu *agenda* inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
### Wizara ya Elimu na Utamaduni

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, likae kama Kamati ya Matumizi ili liyapitishe Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawapongeza na kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa hotuba yake ambayo imetoa kwa ufasaha tathmini, mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa Taifa kwa ujumla na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yake iliyofafanua kwa ufasaha mkubwa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004 ambayo imetoa kipaumbele kwa sekta muhimu katika kukuza uchumi ikiwemo sekta ya elimu ambayo inayo wajibu mkubwa katika mkakati wa kupunguza umaskini na katika kuboresha ufanisi wa nguvu kazi ya Taifa kwa njia ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Huduma za Jamii, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge mashuhuri wa Babati Mashariki, kwa kuichambua kwa kina Bajeti ya Wizara yangu na kunipa ushauri wa kuiboresha na kwa kuiunga mkono ipitishwe na Bunge hili heshimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2002/2003, Wizara ya Elimu na Utamaduni, imeendelea kuwa na majukumu saba ambayo ni kwanza, Elimu ya Msingi na Elimu ya awali, pili, Elimu ya Sekondari ya Kawaida (Kidato cha 1 hadi cha 4) na Elimu ya Sekondari ya Juu (Kidato cha 5 hadi cha 6) na tatu, Elimu Maalum *(Special Education)* itolewayo kwa wenye ulemavu kama vile wasioona, viziwi, wenye ulemavu wa akili na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Elimu ya Watu Wazima *(Adult Education)* ikiwa ni pamoja na utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari kwa mfumo usio rasmi kwa watoto na watu wazima walioikosa, tano, Utamaduni wa Taifa ikiweko Lugha, Sanaa, Mila na Desturi na Ukaguzi wa filamu, sita, ni mafunzo ya Ualimu wa Daraja A na Stashahada *(Diploma)* na saba, kusimamia Taasisi, mabaraza na mashirika yaliyo chini ya Wizara ambao ni:-

(a) Tume ya Utumishi wa Walimu *(TUW);*
(b) Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET);*
(c) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima *(TEWW);*
(d) Baraza la Mitihani la Taifa *(BAMITA);*
(e) Baraza la Kiwahili la Taifa *(BAKITA);*
(f) Baraza la Sanaa la Taifa *(BASATA);* na
(g) Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania *(BOHUMA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara inaongozwa na sheria ya Elimu namba 25 ya 1978 pamoja na sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, sera ya Utamaduni, dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, mkakati wa kupunguza umaskini na Ilani ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 ya Chama Tawala cha CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakiki ubora wa elimu itolewayo katika shule zote nchini, Wizara huendesha ukaguzi wa shule na hutoa mitihani ya Kitaifa ya Darasa la IV na Darasa la VII na Vidato vya 2, 4 na 6 kupitia Baraza la Mitihani la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Wizara imeandaa dira na dhima yake. Pamoja na maamuzi ya kisera yaliyomo katika nyaraka nilizozitaja, Wizara inatoa kipaumbele katika utekelezaji wa malengo maalum katika ngazi mbalimbali yanayozingatia upanuaji na uboreshaji wa elimu.

Malengo maalum ya Elimu ya Msingi ni kwanza, kurejesha *Universal Primary Education (UPE )* yaani Elimu ya Msingi kwa wote kwa kuingiza darasa la kwanza kila mwaka watoto wote wa miaka 7 na kuwaendeleza mpaka wahitimu Darasa

la VII kwa kuzingatia Kifungu Na.35 cha Sheria ya Elimu Na.25 ya 1978 kama kilivyorekebishwa na Sheria Na.10 ya 1995.

Pili, kuongeza idadi ya watoto wenye umri wa miaka 7-13 katika Elimu na Msingi kutoka asilimia 57 mwaka 2001 hadi asilimia 70 mwaka 2003, tatu, kuongeza idadi ya watoto wote walioko shuleni kwa asilimia ya rika lengwa (miaka 7-13) yaani *Gross Enrolment Ration (GER)* kutoka asilimia 78 mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 85 mwaka 2003 katika kila Shule, Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na katika ngazi ya Taifa na nne, kupunguza kasi ya kuacha shule *(Drop Out Rate)* kutoka asilimia 6.6 kwa mwaka hadi asilimia 3.0 kwa mwaka ifikapo 2005 katika kila shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kuboresha Elimu ya Msingi kutoka waliofaulu asilimia 22 mwaka 2000 hadi zaidi ya asilimia 50 mwaka 2005 na sita, kuongeza wahitimu wa Darasa la VII wanaoingia Sekondari kutoka asilimia 19.5 mwaka 2001 hadi asilimia 21 mwaka 2003 na kufikia zaidi ya asilimia 50 mapema iwezekanavyo baada ya hapo.

Malengo maalum ya Elimu ya Sekondari ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kupanua Elimu ya Sekondari kutoka kupokea asilimia 19.5 mwaka 2001 hadi asilimia 21 mwaka 2003 ya wahitimu wa darasa la VII wa kila mwaka na baada ya hapo hadi zaidi ya asilimia 50 ifikapo mwaka 2015 na pili, kuongeza nafasi ya utoaji Elimu ya Sekondari kwa rika la Elimu ya Sekondari (miaka 14-17) kutoka asilimia 7 ya sasa hadi kufikia asilimia 30 ifikapo 2015.

Tatu, kuboresha Elimu ya Sekondari kwa kuongeza asilimia ya wanaofaulu mitihani ya Kitaifa ya Kidato cha 4 na 6 katika madaraja I, II na III kutoka asilimia 25 mwaka 2001 hadi zaidi ya asilimia 50 fikapo 2003, nne, kutoka Elimu ya Sekondari kwa usawa kwa Mikoa na Wilaya zote kwa kuzingatia maelekezo ya kifungu 11(3) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachosema: "Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo."

Malengo Maalum ya Mafunzo ya Ualimu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuandaa Walimu wa ngazi ya Cheti Daraja A na Stashahada ili kukidhi mahitaji kwa shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, pili, kuboresha mazingira ya kutolea mafunzo katika Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu kwa kutoa vifaa bora vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia, tatu, kuimarisha Vituo vya Walimu yaani *Teachers Resources Centres (TRCs)* katika ngazi ya Wilaya, Kanda na Taifa, nne, kuboresha taaluma na utaalamu wa ufundishaji wa masomo ya Shule za Msingi hususani kwa kuwapatia mafunzo maalum ya Daraja A kazini *(In-Service Grade A)* Walimu wote wa Daraja B/C na kuwatahini katika masomo ya Elimu ya Msingi ili wafaulu katika Daraja lisilo chini ya B na tano, kupanua mafunzo ya Walimu sambamba na upanuaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo maalum ya maendeleo ya utamaduni ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kupanua kiwango cha wananchi katika kushiriki shughuli za utamaduni, kuboresha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za utamaduni, kuimarisha Elimu na Mafunzo ya Fani za Utamaduni, kuimarisha na kukuza Tasnia na Miundombinu ya Utamaduni, kulinda na kuimarisha Maadili na Utambulisho wa Taifa na kuimarisha Ushirikiano wa Kimataifa katika Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mipango ya Wizara yangu kwa mwaka 2002/2003 na malengo ya mwaka 2003/2004 kwa kila Idara, Taasisi na ngazi ya elimu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha elimu ya Msingi ni lazima kuanzia na Elimu ya Awali kwa watoto wa miaka 5-6. Katika mwaka 2002/2003, zilianzishwa Shule za Awali na Serikali 1,687. Idadi ya watoto katika Elimu ya Awali imeongezeka kutoka watoto 313,310 mwaka 2002 hadi 744,750 mwaka 2003. Hili ni ongezeko la watoto 431,440 sawa na asilimia 138. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa ili kufikia lengo la kuwa na darasa la awali katika Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003 kumekuwa na ongezeko la Shule za Msingi za Serikali 497 sawa na ongezeko la asilimia 4 kufikia shule 12,649 Aidha, idadi ya wanafunzi wa Shule zote za Msingi imeongezeka kutoka 5,972,077 (2002 hadi 6,562,772 (2003). Hili ni ongezeko la asilimia 10. Walimu 13,050 wameongezeka sawa na ongezeko la asilimia 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mwaka wa pili wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002-2006 ambao lengo kuu ni kurejesha Elimu ya Msingi kwa wote ifikapo mwaka 2005, mafanikio ya utekelezaji kwa mwaka wa pili ni kama ifuatavyo:-

Lengo la kuandikisha watoto 1,600,000 darasa la kwanza halifikiwa. Watoto walioandikishwa ni 1,481,354 sawa na 93 kwa sababu wengine waliopangwa mwaka wa pili walijipenyeza mwaka wa kwanza ndio maana hatukufikia asilimia 100. Jumla ya wanafunzi katika Shule zote za msingi mwaka 2003 ni 6,562,772 ikilinganishwa na 5,972,077 mwaka 2002 ambalo ni ongezeko la wanafunzi 590,695 sawa na asilimia 9.9

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na takwimu zilivyooneshwa hapo juu idadi ya watoto wote walioko shuleni kama asilimia ya idadi ya watoto wa rika lengwa *(Gross Enrolment Ratio (GER)* imeongezeka kutoka asilimia 98.6 mwaka 2002 hadi kufikia asilimia 105.3 mwaka 2003. Kwa hiyo, malengo yaliyomo katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini *(MKU)* ifikapo mwaka 2003 ya *NER* ya 77% na *GER* ya 85% yamevukwa.

Idadi ya watoto wa rika la Elimu ya Msingi (miaka 7-13) walioko shuleni *(Net Enrolment Ration - NER)* imeongezeka kutoka asilimia 80.7 mwaka 2002 hadi kufikia asilimia 88.5 mwaka 2003.

Mikoa 16 imefikia *GER* ya asilimia 100 au zaidi. Mikoa mitano ya Rukwa (96.9%), Mtwara (95.8%), Tabora (87.8%), Dodoma (87.5%) na Lindi (85.2%) haijafikia kiwango cha *GER* ya asilimia 100 ambayo ni hatua ya lazima ingawaje si ya kutosha ya kufikia Elimu ya Msingi kwa Wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu 10,719 wameajiriwa hadi Mei, 2003 sawa na asilimia 92 ya lengo la 11,651 la MMEM. Bado ziko nafasi za ajira ya Walimu 932. Kuanzia mwaka huu, Walimu kutoka Vyuo vya Ualimu waliofaulu wanaajiriwa moja kwa moja na hakutakuwa na Mwalimu anayesubiri ajira isipokuwa kama anachagua mahali pa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu Tarajali wa daraja 3A wanaochukua mafunzo ya Ualimu wameongezeka kutoka 7,254 mwaka 2002 hadi 11,290 mwaka 2003. Hili ni ongezeko la asilimia 55.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasimu ya kwanza ya mitaala mipya ya Elimu ya Msingi inayolenga kuboresha elimu imefikia hatua ya kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya shilingi 62,326,238,096 ya ruzuku ya maendeleo imetolewa kwa Halmashauri katika mafungu matatu kwa ajili ya ununuzi wa madawati 107,007 na ujenzi wa majengo ya shule za Msingi yakiwemo madarasa 13,396 na nyumba za Walimu 7,732. Fungu la kwanza lilitolewa Novemba 2002, jumla ya shilingi 3,210,220,028 zilitumwa kwa Halamshauri.

Aidha, Fungu la Pili shilingi 11,801,400,000.00 zilitolewa Desemba 2002; na Fungu la Tatu shilingi 48,705,308,700 zitatolewa baada ya mwaka huu wa fedha. Mchanganuo wa ruzuku hiyo umeonyeshwa katika nyongeza A katika kitabu maalum kinachogawanywa pamoja na Bajeti hii.

Katika juhudi ya kuongeza idadi ya vitabu vya kiada na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia, Serikali na wahisani wameshatoa jumla ya shilingi 32,193,727,772.2 ambazo zimetolewa kwa Halmashauri hadi kufikia Julai, 2003. Hii ni sawa na shilingi 4,925.00 kwa kila mwanafunzi. Fedha iliyobaki kufikia Dola kumi inatumwa mwezi huu wa Julai.

Fungu la Uwezeshaji *(Capacity Building)* jumla ya shilingi 2,821,050,125 zimetumwa kwa Halmashauri na Mikoa kwa ajili ya ngazi ya Halmashauri shilingi 700,000,000, ngazi ya Kata shilingi 240,000,000, gazi ya Mkoa shilingi 60,000,000 na mafunzo ya Kamati ya Shule shilingi 1,471,050,125 na Ukaguzi wa Shule shilingi 350,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi mingine ya Elimu ya Msingi uliendelea kama ifuatavyo:-

Mradi wa Lishe Shuleni, mradi huu unaendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Mpango wa chakula Duniani yaani *World Food Programme (WFP)* na utaendelea 2002-2006 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma Vijijini, Singida Vijijini na Manyara ambapo Wilaya 10 zipo katika mpango huu. Lengo la mpango huu ni kuwasomesha watoto wa makundi maalum ya wahamaji kama vile wafugaji na wanaoishi kwa kuwinda nyama pori, kula matunda pori na kurina asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya za mradi wa Lishe Shuleni ni Monduli; Ngorongoro; Simanjiro; Kiteto; Dodoma; Kondoa; Mpwapwa; Singida; Iramba na Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya shule 216 zinanufaika na mpango huu zikiwemo 9 za bweni na 207 za kutwa. Aidha, jumla ya wanafunzi 94,163 wananufaika na mpango huu. Kati ya hao wavulana ni 49,921 na wasichana ni 44,242.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa shule zenye mazingira yanayomjali mtoto *(Child Friendly School Project (CFS)* unatekelezwa katika Wilaya 11 zifuatazo Kisarawe; Masasi; Songea Vijijini; Musoma Vijijini; Ngara; Magu; Mufindi; Hai; Ilala; Kinondoni na Temeke. Hatua ya utafiti wa awali *(Baseline Survey)* umefanyika na kukamilika katika Wilaya 5 nazo ni Kisarawe; Masasi; Songea Vijijini; Musoma Vijijini na Ngara kwa kutumia fedha za wahisani wa *UNICEF.* Aidha, katika kila Wilaya zilibainishwa shule 20 za mradi, zenye maendeleo mazuri, wastani na hafifu. Kwa hali hiyo, shule 110 zitafaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa uboreshaji wa elimu ngazi ya kata *(UBEKA)* au *Ward Based Education Management (WABEM)* unatekelezwa katika Wilaya sita zifuatazo Kisarawe, Masasi, Hai, Musoma Vijijini, Mufindi na Songea Vijijini.

Semina za awali katika ngazi ya Kata zilikwishafanyika. Katika gharama za awali mradi ulikadiriwa kutumia Dola za Kimarekani 1,189,553 ambazo zimetolewa kwa uhisani wa *UNICEF.* Kwa makubaliano ya *UNICEF* na Wizara shughuli hizi zitakwenda kwa pamoja na mradi wa Shule zenye mazingira yanayomjali mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa utafiti wa hali halisi ya shule *(School Mapping)* umepanuliwa kutoka Halmashauri 82 mwaka 2002 kufikia Halmashauri 98 ilipofika Juni, 2003 ambayo ni asilimia 82 ya Halmashauri zote nchini.

Halmashauri zilizofanyiwa *school mapping* ni Kisarawe, Bagamoyo, Kibaha, Morogoro Vijijini, Serengeti, Musoma Vijijini, Magu, Bunda, Tarime, Ngara, Kyela, Mbarali, Chunya, Morogoro Mjini, Mtwara Vijijini, Mtwara Mjini, Tunduru, Newala, Mbeya Mjini, Songea Mjini, Mbinga, Masasi, Tandahimba, Mafia, Mufindi, Kibondo, Hai, Makete, Bariadi, Manyoni, Kilombero, Geita, Iringa Vijijini, Kilosa, Mkuranga, Misungwi, Ulanga, Ileje, Meatu, Ukerewe, Rufiji, Kinondoni, Ilala, Temeke, Arusha

Mjini, Babati, Dodoma Mjini, Iringa Mjini, Bukoba Vijijini, Moshi Mjini, Lindi Mjini, Musoma Mjini, Mwanza Jiji, Kahama, Shinyanga Vijijini, Shinyanga Mjini, Tabora Mjini, Tanga Mjini, Simanjiro, Kongwa, Nkasi, Sikonge, Tabora Vijijini, Karatu, Mbulu, Njombe, Bukoba Mjini, Muleba, Kigoma Mjini, Sumbawanga Mjini, Maswa, Singida Mjini, Nzega, Pangani, Rombo, Mwanga, Bukombe, Arumeru, Moshi Vijijini, Ruangwa, Karagwe, Sengerema, Kasulu, Kigoma Vijijini, Sumbawanga Vijijini, Mpanda, Mbozi,Mbeya Mjini, Songea Mjini, Korogwe, Muheza, Handeni, Kilindi, Liwale, Nachingwea, Lindi Vijijini, Rungwe na Lushoto.

Aidha, Halmashauri 16 zitakuwa zimefanyiwa Mipango ya Elimu *(Microplans)* ifikapo Novemba 2003 na kufanya jumla ya Halmashauri 69 kuwa na mipago ya elimu *(Microplans)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zitakazokuwa zimefanyiwa *microplans* Novemba 2003 ni Kasulu, Kigoma Vijijini, Sumbawanga Vijijini, Mpanda, Mbozi, Mbeya Mjini, Songea Mjini, Korogwe, Muheza, Handeni, Kilindi, Liwale, Nachingwea, Lindi Vijijini, Rungwe na Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa madarasa, mwaka 2002/2003 kutokana na uhisani wa Serikali ya Japan yamejengwa madarasa 172, Ofisi za Walimu 7 na matangi ya maji 12 katika shule 12 za Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni au mkoa wa Shinyanga madarasa 250.

Shule zilizojengewa madarasa Mkoa wa Dar es Salaam ni Kinyerezi, Tabata, Ukonga, Kiwalani, Tandale Magharibi, Kunduchi, Mburahati, Kawe, Mbagala, Ufukoni, Yaleyalepuna na Vijibweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, 2003/2004 ni mwaka wa tatu wa utekelezaji wa MMEM ambao una malengo yafuatayo:-

Kwanza, kujenga madarasa mapya 14,203 kwa kutumia fedha za wahisani na Serikali itatoa ruzuku ya maendeleo ya shilingi 55,391,000,700.00 kwa Halmashauri za Wilaya, miji na Manispaa katika ujenzi wa madarasa.

Pili, kuandikisha darasa la kwanza Januari 2004 watoto 1,640,969 wenye umri wa miaka 7 na waliobakia wa miaka 8 na 9 wa mwaka jana na kutoa ruzuku ya uendeshaji ya Dola kumi kwa mwanafunzi.

Tatu, kujenga nyumba za Walimu 8,197 hasa vijijini ili ziwe vivutio kwa Walimu kwenda kufudisha katika shule za vijijini. Mchango wa Serikalini katika ujenzi wa nyumba hizo ni Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 12,086,000,000 kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa.

Nne, kuajiri Walimu wapya 10,563 li kukabili ongezeko kubwa la uandikishaji watoto darasa la kwanza na tano, kuongeza nafasi za mafunzo tarajali ya Walimu wa Daraja la A katika Vyuo vya Ualimu kutoka 9,000 mwaka 2002/2003 hadi 11,290 mwaka

2003/2004 kwa lengo la kukabili ongezeko la mahitaji ya Walimu kutokana na ongezeko la wanafunzi katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kujenga majengo ya maliwato ya kutosha kwa kila shule na kujenga matangi ya kukusanya maji ya mvua katika shule zenye upungufu wa maji, saba, kutekeleza Mpango wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) nje ya mfumo rasmi wa shule na nane, kuendeleza uwiano wa kitabu kwa wanafunzi watatu (1:3) kwa vitabu vya kiada vya kufundishia na kujifunzia kukidhi ongezeko la wanafunzi ili hatimaye kufikia hadi kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1) ifikapo mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 ili kuziwezesha Halmashauri kutekeleza malengo hayo zimetengwa jumla ya shilingi 250,080,590,800. Kati ya hizo shilingi 104,367,638,900 zikiwa katika Fungu 56 ambalo limeombewa na mwenzangu mwenye dhamana ya TAMISEMI; zitakazopelekwa kwenye Halmashauri shilingi 107,781,000,000 ambazo baadhi yake zitatumika kwa ruzuku ya uendeshaji na maendeleo na shilingi 37,931,951,900 zinazombwa na Wizara yangu kwa ajili ya MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003/2004 kutokana na uhusiano na Serikali ya Japan yatajengwa katika Mkoa wa Dar es Salaam madarasa 71, Ofisi za Walimu 7, matangi ya maji 15, katika Shule za Msingi 15 za Manispaa ya Ilala, Temeke na Kinondoni Shule zitakazonufaika ni Boma, Mchikichini, Gongo la Mboto, Msongola, Mvuti, Kimara, Uzuri, Mbezi, Mabibo, Mwananyamala B, Azimio, Sokoine, Madenge, Rangi Tatu na Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002/2003, Idara ya Elimu ya Sekondari ilikuwa na mafanikio yafuatayo:-

Shule za Sekondari ziliongezeka kwa asilimia 6 toka shule 1,024 mwaka 2002 hadi 1,083 mwaka 2003. Wanafunzi wa Kidato cha 1-4 waliongezeka kwa asilimia 10 kufikia 319,487 ambao ni sawa na asilimia 10.2 ya rika lengwa (miaka 14-17). Ngazi hii ya elimu inakisiwa kuwa na watoto 3,138,360 wa rika lengwa kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, watahiniwa waliofaulu mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV katika Daraja la I-III katika Sekondari za Serikali wameongezeka kutoka 5,285 (asilimia 35) hadi 6,212 (asilimia 45) na Sekondari zisizo za Serikali (ukiondoa Seminari) kutoka 4,922 (asilimia 28) hadi 6,339 (asilimia 38).

Mheshimiwa Naibu Spika, watahiniwa wa Kidato cha 4 waliotimiza masharti ya kuingia Kidato cha 5 walikuwa 17,077 kulinganisha na 13,448 wa mwaka uliopita lakini waliopata nafasi Sekondari za Serikali walikuwa 10,397 sawa na asilimia 61. Watahiniwa 6,680 sawa na asilimia 39 walikosa nafasi na wameshauriwa kuomba nafasi katika Sekondari zisizo za Serikali au katika Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi 10,397 wanaingia Kidato cha 5 katika Shule za Serikali ni ongezeko la wanafunzi 935 ambao ni asilimia 10 kuliko mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkondo mipya ya Kidato cha 5 imenzishwa katika Sekondari za Dodoma, Mwika, Chato, Tarekea, Pamba na Bihawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule zinazotoa Elimu ya Sekondari ya Juu zimeongezeka kutoka 183 hadi 190 na zina wanafunzi 25,954 ambao ni asilimia 1.7 ya watoto wa Rika Lengwa (miaka 18-19) kwa ngazi hii ya elimu wanaokisiwa kuwa 1,521,663 kutokana na takwimu za awali za sensa ya watu ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uhisani wa Serikali ya Japan shule za Serikali 10 zifuatazo zimekarabatiwa, Kibao, Mgololo, Sadani, Mwaya, Isagenhe, Kiteto, Kabanga, Ngara, Rugambwa na Kiluvya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni taarifa fupi ya miradi mbalimbali iliyotekelezwa na Wizara yangu kwa lengo la kuboresha elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sayansi *(Science Education for Secondary Schools - SESS)* ulitoa mafunzo ya mbinu bora za kufundisha masomo ya Sayansi na Hisabati kwa walimu 322. Kazi mahsusi zilizofanywa na mradi huo katika kipindi hiki ni kutoa mafunzo kwa wawezeshaji *(trainers)* 124, walimu 159 walipatiwa mafunzo mahali pa kazi *(cluster workshop)* katika Mikoa ya Iringa, Dodoma, Pwani, Mara, Mwanza na Kagera, walimu 24 kutoka Mikoa ya Dodoma, Pwani na Iringa walipatiwa mafunzo ya kufunidisha mada za *HIV/AIDS* na walimu 15 walipata mafunzo ya kuandaa kambi ya Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kugharamia elimu ya Sekondari kwa Wasichana *(Girls Secondary Education Support - GSES) Project* ambao wazazi wao hawana uwezo wa kumudu gharama za karo na mahitaji mengine ya shule uligharimia jumla ya wasichana 3,583 kama ifuatavyo:-

(a) Wanafunzi 3,381 wa kidato cha 2 - 4;
(b) Wanafunzi 50 wa kidato cha 5 - 6; na
(c) Wanafunzi 43 wa *VETA* na 109 wa vyuo vya ualimu wa daraja la A.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *Education II* uliendelea na ujenzi wa maabara za masomo ya Sayansi katika Shule za Sekondari 36 za Serikali zilizojengwa na wananchi. Ujenzi wa maabara katika shule hizo unafanywa kwa awamu tatu kama ifuatavyo:-

(a) Awamu ya kwanza Shule 12 ambazo ni Kilangalanga, Matola, Igunga, Kaliua, Chalao, King'oti, Nangwanda, Kitomondo, Mbinga, Mogabiri, Manga na Maganga.

(b) (i) Shule 12 awamu ya pili ambazo ni Oldonyosambu, Mnyambe, Lukuledi, Mkongo, Kizwite, Mambwe, Malagarasi, Bugagi, Chato, Mnyonga, Kijota na Gallapo.

(ii) Shule 12 awamu ya tatu ambazo ni Kongwa, Matekwe, Mitole, Mwaya, Meatu, Mahiwa, Mbekenyera, Bwisya, Runzewe, Zingibari, Kyela na Makiba.

Wanafunzi 4,720 sawa na asilimia 78.4 ya walengwa 6,019 hadi 10 Juni 2003 walikuwa wamelipiwa gharama za sekondari kutokana na ruzuku maalum ya Serikali ya shilingi bilioni 1.1 iliyotolewa kulipia gharama za sekondari kwa watoto wa familia maskini. Waliobaki walihimizwa kukamilisha taratibu husika kabla ya 30 Juni, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupanua elimu ya sekondari kwa makundi maalumu, Sekondari ya Balang'dalalu katika Wilaya ya Hanang Mkoa wa Manyara imebadilishwa kuwa ya Bweni kwa ajili ya kuwahudumia watoto wa wafugaji. Aidha, idadi ya wasichana wanaoingia sekondari imeongezeka na kuboresha uwiano wa wasichana kwa wavulana kutoka 1:0:87 mwaka 2002 kufikia 1:0:93 mwaka 2003 imebakia tu 1:0:07 ili kuwepo uwiano wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya mwaka 2003/2004 ni kujenga madarasa mapya 48 katika shule 6 zilizopo, shule za sekondari za Serikali kuongeza wanaofaulu kidato cha 4 daraja I, II, III kutoka asilimia 45 hadi zaidi asilimia 50 mwaka 2003, kuanzisha mikondo mipya 6 katika sekondari za juu, kukamilisha ujenzi wa maabara katika Sekondari 12 za awamu ya tatu ya Mradi wa Pili wa Elimu na kuzipatia samani na vifaa vya maabara sekondari 36, kukarabati shule 30 za Sekondari za Serikali na kuzinunulia Sekondari 306 vitabu 382,000 vya Sayansi na Hisabati, kutoa mafunzo kazini kwa Walimu 270 na mafunzo ya kinga dhidi ya Ukimwi na magonjwa ya zinaa kwa shule 200, kuajiri walimu 1,780 na watumishi wasio Walimu 333, kugharamia Elimu ya Sekondari jumla ya wasichana 4,506 na kukamilisha na kuanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* 2004 - 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja kubwa kuiboresha *Pyramid* ya elimu ya sasa kwa watoto wanaohusika ambao katika Elimu ya Msingi ni asilimia 88, Elimu ya Sekondari ya Kawaida asilimia 7, Elimu ya Sekondari ya Juu asilimia 1.8 na Elimu ya Juu chini ya asilimia 1 ya rika lengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni makini, tutahitaji kama jambo la haraka sana kuwa na *Pyramid* ya elimu inayofaa zaidi itakayokuwa na watoto wa rika husika katika Elimu ya Msingi asilimia 100, Elimu ya Sekondari ya Kawaida angalau asilimia 50, Elimu ya Sekondari ya Juu asilimia 25 na Elimu ya Juu tulenge asilimia 12.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuelekea kwenye *Pyramid* hiyo inayofaa zaidi Wizara kwa uhisani wa Benki ya Dunia inakamilisha mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Sekondari *(National Strategy for Secondary Education)* ambayo ni hatua muhimu katika kukamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (2004-2009).

Aidha, mapendekezo ya Wizara yangu kuhusu malengo na maelekezo ya *MMES* yako Serikalini kwa uamuzi wa mwisho wa kabineti. Baada ya hapo, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* utakamilishwa kupitia Kamati ya maendeleo ya Elimu ya Msingi *(Basic Education Development Committee- BEDC)* kwa ushirikiano wa wadau wote wa elimu wakiwemo washiriki wetu wa maendeleo ya elimu. Mpaka sasa upanuzi wa Elimu ya Sekondari umekuwa kwa utashi wa wanaohitaji *(Demand Driven)* ndiyo maana katika Sekondari zaidi ya 1,000 tulizonazo nchini zilizojengwa na Serikali ni 66 tu ambazo ni asilimia 6.3. *MMES* 2004 - 2009 utakuwa ni mpango wa Serikali wa makusudi wa kupanua Elimu ya Sekondari kwa faida ya maendeleo ya nchi na kwa usawa wa Kiwilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003 Idara ya Elimu ya Ualimu ilitoa mafunzo kwa walimu tarajali waliofaulu 8,989 wakiwemo 7,067 wa daraja la A kwa ajili ya MMEM, walimu wawezeshaji 763 wa mafunzo kazini ya kuendeleza walimu wa B/C kufikia Daraja la A *(Inservice Grade)* yaliyoanza June 2003 kwa Walimu 50,000 wa Daraja B/C na walimu 16 ambao hawajasomea taaluma ya Ualimu kwa kuwalipia mafunzo ya Stahashada ya Uzamili katika Elimu *(Post Graduate Diploma in Education).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004 wanachuo tarajali 13,100 wa Daraja A na 3,500 wa Stashahada watajiungana mafunzo ya Ualimu. Aidha, walimu 600 wa Shule za Msingi wa Daraja 3A watapatiwa mafunzo kazini katika fani maalumu na mafunzo kazini yatapanuliwa kwa Walimu 50,000 wa Daraja B/C ili wapande kuwa *In-Service Grade A.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003 Idara ya Ukaguzi wa Shule ilikagua jumla ya asasi za elimu 18,899 sawa na asilimia 108 ya lengo la mwaka. Katika kuboresha kazi ya ukaguzi wa Shule, Wizara imeanunua magari mawili na iliendesha mafunzo ya awali ya ukaguzi kwa Wakaguzi wa shule wapya 127.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli ziangine zinazofanyika ni pamoja na kutoa chapisho "FAHAMU ELIMU" Na. 5 kuhusu somo la Fizikia, utafiti kuhusu maendeleo ya ufundishaji wa somo la Hisabati, kuendesha warsha ya masomo ya sayansi, Hisabati na Biashara kwa wakaguzi wa elimu ya sekondari na kuendesha warsha za masomo ya Hisabati, Stadi za Kazi na Sayansi kwa Wakaguzi wa Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, Idara imepanga kufanya ukaguzi wa asasi mbalimbali za elimu 19,262. Aidha, Idara itaandaa jarida la FAHAMU ELIMU Na. 6 kwa ajili ya somo la Kiswahili ngazi ya Sekondari Vyuo na vya Mafunzo ya Ualimu. Lengo la jarida hili ni kutathmini ufundishaji wa kujifunza somo la Kiswahili ili kuwezesha wadau kujua hali halisi ya maendeleo ya somo hilo, pia Idara itanunua magari 2 ili kuboresha ukaguzi wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza mambo kumi kama ifuatavyo: -

(a) Ilifanya utafiti wa kubaini mila na desturi zinazoweza kutumiwa katika kudhibiti kasi ya maambukizi ya UKIMWI kwa Mikoa ya Lindi na Mbeya.
(b) Iliorodhesha mila na desturi mbalimbali zinazochangia maambukizi ya Ukimwi.

(c) Iliendesha mradi wa sanaa kwa wanafunzi wa Shule za Msingi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Aidha, Idara iliendesha Mradi wa TUSEME katika shule 21 za Sekondari za Wasichana.

(d) Iliendesha mashindano ya uandishi wa hadithi kwa vijana.

(e) Iliendesha mkutano na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kuhusu ukarabati wa majengo ya Chuo Cha Sanaa Bagamoyo, upanuzi na uboreshaji wa program za mafunzo ya Chuo.

(f) Iliendesha Tamasha la Sanaa la Ishirini na Moja la Bagamoyo lililoshirikisha wasanii wa nje na ndani ya nchi.

(g) Ilitoa mafunzo ya Stashahada kwa wanafunzi 67 na mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 200 katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo.

(h) Iliandaa mkutano wa wataalam kutoka nchi za Afrika Mashariki kuhusu uimarishaji wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo.

(i) Iliandaa mpango wa kuendesha mashindano ya kupata vazi la Taifa la Tanzania.

(j) Ilitayarisha tamthiliya inayoitwa Natala.

Mheshimiwa Naibu Spika, fanikio kubwa la Idara hii ni muziki wa Kitanzania kuzidi kushamiri katika Vyombo vyetu vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni itatekeleza mambo tisa kuhusu utafiti wa mila na desturi, maonesho ya utamaduni na mafunzo ya utamaduni yafuatayo: -

(a) Itaendesha mkutano mkuu wa sekta ya utamaduni.

(b) Itakusanya takwimu muhimu za utamaduni pamoja na utafiti wa mila na desturi katika Mikoa kumi.
(c) Itaendesha mashindano ya vazi la taifa kwa wanawake na wanaume.

(d) Itabaini tasnia za utamaduni zinazofaa kukuzwa na kuandaa mkakati wa kuziimarisha.

(e) Itatathmini mafunzo ya fani za utamaduni yanayotolewa na asasi za mafunzo na kuandaa utaratibu wa uwiano na viwango vinavyokubalika.

(f) Itaendesha programu za sanaa kwa wanafunzi wa shule za msingi 70 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro pamoja na programu ya TUSEME kwa shule za sekondari 23 za Mikoa 19 ya Tanzania Bara.

(g) Itaendesha mafunzo ya *diploma* kwa wanafunzi 80 na mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 250

(h) Itaendesha Tamasha la 22 la sanaa Bagamoyo.

(i) Itaendelea kutoa misaada kwa miradi mbalimbali ya utamaduni kupitia Mfuko wa Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Idara ya Utawala na Utumishi ilishughulikia masuala mbalimbali ya wafanyakazi 2,854 ikiwemo ajira za walimu wapya 1,923 wa Shule za Sekondari na Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu na Watumishi wasio Walimu 55.

Aidha, jumla ya watumishi 436 walipata mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2003/2004, Wizara inatarajia kuomba kibali cha ajira mpya ya Watumishi 1,366 wa kada mbalimbali. Pia, katika jitihada za kujenga uwezo wa Watumishi, Wizara itapeleka Watumishi 172 kwenye mafunzo ya muda mrefu na 66 ya muda mfupi ndani na nje ya nchi

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Wakala wa Maendeleo ya Menejimenti ya Elimu *(Agency for the Development of Education Management - ADEM - Bagamoyo),* walitoa mafunzo ya menejimenti na utawala kwa viongozi watendaji wa elimu wa ngazi mbalimbali 417. Katika mwaka 2003/2004 Chuo cha *ADEM* kitatoa mafunzo mbalimbali kwa Viongozi watendaji wa elimu 8,738 pamoja na stadhahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanachuo 170. Aidha, kitakamilisha vitini vya mafunzo ya uongozi kwa ajili ya Maafisa Elimu Wilaya na Walimu wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Elimu Kiongozi pamoja na kuongoza Idara zote za Elimu na kutoa miongozi ya kuboresha elimu husimamia vitengo maalum vilivyo katika ofisi zake. Aidha, Afisa Elimu Kiongozi husimamia shughuli za uhusiano wetu katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kilipanua programu ya MUKEJA na MEMKWA kufikia Wilaya 17. Aidha, nakala 2,000 na Miongozi ya Wawezeshaji (kilimo na Ukimwi, Siasa Jamii, Afya na *Reflect)* zilichapwa na kusambazwa Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya za MUKEJA na MEMKWA ni Biharamulo, Sengerema, Kigoma Mjini, Lushoto, Morogoro, Newala, Masasi, Liwale, Nachingwea, Tunduru, Songea Vijijini, Moshi Vijijini, Temeke, Kisarawe, Ngara, Kinondoni na Ilala.

Miongozo mitano iliyoandaliwa kwa wawezeshaji wa MUKEJA kwa matumizi ya madarasa ya Elimu ya Watu Wazima nchini kote ni sayansi Jamii, Kilimo na Uchumi, Afya, Mwongozo wa Mbinu za *reflect* na Utunzaji rahisi wa mahesabu na stadi za kuendesha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, Kitengo cha Elimu ya watu Wazima kitatekeleza Mpango wa Taifa wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Msingi kwa Walioikosa Nje ya Mfuko Rasmi wa Shule kwa kutoa mafunzo kwa watekelezaji 120 na wakufunzi 312 Wilaya, wawezeshaji wa MEMKWA 1,568 na MUKEJA 2,778 na watapeleka Wilayani vitabu 141,132 vya Moduli za MEMKWA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Kitengo cha Elimu Maalum kilitoa mafunzo ya Ualimu Elimu Maalum *(Special Needs Education)* ngazi ya cheti kwa walimu 134 na pia mafunzo ya muda mfupi Elimu Ujumuisho *(Enclusive Education)* kwa Walimu 90 wa Shule za Msingi. Katika mwaka 2003/2004, Wizara itatoa mafunzo ya muda mrefu kwa walimu wapya 150 wa walemavu ngazi ya cheti na 45 ngazi ya Stashahada. Aidha, Wizara itatoa mafunzo ya Elimu Ujumuisho ya muda mfupi kwa wlimu wa kawaida 330 ili waweze kuwapokea wanafunzi wenye ulemavu katika shule na madarasa ya kawaida. Wizara pia itagharimia Walimu 4 wa elimu maalum kupata mafunzo ya Shahada ya kwanza nje ya nchi. Vile vile, Wizara yangu itaendelea kuchapa na kusambaza vitabu kwa wasioona walioko katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003 , Kitengo cha Usajili wa Shule, Vyuo vya Ualimu na Walimu kilisajili shule zisizo za Serikali 104. Kati ya shule hizo za awali ni 8, msingi 64 na sekondari 32. Aidha, shule 105 zimethibitishwa kwenye shule na meneja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003 shule 11 zilipewa kibali cha kujengwa zikiwemo shule ya awali 1, msingi 2 na sekondari 8 na vyuo vya Ualimu 2. Aidha, shule 51 za sekondari zisizo za Serikali zilipata kibali cha kuanzisha kidato cha kwanza ambapo kati ya hizo shule 8 zilikabidhiwa Serikalini kutoka kwa wamiliki binafsi. Pia, katika mwaka 2002/2003 waombaji 342 walipewa leseni za kufundisha baada ya kuwa na sifa zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Kitengo cha Elimu ya Redio, Wizara yangu kwa kushirikiana na *Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD)* iliandaa na kutangaza vipindi 104 vya ufundishaji vipindi 52 na boresha elimu vipindi 52.

Aidha, vielelezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa mpango wa MMEM vilitayarishwa. Kadhalika, Sanaa za Maonyesho (michezo ya kuigiza) viliandaliwa na kurushwa hewani na Televisheni ya Taifa *(TVT), Independent Television (ITV)* na *Star Television.* Kanda za *video* za michezo, nyimbo, ngonjera zilitayarishwa na kusambazwa na Maafisa Elimu wote wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara imepanga kutangaza vipindi 200, kama ifuatavyo: -

Kwanza, itaandaa na kutangaza vipindi 52 vya Boresha Elimu ili kuendelea kuwaelimisha Wananchi kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002 - 2006 na pili, itaandaa na kutangaza vipindi 52 vya ufundishaji ili kuielezea mitaala mipya ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, itatangaza vipindi 96 vya masomo ya Kiingereza na Maarifa ya Jamii kwa darasa la VI na VII.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Kitengo cha kinga dhidi ya Ukimwi, Wizara iliendesha semina za wadau wanaohusika katika mpango wa kujikinga na Ukimwi shuleni na katika vyuo vya mafunzo ya ualimu. Aidha, vitabu vya shule za msingi darasa la V - VII vinavyohusiana na Elimu ya Kujikinga na Ukimwi vimeandaliwa. Wizara pia imetoa mafunzo kwa Walimu wa sayansi kwa Shule za Msingi na Walimu wa Biolojia wa shule za sekondari za Wilaya za Ukerewe, Mafia, Makete na Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004 Wizara itatekeleza mambo matatu dhidi ya Ukimwi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuendesha mafunzo dhidi ya Ukimwi kwa Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu na Wakaguzi wa Shule.

Pili, kusambaza mwongozo wa Elimu dhidi ya Ukimwi shuleni, vyuo vya ualimu na kwa wadau wote wa elimu.

Tatu, kusisitiza utumiaji sahihi wa Istilahi za mawasiliano wakati wa kutoa elimu ya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET)* ilitekeleza mambo sita yaliyokuwa katika mpango wa mwaka huo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, iliandaa rasimu ya kwanza ya mfumo wa Taifa wa mitaala, pili, ilitoa mafunzo ya MEMKWA kwa wawezeshaji katika Wilaya 12 na tatu, ilitoa mafunzo mbalimbali kwa wakuza mitaala 33 viongozi 6 na wafanyakazi waendeshaji 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, iliandaa mitaala mipya ya Elimu ya Msingi kufuatana na mahitaji ya mpango wa maendeleo ya Elimu ya Msingi, tano, iliendesha semina kwa walimu wa soko la Urais, biolojia na Kemia wa ngazi ya sekondari na wawezeshaji wa somo la Kiingereza kwa ngazi ya Elimu ya Msingi na sita, iliandaa Randama ya ushirikiano kati ya *TET* na Taasisi ya ukuzaji mitaala ya Namibia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, *TET* itatekeleza mambo makuu sita kama ifuatavyo: -

Kwanza, kukamilisha na kuchapisha mfumo wa Taifa wa mitaala *(National Carriculum Framework)*, pili, kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji na wakufunzi 100 wa MEMKWA katika Wilaya 12 na tatu, kutoa mafunzo kwa wakuza mitaala 33 na waendeshaji 41 katika maeneo ya taaluma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuandaa miongozo miwili ya ufaraguzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, tano, kurekebisha mtaala wa elimu ya msingi na sita, kuandaa mihtasari na moduli za mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti kwa masomo ya sanaa, muziki na elimu ya viungo/michezo *(physical education)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima *(TEWW)* imetekeleza mambo matano kati ya saba yaliyokuwemo katika mpango wake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, imetangaza masomo ya elimu kwa njia ya Posta, pili, imeandaa moduli 16 za Hisabati, tatu, imeendesha awamu ya kwanza ya kampeni ya Kitaifa dhidi ya Ukimwi na kuhamasisha wadau 54 na wanafunzi 119 wa stadhahada. Pia, itatoa mafunzo kwa wawezeshaji wa Kitaifa 28 na wa kanda 360, nne, imerekebisha elimu ya sekondari za jioni kuwa ya mfumo usio rasmi na tano, imeendesha kozi ya stashahada ya Elimu ya watu Wazima, cheti cha Sheria na kozi ya ushonaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza mpango wenye mambo tisa kwa lengo la kuimarisha utoaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Kujiendeleza nje ya mfumo rasmi kwa walioikosa walipokuwa katika umri sahihi wa kuwa shuleni. Aidha, *TEWW* itaendelea kutoa elimu ya Ukimwi kwa jamii kwa kuendesha kampeni ya Kitaifa ambayo inawalenga wananchi Vijijini ambao hawapati taarifa sahihi juu ya mbinu za kupambana na janga la Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *TEWW* 2003/2004 ni kukarabati majengo katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Tabora na Morogoro, kujenga vituo vya masomo ya kujiendeleza na kuboresha elimu ya kujiendeleza ya mfumo usio rasmi.

Pia, kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Taasisi kwa lengo la kuinua viwango vyao vya elimu na ujuzi, kurekebisha mihtasari ya cheti na stashahada ya juu ya Elimu ya Watu Wazima na kutoa majarida ya *Studies in Adult Education No. 60 Journal of Adult Education No. 12.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuboresha na kuendesha elimu ya masafa, (Elimu kwa njia ya Posta), kuendesha kozi ya Cheti cha Sheria, Stashahada ya Elimu ya Watu

Wazima na kozi ya ushonaji na kuendesha kampeni ya Kitaifa ya Ukimwi yenye kaulimbiu "Tubadili tabia tushinde Ukimwi."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Bodi ya Huduma za Maktaba kupitia Maktaba zake pamoja na uendelezaji wa ujenzi wa Maktaba ya Dodoma ilitekeleza mambo manne kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, iliimarisha na kuboresha huduma za Maktaba za Mikoa 18, pili, ilipanua huduma za wasioona katika Maktaba Kuu, tatu, ilitekeleza ujenzi wa awamu ya kwanza kwa Maktaba ya Dodoma na nne, ililipia kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ukutubi na uhifadhi nyaraka Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003/2004, Bodi ya Huduma za Maktaba itatekeleza mambo manne yafutatayo ya kuboresha Huduma za Maktaba, itaimarisha na kuboresha huduma za Maktaba katika Mikoa 18, itajenga Maktaba katika Mikoa ya Singida na Dodoma, itapanua na kuongeza uwezo wa ujuzi wa watendaji wa Maktaba kwa kupeleka Watumishi 57 kwenye mafunzo ya stashahada ya uzamili, shahada, stashahada na cheti. Aidha, itajenga jingo mahsusi la Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka na itaongeza uelewa wa athari za ugonjwa hatari wa Ukimwi kwa kuendesha semina, kuchapisha vipeperushi na vijitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003 Baraza la Mitihani liliendesha mitihani ya Kitaifa ya kumaliza Elimu ya Msingi ya Darasa la VII Tanzania Bara, Elimu ya Sekondari ya Kidato cha 4 , ya kidato cha 6 na Mitihani ya Ualimu Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mtihani wa Kitaifa wa kumaliza Elimu ya Msingi yaani Darasa la VII mwaka 2002 kati ya watahiniwa 492,472 waliofanya mtihani waliofaulu walikuwa 133,674 sawa na asilimia 27.1 hilo ni ongezeko la watoto 23,041 waliofaulu ukilinganisha na mwaka uliopita. Nawapongeza Walimu, Walimu Wakuu, Maafisa. Nawahimiza waendelee na juhudi hiyo ili tufikie lengo la kufaulu asilimia 50 ifikapo mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha 4 mwaka 2002, kati ya watahiniwa 49,512 wa shuleni waliofaulu katika daraja I, II, III walikuwa 17,939 sawa na asilimia 36.21 kulinganisha na 14,397 sawa na asilimia 28.32 waliofaulu mwaka 2001. Nawapongeza wakuu wa shule na walimu wote waliohusika na ongezeko la waliofaulu 3,542 pamoja na wanafunzi husika wote 17,939.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha 4 mwaka 2002 unaonesha kuwa juhudi za kuboresha Elimu ya Sekondari zinazaa matunda mema kama inavyoonyeshwa katika vielelezo vifuatavyo:-

(a) Kielelezo Na. 38.4 Watahiniwa wa Sekondari zote za Serikali na zisizo za Serikali kwa pamoja.

(b) Kielelezo Na. 38.5: Watahiniwa wa Sekondari za Serikali Tanzania Bara.

(c) Kielelezo Na. 38.6 Watahiniwa wa Sekondari zisizo za Serikali Tanzania Bara.

(d) Kielelezo Na. 38.7 watahiniwa wa Sekondari za Serikali Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mtihani wa Kitaifa kidato cha 6 mwaka 2001/2002 kati ya watahiniwa 15,000 waliofaulu katika Daraja I, II, III walikuwa 10,810 sawa na asilimia 72.6 ikilinganishwa na 9,870 sawa na asilimia 65..7 waliofaulu mwaka 2001/2002. Hilo ni ongezeko la waliofaulu 940.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mitihani ya Ualimu ya mwaka 2002 waliofaulu walikuwa 11,801 sawa na asilimia 90.7 ya watahiniwa wote 13,010. Katika mitihani ya Elimu ya Ufundi ya mwaka 2002 waliofaulu walikuwa 517 sawa na asilimia 52 ya watahiniwa 1,003 wa mitihani hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002/2003, BAMITA limetekeleza mambo muhimu sita yafuatayo yaliyopendekezwa na Tume maalumu ya Serikali iliyochunguzwa mianya ya uvujaji wa mitihani mwaka uliopita. Mambo yaliyotekelezwa na Baraza la Mitihani ni ujenzi wa jengo la usajili wanapofikia wageni bila kuingia ofisi zingine za Baraza la Mitihani Tanzania, ukarabati wa jengo la kitengo cha chapa na uchapishaji, ununuzi wa baadhi ya mashine za uchapaji mitihani, ununuzi wa baadhi ya kompyuta na vifaa vyake kwa ajili ya kuandaa na kutoa matokeo ya mitihani, kuweka mtandao wa kompyuta *(Local Area Network - LAN)* kwa madhumuni ya kutoa huduma bora na kufanya maandalizi ya awali ya ujenzi wa kituo cha Usahihishaji Mitihani Mbezi Wani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utekelezaji huo, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tufuku kuwa kuanzia mwaka huu mitihani ya Kitaifa ya darasa la VII, Kidato cha 4 na Kidato cha 6 imeanza kuchapwa hapa nchini kwa usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, Baraza la Mitihani la Taifa limejiandaa kwa ukamilifu zaidi kutekeleza wajibu wake wa kutunga na kuendesha mitihani yote ya kitaifa kwa ufanisi unaohitajika, ikiwa ni pamoja na kuendesha na kusimamia mitihani itolewayo na Bodi 9 za mitihani ya nje. BAMITA litatelekeza malengo yafuatayo:-

Kwanza, litafanya utafiti, tathmini, usanifu na ukuzaji mitihani mbalimbali ya Kitaifa.

Pili, litaendesha mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, maarifa *(qualifying test)* kidato cha 4 na 6, kuhitimu mafunzo ya ualimu Daraja la A na Stashahada *(Diploma)* ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, litaendesha mitihani ya cheti cha ufundi stadi, ufundi sanifu *(Full Technician Certificate- FTC)* na Stashahada ya juu ya Uhandisi kwa niaba ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, litasimamia mitihani ya nje inayofanywa na watahiniwa wa hapa nchini, tano, litaendeleza ujenzi wa Kituo cha Kusahihisha Mitihani na sita, litatengeneza programu ya kompyuta itakayowezesha utoaji wa matokeo ya kufaulu mtihani wa kidato cha 4 na uchaguzi wa wanafunzi wa kuingia kidato cha 5 kwa pamoja ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Tume ya Utumishi wa Walimu imetekeleza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, iliwapandisha vyeo walimu 26,419 katika vikao 4 vya Bodi, ilishughulikia jumla ya mashauri ya nidhamu 359, iliandaa na kuwasilisha Hazina madai ya pensheni na mirathi 887 kwa malipo na ilitangaza vipindi 52 vya ijue Tume ya Utumishi wa Walimu.

Katika mwaka 2003/2004, Tume ya Utumishi wa Walimu imejiwekea malengo yafuatayo ya kuboresha huduma zake kwa walimu ikiwa ni kupandisha vyeo walimu, 16,974 katika ngazi mbalimbali, kushughulikia mashauri 392 ya nidhamu, kushughulikia pensheni na mirathi 905 pamoja na kuanza kuweka kumbukumbu kwenye kompyuta na kuendeleza jitihada za kujitangaza na kuboresha huduma inazotoa kwa walimu nchini ili waweze kutoa elimu bora kwa walengwa na kuwapunguzia kero.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lilitekeleza mambo sita katika mpango wake kama ifuatavyo:-

Kwanza BASATA ilitoa mafunzo kazini kwa wasanii 220 wa fani mbalimbali, ilihamasisha na kuratibu tamasha la Ukaguru kwa kushirikiana na Chama cha Maendeleo ya Watoto na Vijana (CHAYODE), ilitoa mafunzo ya awali juu ya Elimu ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa wasanii 580, ilitoa mafunzo ya tahadhari ya janga la Ukimwi kwa njia ya Sanaa kwa wanavijiji 8,275 wa vijiji vitano vya Mkoa wa Kagera. Vijiji hivyo ni (1) Rugeze, (2) Butulaga, (3) Bimbya, (4), Kyaitoke na (5) Kobushwi, ilianza ujenzi wa uzio katika uwanja wa BASATA na iliratibu tamasha la muziki wa asili lililoshirikisha vikundi 15 vyenye wasanii 200 vya nchi wanachama wa *SADC.*

Katika mwaka 2003/2004 BASATA litatekeleza mpango wenye mambo 7 ya kukuza sanaa yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuboresha elimu ya wasanii kwa kuendesha kozi fupi tatu kwa wasanii 300 na pili, kuhamasisha umma uweze kuthamini sanaa zetu za asili kama kitambulisho muhimu cha Taifa letu katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuendesha warsha za sanaa za ufundi wa mikono, nne, litaanza ujenzi wa ukumbi wa wazi kwa ajili ya mafunzo na maenyesho

mbalimbali kwa umma na tano, litatoa mafunzo kuhusu sheria za Hakimiliki na Hakishirikishi kwa wasanii 250.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, litaendelea na ujenzi wa uzio katika uwanja wa BASATA na saba, litatoa elimu kwa njia ya Sanaa kuhusu janga la Ukimwi kwa Mikoa 6 ya Tanznaia Bara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Baraza la Kiswahili la Taifa limetekeleza yafuatayo katika mpango wake:-

Kwanza, lilifanya maadhimisho ya saba ya ya siku ya Kiswahili, lilisanifu istilahi 830 za Ukimwi na magonjwa husianifu pamoja na kudurusu istihahi 10,337 za fani mbalimbali na tatu, liliendesha warsha ya uchapishaji kuhusu umuhimu wa kuthibitisha Lugha ya Kiswahili na mbinu za kufanikisha uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili.

Katika mwaka 2003/2004, Baraza la Kiswahili la Taifa litatekeleza majukumu matatu ya kukuza Kiswahili. Malengo ya BAKITA 2003/2004

Kusanifu Istilahi mchanganyiko kwa ajili ya kuziba pengo la msamiati katika mawasiliano ya kila siku Serikalini na katika Mashirika.

Kufuatilia kwa karibu na kusahihisha makosa ya ufasaha wa lugha ili kuzuia upotoshaji wa hadhira kuhusu matumizi ya lugha.

Mheshimiw Naibu Spika, pia BAKITA ina jukumu la kufanya semina kwa wafasiri na wakalimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imebaini matatizo yafuatayo:-

Kwanza, baadhi ya Halmashauri zimeonyesha udhaifu katika kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na matumizi yake ya fedha kwa wakati unaotakiwa. Udhaifu huu umesababisha kuchelewa kwa fedha kutoka kwa Wahisani, kwa hiyo inabidi uvaliwe njuga na sisi wote tunaohusika.

Pili, baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Elimu wa Wilaya kutowataarifa Walimu Wakuu wa Kamati za Shule mgao wa ruzuku ya uendeshaji uliopokelewa kutoka Serikali Kuu. Kuanzia sasa lazima Walimu Wakuu na Kamati za Shule wapewe taarifa hiyo ili wafuatilie mgao wa fedha zao kwa jumla ya wanafunzi walionao ili waweze kuzipangia matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, baadhi ya Halmashauri kupuuza vigezo sahihi vifuatavyo katika ujenzi na uendeshaji wa Shule za msingi na nne, umri wa wanafunzi Darasani uwe sawa au karibu sawa ili wafundishike vizuri kwa kasi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, wingi wa Wanafunzi Darasani *(Class Size)* wasiwe zaidi ya wanafunzi 40, sita, ukubwa wa shule *(School Size)* ya Msingi kwa wingi wa wanafunzi: Vijijini usizidi mikondo miwili (40x2x7) sawa na wanafunzi 560 na Mijini usizidi mikondo mitatu yaani 40x3x7 sawa na wanafunzi 840, saba, viwango vya ubora wa majengo ya shule yakiwemo madarasa nyumba za walimu na vyoo na mwisho, ili kufanikisha MMEM lazima vigezo hivyo vifikiwe katika Wilaya zote kwa kujenga madarasa na nyumba za walimu za kutosha na kuajiri walimu wa kutosha. Aidha, lazima viwango vya ubora wa majengo ya shule vizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itasimamia kwa nguvu zote maamuzi muhimu yafuatayo:-

Kufutwa kwa ada na michango ya wazazi peke yao katika shule za msingi. Nachukua fursa hii kusisitiza kwa mara nyingi kuwa Serikali inakataza kabisa kuwachangisha wazazi wa wanafunzi wa shule ya msingi peke yao kwa sababu yoyote. Huu ni uamuzi wa Serikali ambao hauwezi kubadilishwa na Kamati ya Shule, Mwalimu Mkuu ndiye Afisa Elimu wa Kijiji au Mtaa wa kuiambia Kamati ya Shule kuwa hairuhusiwi kuwachangisha wazazi.

Kuhakikisha kuwa mafungu ya MMEM hususan Ruzuku ya Maendeleo na Ruzuku ya Uendeshaji na Mfuko wa uwezeshaji yanatumika ipasavyo na siyo vinginevyo.

Pia kuhakikisha kuwa siku 194 za kufundisha na kujifunza madarasani na ratiba za shule za msingi, sekondari na vyuo kama ziliyopangwa na Afisa Elimu Kiongozi zinazingatiwa.

Ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa elimu Wizara yangu imeamua kuanzia mwaka ujao watahiniwa wa Kidato cha Nne wanaochaguliwa kuendelea na Kidato cha Tano wataaanza masomo mwanzoni mwa mwaka unaofuata badala ya Julai.

Kwa hiyo, watakaohitimu Kidato cha Nne Novemba, 2004 wajiandae na shule zijiandae kuanza Kidato cha Tano Februari, 2005. Aidha, mashauriano yanaendelea na wenzetu wa Elimu ya Juu na Hazina ili hata wahitimu wa Kidato cha Sita wanaochaguliwa kuendelea na Elimu ya Juu (Chuo Kikuu) waunganishe bila kuchelewa badala ya utaratibu wa sasa wa kusubiri miezi 16. Lengo la zoezi hili ni kuwawezesha vijana wetu kuhitimu Chuo Kikuu wakiwa na miaka 24 badala ya miaka 26 au zaidi kama ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wao katika kufanikisha MMEM. Nawapongeza na nawashukuru sana Wakuu wa Shule, Walimu Wakuu na Walimu wote kwa matokeo ya mitihani ya Kitaifa ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari ambayo yameanza kuboreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wabia wetu katika maendeleo ya elimu na utamaduni zikiwemo nchi rafiki za Sweden, Japan, Norway, Uingereza,

Ufaransa, Ireland, Uholanzi, Finland, Canada, Ujerumani, Ubelgiji, Jumuiya ya Ulaya, China na Korea ya Kusini na Mashirika ya *SIDA, NORAD, GTZ, DFID, ADB, WFP, UNICEF, UNESCO, UNFPA, UNDP, ILO, JICA, JOVC, Peace Corps,* Benki ya Dunia, *Aga Khan Education Foundation, World Vision, Ireland Aid, Plan International, CARE International TASAF* na *Equal Opportunity For All Trust Fund (EOTF)* wanaosaidia sana katika upatikanaji wa vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge mashuhuri wa Jimbo la Kwimba, kwa ushirikiano wake mzuri katika kuiongoza Wizara ya Elimu na jana nimeongea naye kwa simu amekwisharudi Dar es Salaam kutoka katika matibabu India, anawasalimia sana. *(Makofi)*

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara yetu bibi Mwatumu Malale, pamoja na wasaidizi wake akiwemo Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi wa Idara pamoja na walimu na wafanyakazi wengine wote wa Wizara yangu kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hususan jukumu mama la utoaji elimu iliyo bora kwa mwaka jana na pia katika maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Wenyeviti, Wakurugenzi Watendaji, Makatibu Watendaji na wajumbe wa Mabaraza na Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara yangu na wafanyakazi wengine wote kwa mchango wao mzuri. Aidha, nawashukuru viongozi wa *CWT* na Tawi la *TUGHE* la Makao Makuu ya Wizara kwa ushirikiano na ushauri wao katika masuala ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza yote hayo, naliomba sasa Bunge lako Tukufu baada ya kujadili hoja yangu pamoja na kuzingatia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Huduma ya Jamii lipitishe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 106,719,657,550/= ili kuwezesha Wizara ya Elimu na Utamaduni pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu kutekeleza mipango ya mwaka 2003/2004.

Kati ya fedha hiyo shilingi 45,721,360,100/= zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, shilingi 58, 892,856,200/= zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo na shilingi 2,105,441,250/= zinaombwa kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** *Speaker's Guidance.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kidogo, naomba tu msaada wa kiti. Pengine maombi haya yangekuja mapema zaidi lakini kwa bahati mbaya yamekuja leo.

Msaada wa kiti ninaoomba ni kwamba tangu tumeanza shughuli hizi za Bajeti ya mwaka 2003/2004 ukiacha Hotuba ya Mipango na Bajeti ya Serikali na Hotuba ya Waziri Mkuu, hotuba nyingine zote za Mawaziri zimewasilishwa hapa kwa mwendo wa *speed* kubwa sana kwa sababu ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi ambacho kila Waziri mmoja aliyewasilisha hotuba yake hapa, Wabunge wengi tunashindwa kuifuatilia inakwendaje. Sasa mwongozo wa kiti ninaoomba na pengine wenzangu wataniunga mkono. Wakati Waziri akimaliza tu kusoma hapo hapo tunaanza kuchangia, hivi *speed* hii inakuja kwa sababu gani? Maana hatuwezi kuifuatilia hotuba ya Waziri mpaka tukamaliza, tukajiandaa kujadili wakati hiyo ndiyo kazi iliyotuleta Dodoma, kwa nini tunaruhusu haraka yote hii ili tufanyeje?

Naomba mwongozo wa kiti, hivi hatuwezi kubadilisha mtindo huo tukarekebisha, ili Wabunge wapate muda wa kutosha wa kuielewa hotuba na kutoa michango yao kama inavyotegemewa na wale waliowaleta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sina uhakika aliyesimama ni kuunga mkono au ushabiki au mambo mengine. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo nimeisikia, ni suala la Kanuni, Kanuni zetu zinampa muda wa nusu saa Mheshimiwa Waziri kusoma hotuba yake. Sasa kama muda huo mnadhani hautoshi basi ni suala la kupeleka maombi yenu kwenye Kamati ya Kanuni ili kama ni mabadiliko yafanyike kwa sababu mnajua jinsi tunavyobadilisha. Tulikuwa na utaratibu mwingine, tukabadilisha lakini kwa hivi sasa mpaka tutakapomaliza kipindi hiki cha Bajeti bado watakuwa na nusu saa.

Sasa katika kipindi cha nusu saa ili wote mpate yale yanayotendeka Wizarani na Wizara ni kubwa lazima ajitahidi kuyaweka pamoja na kusoma pengine kwa haraka haraka. Kwa hivi sasa tutumie hivyo vitabu ambavyo tumepewa katika kujiandaa na bado tutakuwa na muda kwa hii Wizara, lakini kwa hivi sasa kwa sababu Kanuni zetu zinasema hivyo hatuna namna nyingine isipokuwa kwenda na huu mwendo ambao tunakwenda nao.

Sasa namwita Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, ili atoe maoni ya Kamati.

**MHE. HAMISI J. NGULI (k.n.y. MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni Fungu Na. 46 na 67 kwa mwaka 2003/04.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Bajeti ya mwaka 2002/2003 (Fungu 46 na 67) na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004. Aidha, kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii nachukua fursa hii kuwapongeza na kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa hivi karibuni katika chaguzi ndogo na wale walioshinda kesi na kuendelea na Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo yaliyowekwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 na pia ilipitia malengo ya mwaka wa fedha wa 2003/2004 kwa Fungu 46, Wizara ya Elimu na Utamaduni na Fungu 67 linalohusu Tume ya Utumishi wa Walimu. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati yangu ilipitia vifungu vifuatavyo:-

- Dira na mwelekeo wa Wizara ya Elimu na Utamaduni.

- Majukumu ya Wizara.

- Utekelezaji wa mapendekezo na Maagizo ya Kamati iliyochambua Bajeti ya mwaka 2002/2003.

- Mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2002/2003.

- Malengo, mafanikio na matatizo ya utekelezaji wa mwaka 2002/2003.

- Malengo yaliyowekwa mwaka wa 2003/2004 na maombi ya fedha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili, ilichambua na kuhoji vipengele vilivyotajwa hapo juu. Vile vile Kamati ilipewa maelezo na ufafanuzi wa masuala yaliyohojiwa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni akisaidiwa na timu ya Wataalam wake wakiongozwa na Katibu Mkuu. Kamati iliridhishwa na kazi inayofanywa na Wizara na kuafiki kuwa hoja hiyo iwasilishwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Kamati ya Huduma za Jamii inazingatia Kanuni ya 81(1) (2003) na inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yake kwa Serikali kwa nia ya kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara hii kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma za Jamii imeridhika na mwelekeo wa Dira *(Vision)* ya Wizara kuwa inakidhi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwani inalenga kuona kuwa Wizara inatoa elimu bora katika ngazi zote ili Taifa liwe na watu wengi wenye elimu bora na maarifa yatakiwayo katika kutatua matatizo ya jamii, kukabiliana na mabadiliko yatokanayo na maendeleo na kuwa na uwezo wa ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi Dira hii muhimu, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara hii kwa mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza mpango wa MMEM kwa kuandikisha watoto wa darasa la kwanza kwa asilimia 105.4 ya lengo mwaka 2002. Hata hivyo Kamati inashauri Serikali iendeleze juhudi za kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia hasa ujenzi wa madarasa bora ya kutosheleza uwiano wa 1.40.

Aidha, zoezi hili liendeshwe sambamba na ununuzi wa samani hasa madawati ambayo kwa sasa kuna upungufu wa madawati 1,283,386, vitabu vya kiada na ziada na madaftari ya kukidhi mahitaji ya idadi ya wanafunzi inayoongezeka kila mwaka.

Vile vile zoezi hili liimarishwe kwa kuweka mazingira bora ya kuishi Walimu waliosambaa nchini kote na kupunguza uwezekano wa kushindwa kutekeleza majukumu yao na kusababisha wanafunzi kuacha shule au walimu kuacha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendeleze jitihada zake za kuajiri Walimu wa kukidhi mahitaji na wenye sifa za kufundisha Elimu ya Msingi.

Aidha, Serikali itathmini utaratibu wake wa sasa wa kuandaa Walimu wa Daraja la IIIA kwa mwaka mmoja chuoni na mwaka mmoja mafunzo kwa vitendo shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia utaratibu huu Kamati inaona kuwa kuna uwezekano wa Walimu tarajali kutotayarishwa vizuri ikizingatiwa kuwa mwaka wa mafunzo kwa vitendo *(Practicals)* Walimu hao husambazwa kwenye shule mbalimbali nchini ambako huwa si rahisi kwa Wakufunzi na Walimu wao kuweza kuwafuatilia kwa karibu na kuwapa mwongozo na maelekezo kila inapobidi hasa kwa maeneo ya Vijijini ambayo hayafikiki kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa kukidhi mahitaji ya idadi ya wanafunzi inayoongezeka kila mwaka. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali Kuu kupeleka fedha za ujenzi katika Halmashauri za Wilaya mapema iwezekanavyo. Aidha, Kamati inashauri kuwa kila Halmashauri ihakikishe kuwa inasambaza ramani inayokubalika Kitaifa kwa Wakandarasi wanaoteuliwa kujenga madarasa na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati inashauri kuwa Wahandisi wa Halmashauri wawajibike kuthibitisha viwango vya ubora vya ujenzi badala ya kuziachia Kamati za Shule peke yake. Aidha, taarifa ya kukamilika kwa ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu baada ya ukaguzi ijadaliwe pia kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata na hatimaye Taarifa hizo zifikishwe kwenye vikao vya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mapato na matumizi ya fedha za ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu pamoja na fedha za kuendeshea shule *(Capitation Grant)* zinazotolewa na Serikali kuu kwa ajili ya kukarabati majengo, ununuzi wa vitabu vya

kiada, miongozo ya kufundishia, madaftari, chaki na kadhalika zijulikane kwa Kamati ya Shule badala ya Walimu Wakuu na Wenyeviti wa Shule tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali itekeleze kwa ukamilifu ahadi yake ya kutoa fedha za kuendeshea shule *(Capitation Grant)* kiasi cha Dola za Kimarekani kumi kwa kila mwaka kwa kila mwanafunzi. Kamati inayo taarifa kuwa kiwango kilichowahi kufikiwa ni dola za Kimarekani sita tu na hivyo kuathiri maendeleo ya elimu na mipango ya shule kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa endapo kiwango hicho hakikufikiwa Serikali itoe maelezo ya kina kwa wadau wote mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaelewa fika umuhimu wa shule kukaguliwa mara kwa mara ili kutathmini maendeleo na kubaini mapungufu yanayohitaji kuboreshwa. Pamoja na jitihada zilizofanywa na Serikali kutokana na kuongezeka kwa idadi ya shule za msingi na wingi wa mikondo na uchache wa Wakaguzi, bado ukaguzi katika Shule za Msingi haujatosheleza. Hivyo Kamati inashauri yafuatayo:-

Serikali iendelee kufundisha Wakaguzi ili idadi yao iongezeke kwani katika kazi zilizopangwa kufanyika mwaka huu wa fedha katika eneo hili ni kuendesha mafunzo ya awali ya wakaguzi 127, lakini mahitaji halisi ya wakaguzi mwaka jana ilikuwa ni 1,269. Hivyo idadi hii ni ndogo sana.

Waratibu wa Elimu wa Kata ambao kimsingi kazi yao ni kuwa Waratibu wa Elimu ya Watu Wazima kazi ambayo kwa sasa inalegalega, Serikali iwapatie mafunzo maalum ya ukaguzi wa Shule ili wawe Wakaguzi Wasaidizi katika Kata zao. Aidha taarifa zao zipelekwe kwa Wakaguzi wa Elimu wa Wilaya ili wazifanyie kazi.

Serikali iongeze nyenzo hasa vifaa vya usafiri kwa ajili ya kufanikisha ukaguzi kwa kuzingatia idadi ya Shule za Msingi na ukubwa wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa utaratibu uliowekwa na Serikali kwa wanafunzi wanaoshindwa kufaulu mitihani wakaririshwe uzingatiwe kuanzia darasa la kwanza badala walimu kusubiri hadi wanafunzi wafike darasa la nne kwani utaratibu huo ukitekelezwa katika ngazi ya darasa la nne tu unasababisha wanafunzi wengi kurundikana kwenye darasa la nne. Tunashauri Walimu Wakuu na Afisa Elimu wawajibike kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Kuhusu vitabu vya kufindishia na kujifunzia *(Text Books),* Kamati inashauri kuwa ili kuwatendea haki watahiniwa wa Darasa la Nne na Darasa la Saba kuwepo na vitabu vya aina moja vilivyokubalika kwa ajili ya Elimu ya Msingi nchini kote, kwani utaratibu wa sasa unaruhusu walimu kuchagua katika orodha ndefu iliyoidhinishwa na Wizara kwa kiasi unachangia kuwachanganya walimu na wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wimbi la Walimu wengi kupenda kufanya kazi maeneo ya Mijini au karibu na Mijini ambako kuna huduma nyingi za jamii. Baadhi yao hata wakitangaziwa kuwepo kwa nafasi za kazi shule za Vijijini huwa hawakubali kwenda kujaza nafasi hizo.

Kamati ilitafakari mazingira ya kazi ya Ualimu na kuona kuwa baadhi ya shule hasa Vijijini, kuna mazingira magumu ya kutowavutia walimu. Kutokana na hali hiyo kuna walimu wa kutosha maeneo ya Mijini na kuna upungufu mkubwa shule za Vijijini. Kamati inashauri kuwa ili Serikali iweze kutekeleza kwa mafanikio azma yake ya kutoa Elimu ya Msingi kwa wote, ione umuhimu wa kutoa motisha *(attractive package)* kwa Walimu wanaopangiwa vituo vya kazi katika maeneo ya aina hiyo. Kamati ina uhakika motisha hiyo itawapa moyo wa kwenda kufundisha watoto katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashawishika kutamka kuwa Serikali kuendelea kufananisha maslahi ya watumishi katika sekta zote bila kuangalia mazingira ya kazi kuna athari kubwa katika kuendeleza sehemu zote za nchi kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Tume ya Utumishi wa Walimu, Kamati inapendekeza kuwa Tume iongeze kasi katika kushugulikia masuala ya nidhamu, matatizo na malalamiko ya Walimu. Aidha, Tume ihakikishe kuwa Serikali inalipa mishahara walimu wanaoajiriwa bila kucheleweshwa sana kama ilivyotokea kwa baadhi ya walimu walioajiriwa mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati inashauri kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu itunze kumbukumbu na takwimu muhimu za utumishi wa walimu wote zikionyesha tarehe za kuajiriwa, kuthibitishwa na tarehe za kustaafu ili walimu wanapostaafu wasilazimike kuhangaika kutafuta kumbukumbu hizo ambazo wakati mwingine huwa vigumu kuwa nazo kutokana na mazingira magumu wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inashauri maslahi ya walimu wanaofariki yatayarishwe haraka bila kuleta adha na usumbufu kwa wanaofuatilia mirathi ya ndugu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye juhudi za makusudi za kupanua elimu ya sekondari nchini kote hadi ngazi ya Kata ili kulinda na kuendeleza mafanikio yanayotokana na mpango wa kuboresha Elimu ya Msingi kupitia mpango wa MMEM.

Kamati inashauri hivyo kutokana na ukweli kuwa wototo wengi wanaomaliza elimu ya msingi na kufaulu huwa hawapati nafasi ya kuendelea na Elimu ya Sekondari kutokana na uchache wa nafasi katika Shule za Sekondari zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, watoto ambao huchaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari huwa hawaendi wote kutokana na tatizo la wazazi wao kushindwa kulipa ada. Katika hali ya kawaida si rahisi mzazi aliyeshindwa kulipa ada ya Shule ya Msingi ambayo ni ndogo sana aweze kulipa ada ya Sekondari ambayo ni kubwa sana kuliko ile ya Shule ya Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kamati inashauri kuwa utaratibu unaotumika katika mpango wa MMEM utumike katika ngazi ya elimu ya sekondari kwa watoto wote wanaochaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa wengi wetu tuliomo ndani ya Bunge hili Serikali ilitugharamia ada za Elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo vya taaluma mbali mbali na hata Vyuo vya Elimu ya Juu. Hivyo Serikali ione tatizo hili kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa kutokana na ukweli kuwa elimu ya sekondari ni maandalizi kwa ajili ya elimu ya juu na taaluma nyingine na ukweli kwamba nchi yetu ipo nyuma sana katika ngazi ya elimu ya Sekondari katika Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki, Serikali isaidie wananchi katika ujenzi wa sekondari kama inavyosaidia katika mpango wa MMEM kwa kugharimia sehemu ya ujenzi kama kupaua na kuezeka majengo ya Shule za Sekondari za kutwa za Serikali zinazojengwa kwa nguvu za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii itasaidia katika maandalizi ya awali ya ushindani katika soko la ajira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shule za Sekondari za binafsi, Kamati inapongeza wananchi na Taasisi kwa kuanzisha shule hizo. Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ione namna ya kuzisaidia shule hizi ambazo zinaongezeka zikisaidia jukumu la Serikali la kupanua Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fungu la Mfuko Maalum kwa kusaidia ada ya sekondari kwa ajili ya watoto yatima na wale wanaotoka kwenye familia zisizo na uwezo kutoka shilingi billioni moja mwaka 2002/2003 hadi bilioni 1.4 mwaka wa 2003/2004. Hata hivyo Kamati inashauri kuwa taratibu zilizotolewa na Wizara kuhusu namna ya kutumia mfuko huo zizingatiwe na kila Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa utaratibu wa kubakiza fedha za ada shuleni katika utaratibu wa *retention* kwa ajili ya matumizi ya kila sekondari, kwa kuzingatia upungufu wa wahasibu uliopo kuwepo udhibiti wa kutosha wa matumizi ya fedha. Aidha, matumizi yake yazingatie mwongozo wa Wizara. Kamati itapenda kuona utekelezaji wa taratibu nzuri za kihasibu katika taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza kuwa Elimu Maalum inayotolewa kwa watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali iimarishwe kwa kuweka mazingira sahihi yanayowafaa watoto wenye ulemavu katika majengo ya shule, vifaa maalum vya kuwafundishia, kuwatahini na kadhalika. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kusaidia shule za watu binafsi na za Mashirika zinazohudumia watoto hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati tangu mwaka 2002 ilieleza kutoridhishwa kwake na maendeleo ya Elimu ya Watu Wazima katika miaka ya hivi karibuni ingawa Bunge limekuwa likiidhinisha fedha kila mwaka kwa ajili ya kufufua na kuendeleza Elimu hii. Kutokana na hali hii idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika inazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kamati inaishauri Serikali ifanye jitihada za kufufua Elimu ya Watu Wazima kote nchini kwa kampeni maalum kama ilivyokuwa miaka ya sabini ambako elimu hii ilifikia hatua nzuri. Kwa sasa kinachoonekana ni vibao vya kuonyesha vituo vya Elimu ya Watu Wazima katika shule za msingi. Kwa ujumla Elimu ya Watu Wazima ambayo ni njia fupi sana ya kutoa elimu kwa jamii sasa haitolewi kwa kiwango kinachotakiwa.

Hatua hii ya kuendeleza Elimu ya Watu Wazima pia ihusishe kuandaa motisha au marupurupu kwa walimu watakaoteuliwa kufundisha Elimu ya watu Wazima kama tunataka elimu hii itolewe kwa kiwango kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawapongeza wanataaluma wote wanaojitahidi kuandika vitabu mbalimbali kwa ajili ya kufundishia katika Shule za Msingi na Sekondari. Pamoja na pongezi hizo Kamati inashauri Serikali kuwa ili kuwatendea haki watahiniwa, ni vema Serikali ikaweka bayana vitabu vya kutumia katika shule zote. Aidha, vitabu vinavyotumika katika kuandaa mitihani vijulikane na visambazwe katika shule zote na vikibadilishwa iwe ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo kwa kukuza na kulinda utamaduni wetu wa asili. Kamati inashauri kuwa Chuo hicho kiimarishwe na kuendelezwa ili kifikie dhima yake ya kuwa mfano wa kuigwa *Center of Exellency* na kiwezeshwe kuelimisha jamii madhara ya kuiga utamaduni wa kigeni bila kutafakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai kwa ushirikiano wake na Kamati yangu wakati wa kujadili na kuchambua Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2003/2004. Pia Kamati inamwombea dua njema Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni Mheshimiwa Bujiku Sakila apone haraka na aungane nasi katika ukumbi huu. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Wataalam wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Mwantumu Malale, kwa ushirikiano waliotoa kujibu hoja na maswali wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa umakini na ushirikiano wao mkubwa wakati wa kujadili Fungu 46 na 67 na sasa naomba niwatambue kwa majina, Mheshimiwa Omar Kwaangw' -Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ali, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan.

Wengine ni Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Halmenshi Mayonga, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Benedict Mutungirehi, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi na mimi mwenyewe Mheshimiwa Hamisi Nguli. *(Makofi)*

Mwisho, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioshirikiana na Kamati kuchambua Bajeti ya Wizara hii chini ya Kanuni ya 88(6).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS ALI SALEHE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni kwa Niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa elimu ina umuhimu mkubwa katika kupambana na maadui wakubwa watatu wa nchi yetu; yaani ujinga, maradhi na umaskini. Pia ni ukweli usiofichika kuwa nchi yetu imeshindwa kupambana na maadui hawa kutokana na Serikali ya kutokuwa makini katika utoaji wa elimu nchini. Kama tulivyosema mwaka 2000, bado tunasisitiza kuwa Serikali imepalilia zaidi ujinga, maradhi na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya elimu katika nchi yetu yanajulikana wazi kwa kila mtu kwa sababu yamekuwa wimbo katika ngazi zote, kuanzia Chekechea, Msingi, Sekondari, Vyuo na hata Vyuo vikuu. Naishukuru Serikali kwa kukiri na kukubaliana na Kambi ya Upinzani juu ya matatizo katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengi na makubwa ya elimu katika nchi yetu kwa muda mrefu sasa na kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakisababishwa na bajeti finyu, ambayo imekuwa ikitolewa kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Suala la Bajeti finyu nalo limekuwa ni wimbo na kero katika masikio ya wengi, kwa sababu limekuwa kimbilio la Mawaziri na Manaibu Waziri pale wanapobanwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kutakiwa kueleza ni kwa nini wameshindwa kutekeleza ahadi zinazotolewa Bungeni. Je, ni lini Bajeti finyu itakuwa Bajeti pana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ambazo zimekuwa zikitengwa kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni hazitoshelezi mahitaji halisi. Takwimu zinaonyesha kuwa katika bajeti ya matumizi ya kawaida, ukilinganisha kiasi kilichotengwa na mahitaji halisi, upungufu umekuwa kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2000/2001 asilimia 27.2;

- Mwaka 2001/2002 asilimia 4.3;
- Mwaka 2002/2003 asilimia 40.1; na
- Mwaka 2003/2004 asilimia 52.9.

Je, Serikali itaboreshaje elimu duni tuliyonayo katika upungufu huu wa Bajeti? Hili bado ni swali sharti lijibiwe na Serikali pamoja na wadau wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya elimu, ambayo yamekuwa yakitokana na upungufu wa Bajeti ni kama yafuatayo:-

Upungufu wa walimu na watumishi wasio walimu kwenye ngazi mbalimbali; hii ni pamoja na uwiano mbaya kati ya walimu na wanafunzi. Taarifa ya Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa Kamati ya Kisekta ya Huduma za Jamii kwa mwaka wa fedha 2003/2004 inaonyesha kuwa kufikia Novemba 2002, jumla ya walimu wote walioajiriwa walikuwa 8,007. Ajira hiyo ina upungufu wa asilimia 12.02. Mwaka 2003, Wizara imepeleka maombi ya walimu wapya 11,651. Kawaida ya ombi ni kukubaliwa au kukataliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyombo vya Habari vya ndani na nje, ikiwa ni pamoja na magazeti, redio na *television*, vimekuwa vikiripoti kwa nyakati tofauti juu ya upungufu mkubwa wa walimu katika shule mbalimbali. Baadhi ya madarasa, hasa katika shule za msingi yameonekana kuwa na zaidi ya wanafunzi mia moja wanaofundishwa na mwalimu mmoja. Licha ya hayo, wanafunzi katika shule mbalimbali, hasa za Sekondari, wamekuwa wakiripotiwa kuandamana kwenda kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kudai waletewe walimu wa kutosha na wenye sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wale walimu wachache waliopo mashuleni, hawakuandaliwa vizuri. Kumekuwepo na upungufu wa walimu wenye sifa za kufundisha kwenye ngazi mbalimbali. Hao walimu wachache pia hawana nyumba za kuishi. Je, tutapataje elimu bora bila walimu bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza kwa kuanzisha mpango wa MMEM ambao unasaidia kumaliza upungufu wa nyumba za walimu na madarasa hivyo kuongeza idadi ya wanafunzi wa *Primary.* Mpango huu wa MMEM usiishie tu kwenye Elimu ya Msingi inafaa unendelezwe hadi Sekondari. Hii itatoa nafasi kwa watoto wengi angalau kuwa na Elimu ya Sekondari wananchi wameitikia wito wa kujenga shule tusiwakatishe moyo kwa jinsi walivyoitikia kujenga nyumba za walimu na madarasa kwa moyo ule ule wananchi tuwahamasishe kujenga shule na nyumba za walimu wa Sekondari.

Kuendelezwa kwa mfumo huu utatoa uwiano mzuri kwa wanaomaliza *Primary Education* kupokewa kwenye Sekondari, bila kuwa na uwiano mzuri tunavyoona tutakuwa na namba kubwa ya *Primary School leavers* na wachache kuingia Sekondari. Shule nyingi zaidi za Sekondari lazima zifunguliwe. Ukiritimba wa kuandikisha Sekondari nao lazima upungue. Mara nyingi kumekuwa na ukiritimba wa kuanzisha shule za sekondari kama ukiachwa hivyo ulivyo ni Sekondari chache zitaandikishwa na hivyo wanafunzi wachache watachukuliwa na kufanya wazo la wanafunzi wengi kumaliza angalau Sekondari.

Mheshimiwa Naibu  Spika, walimu wachache waliopo mashuleni wamekuwa wakikatishwa tamaa na maslahi duni.  Waziri wa Elimu na Utamaduni alikiri mwenyewe mbele ya Kamati ya Kisekta ya Huduma za Jamii mwezi Juni 2003, kuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni imekuwa na tatizo la upungufu mkubwa wa walimu wenye shahada, unaosababishwa na baadhi yao kuacha kazi ya ualimu Serikalini na kujiunga na shule zisizo za Serikali au kujiunga na ajira nyingine nje ya ualimu kwa kufuata maslahi bora. Pamoja na baadhi ya watu kudai kuwa walimu wana mishahara mikubwa, wanasahau kuwa walimu hawana marupurupu.  Si hivyo tu, bali walimu wengi huishi kwa kutegemea mishahara, tofauti na wafanyakazi wa Wizara na Idara nyingine ambao wanakuwa na posho mbalimbali.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu  Spika, Waziri wa Elimu ameeleza mpango wa kuboresha elimu nchini.  Ukisikiliza na kuangalia Vyombo vya Habari, kuna swali limekuwa likiulizwa kuwa mpango huu unaboreshaje maslahi na hali za walimu? Je, walimu na wazazi wamekuwa wakishirikishwa? Je, sauti ya wanyonge inasikika katika elimu?

Mheshimiwa Naibu  Spika, kikwazo kingine cha kupata elimu bora ni upungufu au ukosefu wa vyumba vya madarasa, vyoo, matanki ya maji. Pia kumekuwapo na uchakavu wa majengo na samani. Hii imekuwa ikihusisha pia upungufu au ukosefu wa vitabu (sio ajabu kukuta darasa zima linatumia kitabu kimoja), upungufu wa maabara na vifaa vya maabara. Suala la upungufu wa madawati bado ni kubwa pamoja na juhudi za Serikali kuwalazimisha wazazi masikini kununua madawati.  Wanafunzi wengi mijini na vijijini bado wanakaa chini (sakafuni au kwenye vumbi), hali ambayo husababisha wanafunzi wachafuke sana na kuwalazimu wazazi hohehahe kuingia gharama za sabuni za mara kwa mara.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu  Spika,  pamoja na mpango wa MMEM kununua samani za shule, ni lazima  Wazabuni  wenye uwezo wapewe ili madawati imara  yatengenezwe na Halmashauri za Wilaya zitoe tenda hiyo kwa wale watakaotengeneza madawati  imara ambayo ni ya chuma.

Mheshimiwa Naibu  Spika, katika hali na mazingira kama hayo, ni kichekesho kuongelea elimu bora kwa watoto wote wa Tanzania na watu wazima. Serikali itarejeshaje elimu ya msingi kwa wote *(UPE)* katika matatizo ya elimu yetu duni?

Je, watoto wote wenye umri wa kwenda shule wakiandikishwa hali itakuwaje? Waziri aliielezea Kamati ya Kisekta ya Huduma za Jamii kuwa Wizara imepanga kuongeza watoto wa rika linalopaswa kuwa shuleni *(Net Enrolment Rale - NER)* wa miaka 7 - 13 kutoka asilimia 88.7 mwaka 2002 hadi kufikia asilimia 90 mwaka 2005.  Je, Waziri anafahamu hali halisi ya matatizo yaliyotajwa hapo juu au anaambiwa tu na watendaji wake bila yeye kushuhudia?  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu  Spika, tunashauri Serikali iachane na maneno matamu ya ahadi nzuri zisizotekelezeka.  Kama CCM ilikiri wazi kuwa Ilani yake ya uchaguzi haitekelezeki, basi hata Serikali yake ikiri kuwa imekuwa ikitoa ahadi hewa. Tunaishauri

Wizara ya Elimu na Utamaduni, iachane na maneno kama Wizara inaandaa utaratibu mzuri wa ..., Wizara ina mikakati ya ..., Wizara inatarajia ..., Wizara inabuni au itabuni utaratibu bora/mzuri wa ... na Wizara inafanya mpango wa ... na kadhalika.

Mambo hayo yanapoahidiwa na kushindwa kutekelezwa, tutaambiwa kuwa kutokana na ufinyu wa Bajeti, lengo fulani au ahadi fulani halikutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kurejesha michezo na mashindano mashuleni na vyuoni ili Taifa liendeleze hazina ya michezo, ambayo maandalizi yake muhimu huanzia shuleni, limekuwa likijibiwa kwa kauli za kisiasa, wakati kiwango cha michezo kinazidi kuporomoka. Kauli za Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kuwa michezo shuleni na mashindano ya michezo yameruhusiwa ili mradi tu yasiingiliane na utaratibu wa masomo ni ya kisiasa. Ukweli ni kwamba michezo hiyo na mashindano hayapo na hayafanyiki. Nchi yetu inazidi kupoteza vipaji vya wanamichezo, ambavyo vilikuwa vinapatikana kupitia michezo na mashindano ya UMITASHUMTA, UMISETA na UMISAVUTA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha michezo na mashindano ya michezo mbalimbali mashuleni na vyuoni, Waziri wa Elimu na Utamaduni atoe kauli katika kikao hiki cha bajeti kwa kuwataka Wakuu wa Shule na wa Vyuo kuanzisha michezo na mashindano mara moja. Baadaye watendaji wa Wizara watembelee mashule na vyuo kuhakikisha kauli hiyo inatekelezwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona Serikali iwekeze katika michezo na mashindano kwenye shule za msingi na Sekondari. Leo Serikali ikiulizwa ni kiasi gani cha fedha kimetenga kwa ajili ya michezo na vifaa vya riadha Serikali haina jibu. Bila kuwekeza katika michezo Tanzania ijitoe katika kushiriki mashindano ya Kimataifa. Zamani Serikali ilikuwa inawekeza kwenye michezo ndiyo maana tulikuwa na nafasi ya kupata medali lukuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inalaani kitendo cha kutopatikana kwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa wakati. Takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2002/2003, Wizara ya Elimu na Utamaduni ilitengewa na Serikali jumla ya shilingi bilioni 38.3, lakini kufikia Aprili 30, 2003, Wizara ilipatiwa jumla ya shilingi bilioni 36.8 tu. Si hivyo tu bali katika mwaka huo wa fedha shilingi bilioni 2.4 za hapa na shilingi bilioni 80.9 za nje ziliidhinishwa kwa matumizi ya maendeleo. Kufikia Aprili 30, 2003, asilimia 53.3 ya fedha za hapa na asilimia 44.75 za fedha za nje zilipokelewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ucheleweshwaji wa fedha hizo, Wizara ya Elimu na Utamaduni inapata kisingizio kizuri cha kutotekeleza malengo. Kama hali hii itaendelea, malengo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ya muda mrefu hadi mwaka 2015 yatakuwa ndoto za mchana kufikiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya malengo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ni kukuza kiwango cha lugha na kukuza matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha. Suala la lugha ipi itumike kufundishia na katika mawasiliano limesababisha

malumbano makubwa kati ya wasomi, Vyombo vya Habari na wananchi wa kawaida. Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusiana na suala hili. Matokeo ya tafiti yanaonyesha kuwa kuna wananchi ambao wangependa lugha ya Kiingereza itumike, wakati wananchi wengine wanaunga mkono lugha ya Kiswahili. Kadiri ya tafiti lugha ya kufundishia ni mojawapo ya matatizo ya elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili siyo la kufumbia macho. Serikali yetu baada ya kusikiliza mawazo yanayounga mkono Kiswahili na mawazo yanayounga mkono Kiingereza, itoe kauli juu ya suala la lugha itakayotumika katika utoaji wa elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi walio chini ya Wizara ya Elimu, waishio Mikoani, kwa muda mrefu wamekuwa wakipata kero ya kusafiri toka Mikoani kufuata huduma Makao Makuu ya Wizara Dar es Salaam. Licha ya kero ya kusafiri na gharama zake, wafanyakazi wa Wizara, Makao Makuu huwa hawatoi ushirikiano wa kutosha kwa wateja kwa maana ya kutoa huduma bora. Suala hili limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu, lakini ufumbuzi wake umekuwa taratibu mno, na wakati mwingine wa nguvu ya soda.

Suala la kutoa faili toka ofisi moja kwenda nyingine, bado ni tatizo licha ya faili kutofanyiwa kazi kwa muda unaotakiwa. Licha ya mafaili suala la vikao Wizarani limekuwa likiathiri wateja. Sio kitu cha ajabu kwenda Makao Makuu ya Wizara ukimtafuta mkubwa fulani mara mbili au tatu na zaidi ukiambiwa anahudhuria kikao au vikao. Suala la madai ya wafanyakazi Wizarani limekuwa likichukua muda mrefu na kuzungushana bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo ni baadhi tu ya kero zilizopo Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kambi ya Upinzani inashauri huduma nyingi zihamishiwe ama Makao Makuu ya Mikoa kwa Maafisa Elimu wa Mikoa au kwenye kanda. Hii itapunguza gharama za kusafiri na kujikimu. Pia kwa kufanya hivyo itawapunguzia waajiriwa wa Wizara kero wanazokutana nazo pale Makao Makuu. Ni wazi kuwa kwa kufanya hivyo Wizara itakuwa imesogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma za Jamii iliambiwa kuwa Idara ya Ukaguzi wa shule na vyuo ilikuwa na lengo la kukagua shule za sekondari 561, lakini ni shule 529 tu zilizokaguliwa. Takwimu za Wizara zinaonyesha kuwa shule za sekondari 32 hazikukaguliwa. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu na Utamaduni, kupitia Idara ya Ukaguzi, haielewi ni kitu gani kinaendelea katika shule hizo, kitu ambacho ni hatari sana. Suala hili lifanyiwe kazi haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Elimu na Utamaduni aliieleza Kamati ya Kisekta ya Huduma za Jamii kuwa mara tu baada ya ukaguzi, ripoti hutumwa kwa wadau mbalimbali, kama Kamati za Shule na Halmashauri ili yatumike kuboresha elimu. Alisema kuwa taarifa hutumwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya au Halmashauri. Nakala hupelekwa kwa Mwalimu Mkuu, mwenye shule, Mkuu wa Chuo, Mkuu wa shule na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutuma ripoti ya ukaguzi bila kukutana na wadau wenyewe ana kwa ana na kujadiliana, halina maana. Wakaguzi wamekuwa wakikutana na Wakuu wa Shule au Vyuo bila kukutana ama na walimu au wakufunzi na kusikiliza mawazo na maoni yao.

Kambi ya Upinzani inaishauri Idara ya Ukaguzi iwe inakutana na watu hao ili kuboresha ukaguzi na ripoti zitakazoandikwa baadaye. Itakuwa vizuri kama wakaguzi hao watakuwa wanakutana na wanafunzi au wanavyuo kusikiliza pia maoni yao, kwa sababu wanafunzi na wanavyuo wengine ni wafanyakazi wa Wizara wa muda mrefu. Sio hivyo tu bali wengine wamewahi kufanya kazi hizo za ukaguzi. Bila kufanya hivyo ukweli wa ripoti za ukaguzi utakuwa na walakini. Pia ripoti za kuandaliwa mezani na kutumwa kwa njia ya posta zinaweza kuishia mezani au makabatini bila kufanyiwa kazi. Sio ajabu pia ripoti hizo zikaliwa na mende au panya licha ya kufunikwa na vumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wenzagu watakumbuka vizuri, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahi kutoa kauli na ahadi ya kulipa mishahara ya wafanyakazi na hasa walimu kila ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi. Agizo hili lilikuwa na nguvu ya soda, baada ya hapo, hali iliendelea kuwa kama ilivyokuwa mwanzoni au kuzidi hapo. Kitu cha kusikitisha zaidi, haijawahi kutolewa kauli nyingine ya kufuta au kuahirisha kauli ya awali. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali itoe kauli ya kufuta agizo la Mheshimiwa Rais kwa sababu halitekelezeki. Kama CCM, Chama Tawala, kilikiri kuwa IIani yake haitekelezeki, basi pia serikali yake ikiri kuwa agizo la Rais halitekelezeki. Wakati mwingine kukiri udhaifu ni suala la uungwana tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dira *(vision)* ya Wizara ya Elimu na Utamaduni isemayo: "Kutoa kwa wote elimu ya msingi *(UPE)* iliyo bora kama mkakati wa kupambana na umaskini, kupanua elimu katika ngazi zote na kutoa fursa sawa ya Elimu kwa Wote (EWO) iliyo bora kwa lengo la kuongeza uwezo wa kujiendeleza na wa kuchangia katika kukua kwa uchumi wa Taifa. Aidha, kuimarisha uendeshaji, usimamizi na miundombinu ya utamaduni."

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali inataka kufanikiwa katika dira hii, kwanza, ni lazima matatizo na kero zilizotajwa katika hotuba hii zitafutiwe ufumbuzi wa kudumu. Pili, Wizara idhamirie au ianze mikakati ya kutoa kwa wote Elimu ya Sekondari (USE) angalau hadi kidato cha nne. Thamani ya elimu ya msingi imekuwa ikipungua kadri miaka inavyokwenda. Tatu, katika ulimwengu wa sasa wa utandawazi *(globalization),* elimu ya kompyuta sio suala la hiari tena.

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ianze kufikiria kuingiza somo la kompyuta katika mitaala ya shule za sekondari na Vyuo vya ualimu. Bila kufikiria hilo dira nzima ya Wizara itawaacha Watanzania nyuma ya wengine. Kambi ya Upinzani imeikumbusha Wizara ya Elimu na Utamaduni katika mojawapo ya majukumu yake makuu, yaani kutoa

ushauri wa kitaalamu na kiufundi unaotokana na mahitaji na mabadiliko katika elimu na utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002/2003, Wizara iliagizwa na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuchukua hatua kali za kinidhamu na za kisheria kwa Halmashauri za Wilaya zitakazokuwa zimekiuka maelekezo ya matumizi ya fedha zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu. Katika utekelezaji wa agizo hilo, Waziri ameiambia Kamati kuwa pale ambapo palijitokeza kasoro, marekebisho ya haraka yalifanywa, ikiwa ni pamoja na kuwawajibisha wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwawajibisha wahusika peke yake halitoshi. Kambi ya Upinzani inashauri kuwafilisi watu hao kwa kuuza mali zao ili pesa iliyohujumiwa ipatikane na kuendelea kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Baada ya hapo, wadau wote wa ngazi zote wapate taarifa. Bila kufanya hivyo, ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu utakuwa hadithi za hekaya za Abunuwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa sasa wa kuwapata walimu wa daraja A kwa kuwa Chuoni mwaka wa kwanza (nadharia na vitendo) na kuwa shuleni mwaka wa pili (mafunzo kwa vitendo) ni mzuri sana kama utasimamiwa vizuri. Wasiwasi wa Kambi ya Upinzani ni jinsi vijana hao watakavyoishi wakiwa mashuleni. Je, Wizara kupitia Maafisa Elimu wa Wilaya, imefanya mpango wowote wa kuwawezesha kuishi vizuri wakiwa mashuleni? Kama kuna malipo yoyote wanapewa, je, malipo hayo yanatosheleza mahitaji yao? Je, fedha ya walimu hao kujikimu iko kwenye bajeti au Serikali inawataka wakajitegemee Wizara ya Elimu na Utamaduni iwe makini juu ya suala hili ili kuepusha vijana wetu wasiwe ombaomba na kushusha haiba *(personality)* ya ualimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za Wizara ya Elimu na Utamaduni zinaonyesha kuwa kasi ya kupanua elimu ya msingi nje ya mfumo rasmi wa shule MEMKWA na MUKEJA ni mdogo sana. Mwaka 2002/2003 programu za miradi hii zimepanuliwa kutoka Wilaya 13 hadi 17 tu. Wilaya zipatazo 100 katika nchi yetu bado hazijafikiwa na upanuzi huu. Kama kasi yenyewe ndio hii, je, zoezi hili litafikia Wilaya zote lini? Je, hali za vijana waliokosa mfumo rasmi wa shule katika Wilaya ambazo bado zitakuwaje? Maana yake ni kwamba Serikali ya CCM inaendelea kupalilia na kumwagilia ujinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuimarisha shughuli za utamaduni kwa shule za msingi limekuwa la upendeleo kwa Mikoa michache, hasa Dar es Salaam, Morogoro na Pwani, ambapo sanaa za maonyesho ziliendeshwa kwa ushirikiano wa Wizara na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kambi ya Upinzani inashauri kuimarisha shughuli za utamaduni mashuleni na vyuoni kwa kutumia kanda. Kwa kufanya hivyo wanafunzi na wanavyuo wengi watashiriki kwa gharama ndogo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango wa maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), baadhi ya Halmashauri zimeonyesha mapungufu makubwa pamoja na kupewa maelekezo sahihi na Wizara ya Elimu na Utamaduni. Mfano wa mapungufu ni

idadi kubwa sana ya wanafunzi katika madarasa, ucheleweshaji wa fedha za ruzuku, hivyo kuchelewesha ujenzi wa madarasa na ununuzi wa vifaa na vitabu. Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya Halmashauri hizi? Hali ya msongamano wa wanafunzi na ukosefu wa vifaa na vitabu katika baadhi ya shule za msingi hata sekondari inatisha sana. Hatua za kivitendo zichukuliwe haraka sana kuokoa jahazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi ambao wamepitia elimu ya awali (chekechea) wameonekana kufanya vizuri kwenye masomo yao ya elimu ya msingi. Hata hivyo, ni shule chache sana zinazoendesha elimu ya chekechea. Kambi ya Upinzani inashauri Waziri atoe agizo kwa shule zote za msingi nchini, ziwe na mafunzo ya elimu ya awali. Kama hilo litafanyika na kufanikiwa, basi darasa la kwanza liwe linaandikisha watoto waliopitia shule za chekechea tu. Kwa kufanya hivyo, tunaamini ubora wa elimu utakua maradufu kwa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya uandikishaji wa watoto wa miaka 7 katika darasa la kwanza ni kubwa sana. Kambi ya Upinzani inaipongeza Serikali kwa mafanikio hayo. Lakini, taarifa za Vyombo vya Habari vya ndani na nje ya nchi zinaonyesha kuwa zoezi limekumbana na misukosuko na matatizo mengi sana, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vyumba vya madarasa, ukosefu wa vitabu, ukosefu wa walimu na kadhalika; kama nilivyosema hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo haya ni lazima yatafutiwe ufumbuzi wa haraka sana kuepuka aibu mbele ya macho ya kimataifa. Serikali isifanye mambo kisiasa katika hili, vinginevyo tunaua Taifa la kesho na tutakuwa tunatafuta umaarufu wa kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya ongezeko la wanafunzi katika shule za msingi ni kubwa; lakini Waziri mwenyewe amekiri kuwa Serikali haina uwezo wa kuhudumia ongezeko la shule za sekondari. Waziri wa Elimu na Utamaduni pia amekiri mbele ya Kamati ya Kisekta ya Huduma za Jamii kuwa nafasi za kujiunga na elimu ya sekondari bado ni chache, ni asilimia 21.7 ya watahiniwa wote wa darasa la saba ndio hupata nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 78.3 hawapati elimu ya sekondari. Hiyo ndiyo hali halisi kwa sasa hivi. Je, hawa wanafunzi wanaoandikishwa sasa hivi wataishia wapi? Je, Serikali inaandaa Taifa la watu wengi waliomaliza darasa la saba? Je, katika dunia ya sasa elimu ya darasa la saba itamfikisha wapi mhitimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitahadharisha Serikali kuwa makini na jambo hili. Bila kuwa na mipango mizuri ya kuwaendeleza vijana hawa, tutakuwa tunatengeneza matatizo badala ya kufikiria tunatatua matatizo kwa kizazi kijacho. Itatulazimu kuwajibika kwa kuharibu kizazi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zilizofanyika zinaonyesha kuwa Maktaba nyingi za Vyuo vya Ualimu nchini zina vitabu vingi ambavyo vimepitwa na wakati *(outdated)* na havina uhusiano na yale yanayofundishwa kwa walimu-wanafunzi *(irrelevant*

*material).* Hali hii imetokana na kubadilishwa kwa mitaala ya mafunzo ya ualimu. Kwa hiyo wakufunzi na walimu wamekuwa wakitegemea moduli *(modules).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii, malengo ya Wizara ya kupanua na kuimarisha mafunzo ya ualimu, na hasa kuboresha mazingira ya kutolea mafunzo katika Vyuo vya Ualimu kwa kutoa vifaa bora vya kufundishia na kujifunzia ni ya kisiasa zaidi kuliko ya kitaalam. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iache mzaha wa kuwadanganya wananchi kuwa mambo yanakwenda vizuri kumbe hali halisi inaonyesha mambo yanaenda ovyo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ya Elimu ya Watu Wazima nchini inasikitisha. Kamati ya Huduma za Jamii ilitamka wazi kuwa Elimu ya Watu Wazima nchini imeshuka sana katika miaka ya hivi karibuni. Tamko hili lilitolewa katika taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mwaka 2002/2003. Idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika imekuwa ikiongezeka siku hadi siku. Kitu cha kushangaza ni kuwa Bunge hili limekuwa likiidhinisha kila mwaka fungu la fedha kwa ajili ya kufufua na kuendeleza elimu hiyo.

Pamoja na kulipa hononaria kwa walimu wa Elimu ya Watu Wazima. Lakini madarasa ya Elimu ya Watu Wazima hayapo huko Wilayani. Sasa Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri wa Elimu na Utamaduni alieleze Bunge hili ni jinsi gani fedha hizo zimekuwa zikitumika. Kama pesa hizo zilitumika kinyume na malengo basi wahusika wawajibike mara moja na Bunge lipewe taarifa katika kikao kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002/2003, Kamati ya Huduma Jamii iliagiza Serikali au Wizara itoe motisha *(incentives)* kwa walimu kutokana na kazi ngumu wanayofanya, kufuatia ongezeko kubwa la wanafunzi madarasani. Kambi ya Upinzani inaomba maelezo ya utekelezaji wa agizo hilo. Kama limepuuzwa tuambiwe pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya Upinzani imefurahishwa na kauli ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 iliyotolewa tarehe 16 Juni 2003 kwa kuona wazi kuwa elimu ya msingi peke yake haitoshi.

Pia Kamati imesema ukweli kuhusu hali halisi ya elimu nchini ambayo ni mbaya sana, nanukuu: “Hali ya madarasa ya shule nyingi za msingi na hata sekondari na nyumba za walimu ni mbaya sana. Kuna hatari ya kuendelea kujipongeza na kusahau hali halisi ya shule za msingi ilivyo. Kuna haja ya kuwa na mkakati mpana wa kuboresha majengo ya shule za msingi katika nchi yetu.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi hapa sio kuendelea kutoa takwimu nyingi na nzuri sana, wakati hali halisi inatisha. Takwimu zinazotolewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni ziwe pia zinalinganisha idadi ya Watanzania kadri ya sensa, vinginevyo tutaendelea kuwaona Watanzania wachache wenye uwezo wakipeleka watoto kupata elimu katika nchi za jirani. Hii ni pamoja na wakubwa kuendelea kupeleka

watoto wao kusoma nchi za nje, japo hawapendi kuambiwa hivyo na wanaweza kucharuka kwa kutaka takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na wimbi kubwa la kuanzishwa kwa shule za msingi zinazofundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza *(English Medium).* Hii ni hatua nzuri kwa sababu nchi za jirani kama Kenya na Uganda, zimekuwa na shule hizo kwa muda mrefu sasa. Tofauti yetu na jirani zetu ni karo ambayo imekuwa ikipanda kila kukicha. Pia ni vizuri Serikali ikaandaa mitaala inayofaa na inayolinda maslahi ya Taifa. Bila kufanya hivyo shule hizi zitakuwa zinatoa elimu ya viwango tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri wa Elimu na Utamaduni kutoa maelezo ya kina juu ya Shirika la Vifaa vya Elimu Tanzania *(Tanzania Elimu Supplies Company Limited).* Pia Waziri wa Elimu na Utamaduni aeleze hatma ya wafanyakazi wa Shirika hilo ambalo linaelekea kubinafsishwa. Kwa kweli Serikali inatenda dhambi kubwa sana kwa kuwatelekeza wafanyakazi wa Shirika hilo. Tulio wengi tumeshuhudia waliokuwa wafanyakazi wa Shirika hilo wakiomboleza juu ya kifo cha Shirika hilo. Tumeshuhudia kwenye Vyombo vya Habari, wafanyakazi hao wakikesha nje ya majengo ya Shirika hilo, wakidai kulipwa haki zao. Maisha ya wafanyakazi hao na familia zao yamekuwa mabaya sana kwa muda mrefu kutokana na likizo zisizo na malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Julai 5, 2000 Kambi ya Upinzani ilisema kuwa viongozi wengi wa kizazi kipya na pia wanasiasa waliopo sasa wameelimika kutokana na kazi nzuri ya Shirika hili. Takwimu nyingi na nzuri san zinazotolewa kwenye Bajeti za Wizara tofauti zinapatikana kutokana na kazi nzuri sana na kubwa ya Shirika hili katika miaka ya nyuma. Serikali ya CCM, kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni, ione aibu na kuomba radhi kwa usumbufu uliowakumba waliokuwa wafanyakazi wa *TES* pamoja na familia zao.

Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara ilipe haki zote za wafanyakazi na kuwapa mkono wa kwaheri. Tukishafanya hivyo twende makanisani na misikitini kutubu dhambi ya kuvunja amri ya upendo. Kwa kweli hatukuwapenda wenzetu kama tunavyojipenda sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa katika Wizara hii ni kuleta mapinduzi makubwa ya kielimu nchini Tanzania. Elimu iangaliwe upya na ubora uzingatiwe kwa makini; yawepo mazingira bora ya kutoa elimu. Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni iongezwe na fedha itolewe yote kwa matumizi ya Wizara kama ilivyoombwa ili Wizara ikamilishe malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza shughuli za elimu zitengewe asilimia 15 ya bajeti nzima. Kwa kufanya hivyo, matatizo na kero ndani ya Wizara yatapungua sana kama sio kwisha kabisa. Pia uongozi bora wa elimu kuanzia kamati za shule hadi Wizarani Makao Makuu uboreshwe. Wazembe, wababaishaji, wapenda rushwa, wawajibishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa elimu nchini upunguze maneno, ahadi na takwimu nyingi na nzuri sana masikioni, wakati hali halisi ni mbaya sana mashuleni na Vyuoni. Kinachotakiwa sasa ni vitendo. Hata wahenga wetu walisema: "Muungwana ni vitendo sio maneno."

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa jinsi mnavyoendesha Bunge la Vyama vingi. Pia nawashukuru sana Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, wakati Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, anasoma hotuba yake ndiyo nikakumbuka yale ambayo leo asubuhi Mheshimiwa Charles Kagonji, ameyasema. Maana kwa *speed* ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, ukichanganya na *speed* ya Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, mambo yanakuwa magumu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge kwanza nikumbushe tu leo asubuhi nadhani Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni ameleta *amendments* hizi nadhani ni za kwako za fungu mbalimbali. Ili vile vile kujibu aliyoyasema siku ile Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira.

Sasa nawakumbusha kwamba kuna *amendments* ambazo zimekuja pamoja na hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Sasa Wizara ya Elimu na Utamaduni inajadiliwa kwa siku mbili.

Kwa hiyo, kwa wale ambao hawako tayari bado siku ya kesho ipo, na mpaka sasa wale wote walioomba watapata nafasi. Maana kwa rekodi tulizonazo Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia ni 16 na Waheshimiwa Wabunge 16 kwa mwendo huu tunaokwenda mpaka wakati tunaahirisha Bunge usiku anaweza kubakia Mheshimiwa Mbunge mmoja tu kama atabaki.

Sasa hapa ninayo maombi ya wachangiaji ambao hawajachangia kabisa, Mheshimiwa Margareth Mkanga yeye ameomba kuchangia jioni. Lakini Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, hawa ndiyo watakaoanza kuchangia sasa hivi. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Rhoda Kahatano.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia katika Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kwa sababu bila shaka umeangalia kwamba mimi ni mwalimu. Napenda kukushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wapya ambao wamechaguliwa kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi hiki hongereni sana na ninaamini kwamba mtaleta michango mizuri hasa wale wenzetu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliorudishwa katika Bunge hili kwa sheria. Sheria ya nchi imewaruhusu hawa baada ya kufukuzwa. Kwa hiyo ninaamini kwamba wenzetu wa Kambi ya Upinzani wanaona kwamba nchi yetu sheria zake bado ni hai na hazina ubaguzi, kwa sababu hazimbagui mtu yeyote akienda Mahakamani kuliko kusemasema mahali pasipoweza kumsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na watumishi wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kazi nzuri wanayoifanya kuondoa ujinga katika nchi yetu, kwa sababu ndiyo msingi wa mambo yote. Nawapongeza sana kwa *speech* waliyoileta ambayo ni nzuri na nina hakika itatusaidia katika kupambana kuleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Elimu ya Msingi nimependezwa na juhudi zao wanazozifanya kuweka mipango na malengo yaliyo wazi ambayo bila shaka yakitekelezwa vyema yatatusaidia kuondoa shida za elimu tunazozipata katika nchi yetu. Kujenga majengo katika shule ni kusaidia kuwawezesha wanafunzi na walimu kufanya kazi zao vizuri na kwa uangalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado ninaona katika elimu msingi kwamba *ratio* ya mwalimu na mwanafunzi bado ni kubwa. Kwa hiyo, japokuwa tutajitahidi na tumejitahidi huko nyuma kuandikisha watoto wengi, lakini mwalimu hawezi kuwafundisha wote hao wakajua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona jambo hili juzi tulipokuwa kwenye Kampeni kuna vijana ambao huwa hawana wasaidizi ninawasaidia kuwapa vifaa wanasoma kule Bukoba na hapa Dar es Salaam ninao wachache. Lakini kila mara nawaambia nikiwepo mniletee vitabu vyenu niangalie. Sasa ninaona misingi wanayoipata pale itatusaidia zaidi kutoa wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika baada ya darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ambacho nimekiona labda Taasisi ya Elimu itanisaidia huko nje au hapa ni jinsi gani mitaala yetu ilivyo siku hizi, kwa sababu sielewi. Kwa sababu naona mtoto wa darasa la kwanza na la pili anaweza kufanya hesabu za maelfu. Wanapewa ninaona kwenye vitabu vyao ninavyoviangalia, hesabu za maelfu kujumlisha na kuzidisha ni kuzidisha ubongo wake jinsi nilivyojifunza ualimu zamani. Hasa mtoto wa namna hiyo hawezi kujifunza kitu chochote kwa sababu ni kama Volkswagen unaipakia mzigo wa tani kumi.

Hasa hiyo mimi naomba Waziri anisaidie hii Taasisi ya Elimu ya siku hizi ni tofauti na Taasisi ya Elimu ya zamani. Mipango iliyo kwenye kitabu alichotupa Waziri ni mizuri, lakini kwa kuangalia wanafunzi wachache ninaowasaidia mimi vitabu vyao vya hesabu shuleni naona ni kazi ngumu wanazozifanya zinazidi ubongo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najua mtoto wa darasa la kwanza anafundishwa heabu mpaka 9 na 10 ndiyo anacheza nayo. Mpaka unamwandaa halafu darasa la pili

mpaka 99 ili akifika yale makumi, mamia na maelfu. Sasa darasa la pili akiwa na maelfu mwisho mtampa matrillioni halafu tutaoa watoto ambao hawawezi kabisa katika nchi hii. Tutakuwa nao wengi darasani lakini kazi wanayoifanya naona haitawezekana.

Kwa hiyo, kwa Elimu ya Msingi mimi naomba Waziri aniambie taaluma zikoje, mitaala yetu ikoje, kwa nini watoto wanafanya mahesabu kuzidi uwezo wao. Pengine ni kwa sababu walimu labda hatujawaandaa vizuri, tumerashia rashia tu labda wamekimbia. Kwa hiyo, nilikuwa naangalia katika kitabu hiki ambacho kwa kweli naungana kabisa na Mheshimiwa Charles Kagonji na kabla Mheshimiwa Charles Kagonji hajasema nilikuwa nazungumza na jirani yangu kama kwa kweli Serikali inatuchezea sasa. Kutupa kitabu asubuhi hiyo hiyo na tuchangie ni kutupima uwezo wetu au ni kutudharau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu kama hiki tulipaswa kuwa nacho *weekend* nzima ili tuweze kutoa mawazo yanayostahili kumsaidia Waziri kama wanaona tunawasaidia. Lakini kama wanaona sisi ni sawa tu ni *rubber stamp* naomba jambo hili mkaliangalie na linatudhalilisha kabisa kupewa kitabu saa hiyo hiyo na kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la *UPE,* kweli ni jambo jema kwa sababu nchi zote zinapeleka wanafunzi wake wote shuleni. Lakini nafikiri pia tuwe na utaratibu wa mahudhurio ya lazima. Waandikishwe na walazamishwe kuhudhuria, hiyo itatusaidia. Namshukuru Waziri amesema michango shuleni imekatazwa, lakini kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri bado inaenda enda tu chini chini. Labda ni kwa sababu wakaguzi hawana nyenzo za kuwapeleka katika mashule na kuona mambo yanakwenda vipi. Bado michango ipo ya shilingi moja, moja kwa mtoto mmoja na kwa hiyo, mtu akiwa na wanafunzi mia moja kwa darasa la kwanza na la pili ujue tuition zinaanza darasa la kwanza. Kwa nchi ambayo elimu yake ni njema tuition hazina haja. Walimu wanatosha sisi sote hapa hatukupewa *tuition.* Walimu walifundisha.

Mimi nakumbuka nilikuwa nafundisha watoto wazito bila ya kupewa hata senti tano au mchicha wa baba mtu au mama mtu na Mheshimiwa Edward Lowassa, anashuhudia kwa sababu ni mwanafunzi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango namjulisha Waziri, mke wake Waziri wa Elimu ni mwanafunzi wangu. Pia michango inaendelea kichini chini sio siri. Kama wakaguzi wake ni wakaguzi kweli kweli wanajua hili hawamwambii, mtanisamehe labda kama kuna chochote. Lakini kama mnakwenda kikazi kweli mmeyaona hayo yapo. Jinsi gani tutayazima hayo Mheshimiwa Waziri Serikali imwezeshe kumpa uwezo wa wakaguzi waweze kwenda katika kila Shule ya Msingi na Sekondari sio kwa kuacha shule 30 au 32 kwa shule zote zikaguliwe kila mwaka ndipo tutaweza kupata ukweli wa maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipuuza elimu tunajipuuza wenyewe. Tunapuuza maendeleo ya nchi yetu, tunapuuza misingi ya kupata watu waaminifu. Kwa hiyo, mimi nafikiri wakaguzi katika Wizara ya Elimu na Utamaduni ndio moyo wa Wizara kwa hiyo wapewe nyenzo na waweze kufanya kazi kama tunavyopata kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na wenzake kwa kuboresha Shule za Sekondari na kuongeza nyingine mpya. Tumekuwa na matatizo ya watoto kutoingia Sekondari baada ya darasa la saba. Kwa hiyo, watoto wengi vijana wetu wamekuwa wanahangaika mijini kubeba mizigo. Unajua ndiyo maana mimi hata wakati ule wa *speech* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu bahati mbaya sikuwepo nilikuwa nimependa kusema juu ya uzawa, hawa wanaobeba mizigo ndiyo tunaowaita wazawa kwa kweli. Hujaona mtu wa aina nyingine anabeba mizigo na kuuza barabarani, wale wengine wana uwezo. Mwalimu alivyotaka kusawazisha mambo alitaifisha majumba. Sasa tusiwe tunavunga vunga mambo halafu tunafikiri tuko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usawa huu na uraia huu ni mzuri lakini una tofauti zake. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu mnaona wanafunzi wake pia ni wa namna gani. Kwa hiyo, Wizara hii ya Elimu na Utamaduni iweze kuimarishwa kwa sababu mnaona walioko huko ni wa aina gani. Wakimaliza Shule za Msingi warudi kujitegemea. Hivi kwa nini tunajipaka wenyewe mafuta kwa mgongo wa chupa. Eti wote ni raia ndiyo!!! Wote ni raia kwa sheria ya uraia, lakini kwa sheria ya uchumi tuko tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, shule zetu ziimarishwe kikweli kweli. Napenda kumwomba Waziri wamefanya vizuri kuwasaidia wasichana ambao wanatoka kwenye familia maskini, kweli nawapongeza sana, lakini tunao na wavulana. Tunao vijana wetu wa kiume wanatoka kwenye familia za kimaskini, naomba hao pia waangaliwe muweze kuwasaidia. Kwa sababu maskini wazazi wana watoto wa kiume na wa kike naomba pia wasaidiwe. *(Makofi)*

Kuhusu elimu ya awali naomba nguvu ziongezwe ile 550 haitoshi, shule hizo hazitoshi. Kwa sababu tuna shule nyingi za Msingi. Kuhusu Vyuo vya Walimu mimi sikubaliani na Wizara kuwa Mwalimu akae mwaka mmoja na mwingine akakaa field, kwa sababu wakaguzi hawapo. Yule kijana atakwenda kule kwenye *field* nani atamkagua.

Naomba Wizara iangalie vizuri jambo hilo. Mwaka mmoja wa kukaa chuoni hautoshi, naomba miaka miwili kama tunataka elimu ya kweli ya kushindana na raia wengine na Mataifa mengine, mwaka mmoja haitoshi. Tulikuwa na *Post Primary* ambazo sasa naona Wizara imezipa kisogo. Ubaya wa Wizara ya Elimu kila Waziri akija anakuja na mipango yake. Mwingine ataita Wizara ya Elimu ya Taifa, mwingine atasema kila kitu ni cha Taifa kwa hiyo, mtafuta tena humu humu. Sasa naomba vyuoni wakae miaka miwili. Kama wanataka mwaka mmoja uwe miezi sita labda itawatosha kukaa shuleni na warudi chuoni kuja kusema yale waliyoyaona kwenye *field* ndipo tutaandaa walimu wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipende kukimbia kimbia bila ya kuangalia warithi wa maendeleo ya nchi. Wewe ukiwa na watoto wawili unataka kucheza cheza tu na watoto hao na huyu unasema wewe ni sawa na huyu wewe ni sawa, wakati mwingine unamdanganya unaua uzao wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzawa wetu, watoto wetu wanaokwenda kwenye Shule za Msingi na sekondari tuwaandae ipasavyo, tuwaandae kujiendeleza baadaye, sijaona ni jinsi gani katika Bajeti hii nilipopita haraka haraka sijaona ni jinsi gani Waziri wa Elimu ameweka mambo ya kufundisha vijana hawa ili watakaporudi baada ya darasa la saba wajitegemee nyumbani, baada ya *Form Four* wajitegemee nyumbani, baada ya *Form Six* wajitegemee nyumbani sijui ni utaratibu gani ambao ameuweka.

Wakoloni walituwekea vyuo vya ufundi, vyuo vya kilimo baada ya darasa la nane na wale wakulima wazuri unaowaona huko vijijini wanaolima korosho vizuri, kahawa vizuri walio wengi ni wazee sasa ni wale waliomaliza darasa la nane. Sasa hawa wa *Form Four* wa darasa la Saba, wa *Form Six* una mpango gani wa hawa vijana watakaporejea nyumbani wamejifunza nini katika shule zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo naomba Waziri anisaidie. Katika kupunguza *pyramid* naiona inakwenda inakuwa nzuri lakini je hiyo *pyramid* hao waliokwenda kule wachache ndio watakaoweza kuja kumaliza matatizo ya nchi hii, wanaomaliza matatizo ya nchi hii ni wale waliobaki nyumbani walio wengi na hao ndio wanatusaidia sisi wananchi.

Kwa hiyo, kwa sababu naona muda wangu unakwisha napenda kurudia tena kumshukuru Waziri na wataalamu wake kwa hotuba nzuri lakini warejee kwa mambo hayo niliyoweza kuyazungumza. Nakataa kabisa mwaka mmoja chuoni. Mwalimu mwaka mmoja mnatuletea midioka huko vijijini hawatusaidii chochote. Kwa hiyo, tunaomba wafundishwe kwa sababu wale wana uwezo ukiwaandaa vizuri mkiwalipa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri kufikiria Watanzania wanaozunguka na mizigo mnawaita Wamachinga. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na kwa kweli napenda kumpongeza kwa hotuba nzuri.

Pia napenda kuwapongeza Wasemaji wetu wakuu wawili mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Elimu Mheshimiwa Khamis Ali Salehe, kwa hotuba nzuri ambazo kwa kweli ni *very challenging* na nafikiri Mheshimiwa Waziri akizifanyia kazi tunategemea kwamba sura inaweza ikawa tofauti mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpongeza Waziri kama alivyokwenda na *speed* yake kwenye *speech* nafikiri ndivyo anavyokwenda na *speed* katika masuala na mipango mizima ya elimu. Ana *speed* kali mno, anakuwa na mipango mingi mno katika muda mfupi. Sasa mimi nasema *speed* ni nzuri lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Charles Kagonji, nayo inafanya watu wanaweza wasielewe au wasimwelewe kwa yale anayozungumza

Sasa ni pamoja na mipango yenyewe. Ni kweli mipango aliyonayo Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake na Wizara nzima kwa ujumla ni mipango mizuri. Lakini vile vile ni vizuri kama tunataka itekelezeke vizuri tukaipa time frame hata ya muda mrefu. Vinginevyo tunaweza tukakuta tunachanganya mambo na wakati watendaji wetu ni wale wale tunaowafahamu na uelewa wao ni ule ule walimu wetu matokeo yake wanachanganyikiwa.

Sasa *outcome* yake inaweza ikafika mahali ambapo hata mipango mingine isitekelezeke. Hata hii mipango ambayo amezungumza Mheshimiwa Waziri kama ule mpango wa kutowacheleweshsha vijana wetu wanaohitimu kidato cha 4 au 6 na kuweza kuingia katika elimu ya juu.

Mimi ningeomba isiwe lugha ile ile aliyozungumza Mheshimiwa Khamis Ali Salehe, kwamba tuko katika mpango, tuko katika mkakati, tuko mbioni. Ningeomba hizo mbio na mikakati aliyozungumza kwamba anataka kukutana na wadau wengine, anataka kukutana na Wizara nyingine husika kwanza wakae na Wizara husika watoe mpango mmoja ambao unaeleweka upite katika Kamati za Bunge ueleweke na uridhiwe *then* uletwe kama mpango maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusije tukastukia nao ameuweka katika mipango yake ya elimu wakati tumesikia kuna MEMKWA, kuna Mpango Maalum wa Elimu ya Sekondari na unakuja sasa hii mipango mingi inaweza ikatuletea matatizo pamoja na kwamba ni mizuri, lakini bora ikapewa muda unaotosha mpango mmoja upewe kipindi fulani uonekane umefaulu na watu wameuelewa uletwe mpango mwingine then nafikiri tutakuwa tunakwenda vizuri. Japo tunajua imebaki miaka miwili mimi naamini kama mambo yakienda vizuri hata yeyote yule anayeweza akaingia madarakani anaweza akaridhia iendelee kutekeleza mipango hiyo ya miaka hata 15 endapo wananchi wa jimbo lako watakukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nichukue fursa hii pia kuwapongeza walimu wa Halmashauri ya Mji wa Bukoba. Shule za Wilaya yangu, jimbo langu limekuwa la kwanza katika nchi katika matokeo ya darasa la saba. Ni jambo la kujipongeza na nawapongeza kupitia Bunge hili na nawatakia kila la kheri katika kazi yao japo wanafanyakazi katika mazingira magumu lakini naamini kwa mwendo ule ule ambao tumedhamiria sisi wenyewe ndani ya jimbo letu na Wilaya yetu tutafaulu na huko mbele ya safari tutaendelea kukamata namba moja tu miaka nenda miaka rudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kazi nzuri ambayo walimu wetu wanafanya ningeomba kwa hivi sasa ile *concept* ya kufikiria wakati wote kwamba Ualimu ni kazi ya wito naomba tuanze kuiweka pembeni. Sasa hivi kazi ya Ualimu ni *profession* sawa na *professions* zingine ni kazi ambayo mtu anaangalia zaidi kumpa shibe, kumpa lishe ya kila siku sawa na daktari, *engineer* na *pilot.*

Kwa hiyo, kazi yoyote huwa inaenziwa. Sasa tusije tukajikuta tunakuja na *concept* hiyo tu Ualimu ni kazi ya wito. Sawa na bwana mmoja anavyo-*act* kwenye Luninga kwamba kazi ya Ualimu ni ya wito. Kipindi hicho kimepitwa na wakati.

Walimu wetu inabidi tuwaangalie maslahi yao, haitoshi kuboresha kujenga madarasa mengi ya *Primary,* haitoshi kujenga majengo mengi tu ya Sekondari, haitoshi kumwekea Mwalimu nyumba ya kuishi tukafikiri basi mambo yake yamekwisha. Hao walimu nao wanaishi katika soko huria kama tulivyojitakia sisi wenyewe. Wanapenda vitu, starehe wanapenda kupata mali. Tuliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda na fikra za Ualimu ni kazi ya wito hatufiki popote. Kwa hiyo, ndani ya mpango mzima wa kuboresha elimu kitu cha kwanza mimi naamini ambacho inapaswa tukiangalie pamoja na madarasa hayo walimu wapate kipato cha kutosha. Kwa kujua na mazingira waliyonayo, mazingira ya Mwalimu anapoingia darasani hana muda wa kuweza kutoka kwenda kuhudumia sijui banda la nguruwe, kuku au vinginevyo utajikuta huko kwenye madarasa wanafuma vitambaa, watauza vitumbua na maandazi na matokeo yake Mwalimu hata *attend* madaftari ya wanafunzi vizuri hata tayarisha somo lake vizuri na matokeo yake walimu wetu tutakuwa tunawafundisha wajinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba Walimu hawa mipango mbalimbali ambayo inapangwa na Serikali nao wafikiriwe. Hivi tunazungumzia kuuziana majumba watumishi wa Serikali walimu katika mpango huo wanaweza wakafaulu vipi kupata nyumba ya kununua ndani ya Serikali. Kama mazingira ya Mwalimu yanasababisha kwamba hawezi kupata nyumba hata siku moja ya kununua ya Serikali basi tuwatengenezee *package* maalum ya kuwakopesha ya kujenga nyumba ambayo anaweza akaimiliki kama nyumba yake na yeye akajua ndani ya mpango wa Serikali naye anathaminiwa na Serikali yake inamjali katika kazi anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba nizungumzie suala la mipango ambayo haitabiriki ya Serikali. Kwa kweli mipango hii inawafikisha wananchi kuweza kuiona Serikali kwamba ni *unpreditable.* Sasa hata sisi wawakilishi tunashindwa hata la kuzungumza. Kweli Serikali inakuwa labada na nia nzuri kwa mfano zilikuwepo shule za kutwa ambazo Halmashari zetu na wananchi ndani ya majimbo yetu walielekezwa wachangie yale madarasa ya kutwa wakatoa fedha nyingi wakachangia michango mbalimbali, madarasa yakajengwa na ikaongeza nafasi za watoto wanaomaliza darasa la saba. Lakini hata miaka haijapata mingi tu tangu mpango huu umekuwepo ndani ya *speed* ile ile kali ambayo ni nzuri siisemi kwamba sio nzuri ni nzuri lakini ukaja na mpango kwamba sasa shule za kutwa kwenye Shule za Serikali huo mpango umekwisha.

Je, wakati tunaupanga huu mpango tulikuwa tumeweza kuupa muda gani na wale watekelezaji wa mpango huo tuliwaeleza hayo kwamba jamani huu mpango aidha, ni wa majaribio au ni wa muda wa miaka 30 ijayo baada ya miaka 30 muwe mmepanga mipango mingine tofauti ambapo mnaweza mkajenga majengo ya kutwa?

Sasa mimi ningeiomba ili kuondoa hilo ni vizuri Serikali ikawa inatoa kwa uwazi kabisa mipango inayotolewa ili hata wananchi wa maeneo husika kama Bukoba Mjini ambako tumeathirika na mfumo huu kwa sababu ndani ya jimbo langu wanafunzi zaidi 500 ambao wamefaulu walikosa nafasi baada ya kupokea utaratibu huu kwa ghafla kwamba huu mpango umesitishwa na wakati tulikuwa tumeelekeza nguvu zetu katika

shule hizi za kutwa ndani ya Shule za Serikali. Sasa kama tunataka kuweka utaratibu mzuri ambao unaweza ukawa wa kuaminika basi ni vizuri tukafika mahali tukawekeana mkataba na kati ya wananchi na Serikali kwamba bwana shughuli hii tunavyoifanya tunaifanya kwa utaratibu huu kwa muda miaka fulani na kwa mkataba huu kuliko kwenda katika mazingira ya kugeukana na mipango ambayo *unpredictable.* Mipango inakuja tu katika njia za ghafla ghafla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na suala hilo ningemwomba Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa ana-*wind up* atueleze sisi hatima yetu ni nini. Wananchi wa Bukoba ambao tumepewa mwaka mmoja. Tunashukuru kwa hatua hizo ambazo Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wameweza kutupa *opportunity* hiyo ya kuweza ku-*accommodate* baadhi ya wanafunzi lakini muda tuliopewa wa kuhakikisha tumejenga shule za kuwa-*accommodate* namba nzuri ya mkoa wetu wa Bukoba nzima wanaoshinda kwa wingi sana bila matatizo yote. Kwamba tutafanyaje iwapo tutafikia mwisho wa mwaka huu na nafasi hizo na shule hazijaweza kujengwa kiasi cha kuwa-*accommodate* wanafunzi wote ambao watakuwa wamefaulu.

Sasa hivi tumeanza, jitihada zipo, lakini nina wasi wasi huo kwamba wanafunzi wataendelea kushinda na nafasi zitakuwa chache sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri anipe uhakika huo namna gani twende kwani haikuwa nia yetu katika kutokuwa na mpango wa kuwa na shule nyingi za kutwa ulikuwa ni mpango tu mzuri ambao tuliitikia wito ule wa Serikali wa kujenga madarasa kwenye shule zile za Serikali, sasa ningeiomba tupewe utaratibu jinsi utakavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalize kwa kuwapongeza na kuwashukuru watu wote binafsi wanaojenga Mashule ya Sekondari na Msingi. Nawapongeza sana na hasa nikiongezea na wewe Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa kuonyesha mfano huo kuwa na shule moja nzuri tu, sana. Kwa kweli tunajua kazi ilivyo ngumu ya kujenga shule. Tunaona katika vijiji vyetu, katika Wilaya zetu inapokuja mtu kukaa, kijiji kukaa, kata kukaa mpaka mkajenga shule ni kazi kubwa.

Sasa inapotokea mtu na mke wake au na marafiki zake na ma-*Director* wenzake wakaweza kubuni mradi na ukawepo wa kuwezeshwa kujenga shule si kazi ndogo. Ni kazi kubwa na ambayo inapaswa ipongezwe. *After all* nafikiri inapunguza mzigo hata kwa Serikali. Hawa watu wanapunguza mzigo mzito wa Serikali. Badala ya Mheshimiwa Waziri hapa anazungumza namna gani accommodate wanafunzi wa sekondari sijui elfu ngapi lakini hawa watu mimi nafikiri ni watu ambao kwa kiasi kikubwa wanaisaidia Serikali katika kuweza ku-*accommodate* wanafunzi wetu. Sasa hawa watu tunawasaidiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba sawa na jinsi ambavyo uliwekwa mpango maalum wakati wa kujenga Makao Makuu Dodoma ambayo mpaka sasa hivi miaka 40 haijakuwepo uliwekwa mpango maalum wa kuwasaidia watu wote wanaojenga, wanaowekeza hapa walio-*invest* hapa kwa kupunguza kodi ya baadhi ya vifaa vya ujenzi. Hivi kuna tatizo gani Serikali ikitoa upendeleo maalum au ikatoa taratibu maalum za

kuwezeshwa watu wanao-*invest* katika kujenga mashule kuweza kusamehewa baadhi ya kodi ya vifaa vya kujenga.

Mimi nafikiri kwa njia hiyo tuta encourage watu wengi kujenga shule nyingi za kisasa, shule ambazo zinaweza kuwa na *structure* za kutosha kwa wanafunzi wetu badala ya kuwaacha tu wakaelea elea kwa jinsi wanavyojua. Mimi naamini tukiwasaidia, Serikali ikiweka mipango maalum ya kuwasaidia na kuhakikisha kwamba vifaa hivyo kweli vinaelekezwa katika kufanya kazi hiyo ya kujenga mashule ninaamini katika muda mfupi tutakuwa na mashule ya kutosha ambayo yatawezesha wanafunzi wetu wengi kuweza kujiunga shule hizo na kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kupigiwa kengele ya pili, naomba kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake wote kwa hotuba nzuri na mipango mizuri ya elimu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami ya kuweza kuchangia asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote nami naomba kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge ambao walioingia ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wale walioingia kwa mujibu wa sheria. Dada zangu karibuni ili tuendelee. *(Makofi)*

Pili, nachukua nafasi hii kutoa pongezi kwa Waziri na watendaji wake wote Katibu Mkuu na watendaji kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ambao wameiandaa imeweza kutusaidia sisi Wabunge kutoa mchango wetu ambao utasaidia sana. Tatu, naomba kupitia Bunge hili kutoa pongezi kwa Rais wa *CWT* ambaye ni Mama Sitta, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuweza kushirikiana na walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kuweza kumsaidia Mbunge mwenzangu ambaye ni Waziri Kivuli kwa hotuba yake ambayo aliyoitoa.

Kwanza napenda kumpongeza ametoa vizuri kwa haraka sana kupita hata Waziri wetu maana yeye alikuwa anasema mengine hata hatuwezi kuyasikia vizuri.

Pili, kuweza kumsaidia kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, chama kilichopo madarakani si kama inakiri kuwa haitimizi yale ambayo yaliyowekwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hii napenda kumsaidia wazo hilo alitoa na wala asiwenalo. Kama angekuwa anapitia hotuba zote za Waziri wa Elimu toka mwaka 2000 ambapo mimi mwenzie Mbunge nilianza toka 2000 ingawa yeye ameingia kuanzia 2003 hotuba zile zingeweza kumsaidia zaidi katika kuboresha hotuba yake ambayo ameitoa leo. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii si kwa yeye na Mawaziri Kivuli wengine wote waweze kupitia hotuba zote za Mawaziri ambao bado hawajatoa hotuba zao za kuanzia mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuanza sehemu ambayo naweza kuchangia mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Elimu. Lakini nashukuru Mheshimiwa Waziri amegusa mahali ambapo nilipotaka kuanzia sehemu ya wanafunzi kuzidi kujaa madarasani. Nashukuru Waziri ameeleza wanafunzi mpaka sasa waweze kuwa arobaini na nina imani utaratibu huo utafanyika na utaendelea kuwa mzuri zaidi ili kuweza kusadia walimu waweze kufanya kazi zao hasa pia kuweza kuwatambua wanafunzi wao. Kwa sababu Mwalimu atakapoweza kumtambua mwanafunzi wake aliyeko darasani itakuwa ni vizuri zaidi hata kuelewa maendeleo yake yule mwanafunzi anakuwaje na ataweza kumsaidia kwa namna gani. Nashukuru sana Wizara kuona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la masomo. Nashukuru Wizara imejitahidi sana kuweza kusaidia masomo mengi, vijana wengi wanaweza kujielimisha na hasa suala la Ukimwi wakianzia bado Shule za Msingi. Lakini kuna somo lingine ambalo tumeweza kulisahau nina imani sasa hivi kama tutaweza kulikumbushia kwa kuwa Katibu Mkuu wetu ni mwanamke naye atakuwa kipaumbele zaidi kulisimamia zaidi somo hili la Sayansi kimu ambayo lilikuwa linaitwa *Domestic Science.* Shule nyingi zilikuwa zinafundisha wanafunzi wengi wakiwa shuleni waweze kusoma hasa kujua kupika, usafi, kushona na mambo mengine mengi ambayo yaliweza kuwasaidia wanafunzi hasa mama zetu wengine hawana muda ambao watakaoweza kujifunza masuala ya kupika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo akinamama ambao wamepitia kwenye Shule za masomo haya ya *domestic science* wameweza kuwasaidia hata ukubwani wanajua kupika. Wanawake sasa hivi muda mwingi wanautumia katika masomo na kama mtu anakaa mbali, mfano katika Jiji la Dar es Salaam utakuta mtu anarudi nyumbani saa mbili usiku au mwanafunzi anafika nyumbani saa mbili usiku, siyo rahisi kuweza kusaidiana na mama yake au mlezi yeyote kujifunza kupika. Itakuwa ni vizuri zaidi kama atapata mafunzo hayo akiwa shule kama ni mojawapo ya masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu Elimu ya Watu Wazima. Namshukuru Ndugu yangu wa Kambi ya Upinzani, naye amezungumzia suala hilo, ni bora zaidi kurudisha utaratibu huo katika Wilaya zetu hadi katika Kata ili Wazee wetu waweze kujielimisha kwani suala hilo linawasumbua sana hasa wakati wa kupiga kura. Watu wengi wanapenda kuchagua mtu yule wanayemhitaji, lakini kutokana na kutojua kusoma, mtu hajui labda huyu ni Aziza ambaye ni lazima nimpe kura ya ndiyo, inampa shida sana inabidi aanze kuchagua mtu mwingine, mfano, Mutungirehi au Lwakatare, kwa sababu haelewi kusoma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri asimamie vizuri suala hili, kwa sababu ni muhimu sana kwetu kwani litatusaidia katika upigaji kura. Hatukatai tunachukua takwimu za wapigakura, lakini pamoja na kuchukua takwimu hizo, hicho ndiyo kigezo kikubwa kinachotusumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuzungumzia kuhusu vijana wa kike ambao wanasoma Shule za Msingi au Sekondari. Wapo vijana wengi ambao wanapata mimba wakiwa Shule za Msingi, wengine wakiwa hata darasa la saba na

inapotokea hivyo kijana aliyepata mimba hataweza kupata nafasi ya kuendelea kusoma au hataweza kufanya mtihani wa kumaliza Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Sheria au kitu kinachoonyesha kwamba mwanafunzi huyo akishajifungua anaweza kurudi darasani au kuendelea na masomo yake na kufanya mtihani. Hiyo itakuwa ni kumnyima haki mtoto wa kike, kwa sababu akishajifungua atakaa nyumbani na huko atakuwa amerudi nyuma kielimu.

Naomba kuwe na utaratibu wa watoto wa kike wanaokatisha masomo yao kwa ajili ya kubeba mimba warudi shuleni na kufanya mitihani yao na waendelee na masomo kama itawezekana. Naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake kwa ujumla waliangalie suala hili kwa kina ili vijana wengi waweze kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Walimu. Napenda kuchukua nafasi hii kueleza kwamba sijui ni utaratibu gani unaotumika katika kuwapandisha Walimu vyeo. Nadhani kuna utaratibu mzuri unaotumika, lakini wapo Watendaji ambao wanaweza kuwa wanaukwamisha. Kwa kuwa tunafanya kazi kwa mafaili, mtu anaweza akaandikiwa kwenye faili lake *XX* kibao na unaweza ukajikuta kila siku hupandishwi cheo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna utaratibu huo napenda Wizara ya Elimu itume watu wake hata chini ili kuweza kuchunguza Mwalimu yule anafanya kazi kwa utaratibu gani na si kwa kutumia faili peke yake. Sisi ni binadamu, tunaweza kutumia njia nyingi kuharibiana mafaili yetu na si kama kupiga kura, kwa sababu kwenye kupiga kura mtu anachaguliwa. Kwa hiyo, naomba suala hili lifuatiliwe ili Walimu wetu wale ambao wamekaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo, wapandishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara ya Walimu, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alichukua nafasi hii kulilia mwenge katika Jimbo lake la Sikonge. Nami nachukua nafasi hii ili nililie matatizo yanayowakabili Walimu yapunguzwe ili nao wapate mahitaji yao mengi. Kilio hiki hakiishii hapa, ninamuomba Mheshimiwa Waziri aangalie suala hili la Walimu wanaotoka mbali kufuata mishahara yao kwenye Halmashauri ambazo ziko mbali kwani wanatumia pesa nyingi na muda mrefu na wakati huo huo wanafunzi wao wanakosa masomo. Nina imani kilio changu hiki kitakuwa kikubwa hadi pale Mheshimiwa Waziri atakaponiambia kuwa tatizo hili limekwisha ndiyo nitakapoacha kulia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kugongewa kengele ya pili, lakini napenda nitoe ombi kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake. Tabora kuna Shule ambazo ni za kihistoria, Viongozi wengi ambao wamo ndani ya Bunge hili na wengine ambao wako nje ya Bunge wamesoma katika Shule ya *Tabora Boys* na wengine *Tabora Girls.*

Napenda kuchukua nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Waziri aziangalie Shule hizo ambazo zipo katika Mkoa wa Tabora, kwa sababu ni Shule za kihistoria, tuweze kuziimarisha kwa kuzikarabati ili ile historia isiweze kufutika, iendele kuwa historia juu ya historia ambayo italeta manufaa katika nchi yetu na kutuletea sifa si Tabora peke yake bali katika nchi yetu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti ya Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa jinsi alivyojitahidi kuwasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu, ukiachilia mbali kuisoma kwa haraka kutokana na muda mchache aliopewa ambao naamini Kamati husika itashughulikia suala hilo kwa ufanisi wetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda niipongeze na niiunge mkono hotuba iliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii iliyokuwa ikichambua kwa ufasaha hotuba ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kama ilivyowasilishwa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja pale ambapo Kamati imezungumza ikiwa inaunga mkono Dira ya Wizara ambayo napenda niinukuu kama ilivyo: "Kamati ilikubaliana kwamba mwelekeo wa Dira ya Wizara kuwa inakidhi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwani inalenga kuona kuwa Wizara inatoa elimu bora katika ngazi zote ili Taifa liwe na watu wengi wenye elimu bora na maarifa yatakiwayo katika kutatua matatizo ya jamii kukabiliana na mabadiliko yatokanayo na maendeleo na kuwa na uwezo wa ushindani."

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia hoja zote hizi mbili, napenda kutoa masikitiko yangu kuhusu mchangiaji wa Upinzani aliyesema kwamba Serikali imeshindwa kuondoa maadui watatu na akitaja kwamba ni ujinga, maradhi na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwamba mchangiaji huyo hakusikiliza vizuri na wala hakusoma kwa makini ile hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni. Nitanukuu maneno machache sana ili kumkumbusha na yeye achukue kitabu asome, akiangalia pale katika Ibara ya 14.2 imeonyesha kwamba: "Watahiniwa waliofaulu mtihani wa Taifa kidato cha 4 katika daraja la *I - III* katika Sekondari za Serikali wameongezeka kutoka 35.6% - 45% na zile Sekondari zisizo za Serikali ukiondoa *Seminary* zimetoka 28.7% - 37.7%. Ibara ya 14.4 inaonyesha kwamba, wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha 5 katika Shule za Serikali ukilinganisha na mwaka 2002 ongezeko ni 12.7%.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuendeleza mengi, lakini hayo yanatosha kuthibitisha kwamba Sera za Chama kilichopo madarakani, Chama cha Mapinduzi, zinatekelezeka na Serikali iko makini kuhakikisha kwamba inajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kuendelea kupunguza kero za Watanzania na kujitahidi kwa kile inachokipata kuhakikisha kwamba Watanzania wote wananufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kwamba, tumezoea kusikia kitu kinaitwa usalama wa raia na tunaona kwamba hiyo ni kazi ya Askari Polisi na watu wengine na kwamba kila raia ajiangalie mwenyewe kwa usalama wake na mali zake kabla ya kutafuta usalama wa Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunatakiwa kuangalia kitu kinaitwa usalama wa elimu. Kwa utaratibu wa karne ya 21 tulionao ambapo tunashindana na ambapo nchi yetu sasa katika nchi ya Afrika Mashariki, Afrika na Dunia kwa ujumla tunayo kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa katika usalama wa hali ya juu sana. Kwa msingi huo, zipo nyanja nyingi za kuzingatia ili kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa katika usalama. Huwezi kushindanisha watu wasioweza kushindana hasa tunapozungumzia suala zima linalohusu elimu!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hilo napenda kuangalia kitu kinachoitwa ada kwa maana ya ada ya Elimu ya Sekondari kwa Shule za Serikali, ambapo ndipo hasa Serikali ilipoweka nguvu zake na mara nyingi ndipo hapo tunapotoa Bajeti na vitu vingine vya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ada ya Elimu ya Sekondari imegeuka kuwa ni kero sasa kwa sababu haitupi ushindani wa kutosha kwa *speed* ambayo tutaipenda. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuondoa kero ya ada kwa wanafunzi wa Shule za Msingi, lakini ukiangalia wale ambao wanamaliza darasa la saba ili kwenda kwenye Elimu ya Sekondari kikwazo kikubwa sana kimekuwa ni katika ulipaji wa ada. Serikali imeangalia mambo haya na hata inatoa fedha za ada kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi waliofaulu na wasiokuwa na uwezo wa kulipiwa ada na wazazi/walezi wao. Lakini kwa kuwa ada hii inawakabili wengi na ambao wana uwezo mdogo, waliokuwa wanashindwa kukabili ada za Shule ya Msingi, tatizo hilo linaendelea kuwakabili wale ambao wanakwenda katika Shule za Sekondari ya Serikali. Kwa msingi huo, ninaunga mkono hotuba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, iliyopendekeza kwamba, ada iangaliwe upya ama ifutwe katika Shule za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo na kwa *speed* ya Serikali yetu ilivyo, ninaamini tutaendelea kupata ongezeko la mapato yetu ya Serikali. Ninashauri kama inawezekana katika Bajeti ya mwaka ujao wa 2004/2005, basi kuwe na uwezekano wa kufuta ada ya Shule za Sekondari, kwa kuanzia zile za Serikali, ili kuweza kuipa nguvu Serikali yetu, kwamba wanafunzi wote wanaofaulu kuingia kidato cha kwanza waweze kuanza na vile vile, wasimamiwe katika mahudhurio yao ili waweze kumaliza kidato cha nne na kuendelea mpaka kidato cha sita kwa wale wanaofanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha Elimu ya Sekondari ni lazima mazingira ya Walimu yawe bora. Katika Jimbo langu la Muleba Kaskazini mwezi Januari mwaka huu, Walimu walitoa kwangu kilio cha kuhitaji mikopo tena midogo midogo. Nashauri kuwe na utaratibu mzuri wa kuwasaidia mikopo Walimu hawa tena mikopo midogo kama baiskeli, televisheli, pikipiki, mabati na kadhalika. Badala ya kuiachia *TUNAKOPESHA Ltd.* peke yake kuwa kama ndiyo njia ya kusaidia Walimu, basi kuwe na utaratibu mzuri

wa kuwasaidia ili wakidhi mahitaji yao kwa vitu ambavyo ni vidogo, lakini ni vya muhimu katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuzungumzia kuhusu suala la ukaguzi. Akisoma hotuba yake, Waziri wa Elimu na Utamaduni alisema kwamba, lengo la mwaka huu ni kupeleka masomoni wakaguzi 127. Lakini nikiangalia mahitaji ya wakaguzi ni 1,269.

Kwa hiyo, kama ndiyo itakuwa mtindo huu juhudi haiongezwi, nafikiri itatuchukua miaka 10 (kama nimefanya hesabu sawasawa) kuwafundisha ama kuwapa elimu wakaguzi wetu tunaowahitaji na iwapo Mwenyezi Mungu kama atatusaidia hakuna aliyefariki dunia, hakuna aliyeacha kazi na wala hakuna aliyekumbwa na mustakabli huu au ule. Elimu bora bila wakaguzi haiwezi ikaenda vizuri, nashauri suala hili liangaliwe vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mishahara ya Walimu pamoja na wakaguzi itazamwe upya, waongezewe mishahara inayoweza kukidhi mahitaji yao. Kazi wanayofanya Walimu ni kubwa sana, naweza kuwafananisha na hata wenzetu wa *TRA* ambao wanapewa mishahara mizuri. Investment yetu kwa Walimu ni kubwa mno na haina mfano! Kila mmojawetu hapa amepitia kwa Mwalimu na kila mmoja ukimuuliza, atakiri kwamba umahiri wa Mwalimu wake ndiyo umemfikisha hapa alipo, tena si ajabu ni yule Mwalimu wa darasa la kwanza na la pili. Binafsi nakiri kwamba Mwalimu wangu wa darasa la kwanza na la pili ndiye aliyeweza kunifikisha katika hatua niliyonayo leo. Kwa msingi huo, nashauri sana mishahara ya walimu iangaliwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, napenda kuzungumzia suala linalohusu fedha za kusaidia kusomesha watoto wanaotoka katika familia maskini. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema kwamba, mwaka jana kuna shilingi bilioni 1.1 zilizotolewa kugharimia watoto wa familia maskini. Ninapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo, lakini nina tatizo moja linalonifanya nizungumzie hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hoja hiyo imetoka, Wakurugenzi waliachiwa wenyewe wapeleka maombi ya wanafunzi hao Wizara ya Elimu, ili wapatiwe misaada hii. Suala hili limesababisha malalamiko mengi sana kwa sababu wale wanafunzi waliopata misaada hiyo si kwamba wote ni walengwa, bali ni watu ambao wazazi wao walifikiria na kuona kwamba sisi hatuna uwezo, wakapeleka barua za maombi na ilipotokea nafasi basi ndiyo walionekana kwamba ni wahitaji zaidi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri ule utaratibu unaotumika kwa *TASAF* uigwe kwa sababu Wanakijiji wanajifahamu yaani iwe wale wanaopendekezwa kupata misaada hiyo ya Serikali ya kusomeshwa kwa ajili ya kutojiweza kwa familia zao, watamkwe na Wanakijiji wote na orodha ya wanafunzi wanaohitaji kusomeshwa na Serikali ipelekwe mapema kabla ya kufanya mitihani yao ya darasa la saba, ili wale watakaokuwa

wamefaulu na kweli walikuwa katika orodha ile iwe ni moja kwa moja majina yao yanapitia huko huko badala ya majina kwenda baada ya mwanafunzi kuwa amefaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ninalifananisha na ule utaratibu unaotumiwa na Tume cha Uchaguzi wakati wa kuchagua nafasi za Viti Maalum, majina yanatangulia bila kungoja ushindani, matokeo ya ushindani yakija yanakuta majina yalishafika kunakohusika, kwa wale wanaostahili kwenda orodha inakuwa imeshafika huko na kwa wale ambao hawakupata nafasi wanabaki. Hii inaweza ikaondoa malalamiko na itazingatia wale ambao ni wahitaji wa kweli kwa sababu Wanakijiji wote watakuwa wamekwenda kujadili hali ya wazazi/walezi wote katika kile Kijiji, kabla hata watoto wao hawajafanya mitihani yao ya darasa ya saba.

Kwa hiyo, hakuna upendeleo wala wasiwasi kwamba mtoto anayetoka kwenye familia yenye uwezo anaweza kuingizwa kwenye orodha ya watoto ambao familia zao hazina uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, suala hili lizingatiwe kwa watoto wote. Ninapongeza msaada uliotangulia kwa ajili ya watoto wa kike, lakini napendekeza na watoto wa kiume nao wawe wanapewa nafasi sawasawa na wale wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napendekeza kuwe na mgawanyiko sawa katika eneo la Wilaya husika linalopewa msaada. Kama Wilaya ile ina Jimbo moja, basi Kata zote ziingizwe katika kusaidiwa au kama Wilaya ile ina Majimbo zaidi ya moja, basi Majimbo yote yaingizwe katika kusaidiwa sawa sawa, kwa sababu wahitaji katika Taifa letu wako katika kila eneo, hakuna Jimbo wala eneo linalozidi eneo lingine, ili mradi tu mwananchi yule mwenye kuhitaji anakuwa anafahamika zaidi katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo napenda kuzungumzia kwa siku ya leo ni kitu kinachoiwa MEMKWA. MEMKWA ilianzishwa na sasa hivi ni kama mwaka wa tatu, lakini naona kama ni mpango ambao hautekelezeki na unakwenda kinyume na *Universal Primary Education* ambayo inasema: “Kila mtoto anayestahi kwenda shule ni lazima aende.”

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi waliachwa kuandikishwa Shule kwa sababu walizidi miaka saba, matokeo yake ni kwamba hata mwaka uliofuata hawakuchukuliwa na wanazidi kukua, wengine sasa wana miaka tisa au kumi. Kwenye Jimbo langu kuna watoto ambao wameshindwa kwenda Shule kwa sababu walikaa kusubiri MEMKWA! Sijui katika Wilaya ya Muleba ni lini hii MEMKWA itatekelezeka!

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kama suala hili linazidi kuchelewesha wale watoto ambao wangeweza kwenda shuleni, kuzidi kukaa nyumbani. Kama mtoto akiwa hakupata nafasi ya kujifunza akiwa na miaka saba, basi ahudhurie Elimu ya Watu Wazima na ni vema hata hiyo ingesimamiwa kuliko hali ilivyo sasa, ambapo watoto wameshindwa kupata elimu. Nina mifano halisi ambayo naweza nikaitoa kama Mheshimiwa Waziri atahitaji, lakini nimeona niongelee suala hili kwa sababu naona kama watoto wanapata matatizo. Kuna maeneo ambayo mawasiliano hayafiki na

utaratibu huo umesikika tu na mpaka sasa hakuna utaratibu wowote unaoeleweka katika kuwashughulikia!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, napenda kutamka kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nimesimama kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Wataalam wake kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuelimisha Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kutumia nafasi hii kumtakia afya njema Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambaye ni mgonjwa na amekuwa ni mtumishi mzuri sana ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ni nzito, ina mambo mengi mazito, lakini muda hautoshi. Mtindo ambao Wabunge tumejiwekea wa kila mmoja kuzungumza dakika tano bila kujali uzito wa hoja, kwa kweli hautusaidii. Sasa, nimepewa dakika 10, ni lazima niende kwenye hoja. Natumaini nitapata muda wa kuchangia mawazo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ndio wanaofanya kazi ya kuelimisha Taifa hili. Kama ni kweli kwamba ubora wa Taifa lolote lile hutegemea ubora wa elimu inayotolewa kwa watu wake, basi ni kweli kuwa matatizo ya Walimu na elimu yanaathiri ubora wa Taifa letu na hali ya baadaye ya Taifa letu itategemea na aina ya elimu itolewayo hivi sasa.

Walimu wetu wanaishi maisha gani? Katika Wilaya yangu ambayo ina ukubwa kama Mkoa wa Kilimanjaro, kila mwisho wa mwezi Walimu hukusanyika Makao Makuu ya Wilaya kungojea wapate mishahara yao. Wakati mwingine hukaa pale juma moja wakisubiri kila mmoja aende dirishani kupokea mshahara, kama fedha imechelewa kuletwa yeye hubaki pale siku nyingi. Kutokana na kuchelewa huko Shule huwa zinakosa Walimu na wengine huja na fedha kidogo kwa hiyo, huwabidi waishi kwa kukopa na wengine kujiingiza kwenye matatizo ambayo husababisha wafe kabla ya wakati wao. Hii ndiyo hali ya Mwalimu ninaowazungumzia hapa. Hivi Ndugu zangu, mtumishi gani katika nchi hii anafanya kazi kama Mwalimu? Najua kuna kazi kama ya Waganga ni *delicate,* sawa, lakini nani anafanya kazi kama Mwalimu na nani kati yetu hapa atalalamika kama tutaongeza mshahara wa Mwalimu? Yuko wapi? Asimame! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia Jeshi kubwa la Watumishi ambao hawapigi kelele, a silent army. Jeshi hilo liko kila mahali, kila Kijiji, lakini linaishi maisha ya ajabu sana! Baadhi ya nyumba za Walimu ni kama mazizi au mabanda ya kufugia kuku au nguruwe. Hapo ndipo anaishi mtu anayelea watoto wako. Napendekeza tuamue kama Taifa, kwamba kwa miaka miwili tuhakikishe Walimu wote wanakaa kwenye nyumba zinazofanana na hadhi ya kazi wanayofanya. Hivi tunaweza nini? Ni

suala la matofali, mawe, mchanga na mabati na vyote hivi vipo. Tukitaka tunaweza na ninapendekeza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye akili huweka akiba yao katika elimu. Ninafurahi kwamba Serikali yetu imeamua kuwekeza katika elimu na hatua zinaonekana. Vile vile, napenda niwapongeze wale watu binafsi ambao wanatumia fedha zao kidogo kujenga Shule, lakini naomba Wizara ya Elimu na Utamaduni isimamie Shule hizo ili kuwalinda watoto na wazazi ili wapate kitu wanachotegemea, maana hawajui elimu bora ni kitu gani, kwa hiyo, wanapeleka tu watoto wao!

Maadam Shule imeandikwa Shule kwenye jengo basi wanadhani ni Shule! Elimu bora haiwezi kupatikana kwa njia ya *osmosis* au kwa mpenyezo tu, kwamba watu wamekaa kwenye majengo ya Shule, basi elimu inapatikana tu. Mahali pengine utapeli na ulanguzi unaendeshwa kwa lengo la kupata fedha. Wengi wanafanya kazi nzuri, lakini Wizara itusaidie kukagua Shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kuna mabadiliko mengi na makubwa, ni kweli, lakini ni lazima tuangalie kwamba katika *mass production, mass recruitment of pupils and teachers* tunaweza tuka-*sacrifice quality* na hili naona ni gumu zaidi na huenda ndiyo maana kuna wakati Mheshimiwa Waziri amethubutu kuwafanya Walimu wa *Primary Schools* wafanye mtihani wa darasa la saba, eti kwa lengo la kutaka kujua uwezo wao, nadhani pale alikosea, siyo mahali pake, anataka kupima nini? Maarifa, *IQ* au kitu gani! Maana hata mimi naweza nika-*fail* ule mtihani! Nadhani pale Waziri anaweza kuzua *humiliation,* kwa sababu kama yule Mwalimu atafanya mtihani wa darasa la saba aka-*fail* na akabaki pale na mtoto aliyemshinda yule Mwalimu yuko pale, kidogo haileti picha nzuri, kuna njia nzuri za kufanikisha lengo lile lile. Natumaini hilo tumejifunza na halitarudiwa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili wazo ambalo nalipongeza, Mheshimiwa Waziri ameonyesha kwenye hotuba, kwamba anataka kupunguza ugani wa Mwalimu na mwanafunzi kutoka Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 iwe ni Mwalimu mmoja mwa wanafunzi 40, ni sawa, lakini bado hili halijibu tatizo za Shule zenye wanafunzi wachache, lakini zina madarasa yote saba. Unaweza kuwa na wanafunzi 90, lakini ni wa madarasa yote kutoka darasa la kwanza mpaka la saba, darasa lingine wanafunzi 10, lingine 15, lakini jumla yote wako 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa *ratio* hii utasema wanafunzi 90 kugawa kwa 45 utapata walimu wawili katika Shule yenye madarasa 7. Kwa hiyo, nasema ni vizuri masuala kama hayo tuyaangalie, kwa sababu wakati mwingine wanafunzi hao wapo kwenye Kijiji ambacho kimeandishwa. Kama ni hivyo basi, wakae na Wizara nyingine ili Vijiji viungane na kuwa Kijiji kimoja kikubwa chenye wanafunzi wengi, kuliko kuwa na Kijiji *registered* na kina Shule, lakini Shule haina watoto wengi na ina tatizo la kimsingi ambalo linaathiri watoto na hasa Wilaya zenye jiografia ngumu, milima na mabonde. Wakati mwingine mambo hayo ni magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo lingine ambalo napenda nilitoe hapa kwa haraka ni suala la kuimarisha Ofisi ya Afisa Elimu wa Mkoa na wa Wilaya.

Tumewaongezea majukumu maofisa hawa wakati tumewapunguzia wasaidizi na madaraka. Elimu ya Sekondari mpaka sasa kwa nadharia inasimamiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Sekondari kutoka Makao Makuu ya Wizara ambaye hawezi kwa nchi kubwa kama hii kusimamia elimu hiyo, kwani Shule zinaota kama uyoga!

Kwa hiyo, inabidi *REO* achukue jukumu hilo la kusimamia Elimu ya Sekondari Mikoani, wakati hana watumishi wa kutosha! Napendekeza waongezewe madaraka na jina *REO* libaki na liwe na maana, siyo *REO* kuwa sehemu ya *secretariat* ya Mkoa. Wachina wakati fulani walifuta vyeo vya Makamanda majeshi yao ikawa hata Mkuu wa Makamanda anaitwa Askari tu! *(Makofi)*

Tuwe na Afisa Elimu wa Wilaya anayesimamia elimu, siyo sekretarieti yaani kuwe na mtu bingwa wa elimu ambaye atasimamia elimu. Napendekeza kwamba tuongeze watalaam wa elimu ya *primary* chini ya *REO* yaani upande wa *Primary, Secondary*, Walimu na ufundi kama ilivyo Kenya kusudi tuweze kusimamia vizuri elimu katika ngazi zote katika Mkoa. Haiwezekani kwa nchi kubwa kama Tanzania tukasimamia elimu kutoka Dar es Salaam. *REO* aongezewe madaraka na taaluma yake na uwezo hata kama atakuwa na sifa kupita Katibu Mkuu au Mkurugenzi. Sioni sababu nchi ni kubwa. Lengo ni kukidhi nia yetu ya kutaka kuimarisha elimu katika nchi yetu. Kwa sasa hali ilivyo haiwezekani, Dar es Salaam ni mbali na *REO* hana watu. Kwa hiyo napendekeza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ngazi ya Wilaya vile vile *DEO* sifa zake tuongeze. Tuunde bodi lakini vile vile tuwaongezee uwezo wa kitaaluma ili waweze kusimamia elimu katika ngazi zote, kama waganga wanavyofanya chini ya Wizara ya Afya.

Napendekeza kwamba Wizara haiwezi kuendelea na mtindo wa sasa wa kuruhusu shule zinajengwa kila mahali. Shule za sekondari zinaota kama uyoga, wakati kuna matatizo ya kimsingi ambayo ni magumu na lazima yatatuliwe. Naelewa tatizo la Wizara Mheshimiwa Waziri aliwahi kuleta pendekezo kwamba popote palipo na shule tano za sekondari tusimame, wakati kuna mahali amepokea shule 34! Njia nzuri ilikuwa kwamba yule aliye na shule 34 asiendelee kufungua nyingine. Kwa hao wengine waendelee na ujenzi wa shule za sekondari mpaka wakamfikie yule. Huo ndiyo mkakati wa busara. Sasa kwa sababu wakati ule tulikataa sasa tumeacha mambo hivi hivi. Kila mahali shule zinajengwa bila kuwa na utaratibu. Tusipoangalia tutakuja kuwa na *extended primary schools*. Tutapunguza hadhi na ubora wa elimu kiasi kwamba baadaye itakuja kuwa *counter productive.* Tutaua elimu ya Sekondari. *(Makofi)*

Napendekeza kwamba Wizara isimamie na kuratibu hizo shughuli, kama maji kwenye shamba. Ruhusu pale wajenge shule wakati ukihakikisha kwamba una walimu na vifaa vya kutosha. Wale wengine waendelee kujenga shule zao kwa nguvu zao. Lakini kwa wengine waendelee mpaka watakapofika pale walipofikia, lakini kwa uratibu na usimamizi chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo lingine katika hili, ili kuimarisha elimu lazima tuangalie upya Vyuo vya Ualimu. Kwa sasa ubora wa Wakufunzi katika Vyuo vya Ualimu kwa kweli hauendi na wakati. Wakufunzi waimarishwe kwa maana ya ubingwa wa kitaaluma, uzoefu na tuweke mabingwa wa masomo muhimu ya *primary schools* wafundishe ili mwalimu akienda vyuoni wafundishwe njia za kufundisha pamoja na masomo yote muhimu ya msingi. *(Makofi)*

Bila hivyo atakuwa anajua kufundisha lakini, hana ujuzi wa masomo ya kufundisha. Ndiyo hali ilivyo hivi sasa. Mwalimu anahesabiwa ni mwalimu wakati hajui *Geography, Physics,* Hisabati anajua *methods* za kufundisha tu, sasa anafundisha nini? Ni vizuri tuviimarishe vyuo hivi kwa vifaa kama ilivyoonyesha katika kitabu cha Wizara. Tupeleke mabingwa wa masomo wakafundishe katika vyuo. Walimu watakapotoka pale watakuwa wameongezwa kiwango cha taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo lingine linahusu Kitabu cha Waziri cha Takwimu ukurasa 16. Pale ameonyesha jinsi wanavyotoa alama kwa wanafunzi wa darasa la saba wanapomaliza mtihani wa darasa la saba. Wanaweka alama ya A, B mpaka C wana maana yake. Kwa kufuatana na uchambuzi wa matokeo ya mitihani kwamba hivi sasa ni asilimia 27 tu wanafunzi wanaofanya mtihani wa darasa ndiyo wanaofaulu. Maana kwamba asilimia 73 huwa wamefeli.

Mimi nimekuwa nikiuliza maswali mara kwa mara hapa Bungeni na nimekuwa nikijibiwa visivyo na bado nauliza tena wale wanaopata chini ya alama ya C maana yake hawana elimu ya msingi? Mimi nilikuwa nadadisi kwa nini? Mtihani huu ambao unatumika kuwapima wanafunzi wa kwenda *secondary school* unaotumika vile vile kupima watu waliomaliza elimu ya msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kipimo hiki siyo sahihi. Ni lazima kibuniwe kipimo kingine cha kupima mafanikio katika elimu ya msingi. Tuko tayari kusaidiana mawazo. Lakini vile vile napendekeza kwamba kama alama ya A ni kutoka 121 mpaka 150 na B ni alama 91 mpaka 120 na C alama 95 mpaka 90, kwa nini tusiongeze alama D iwe ni alama 50 mpaka alama 64, ukiweka pale halafu kufeli iwe kutoka alama 49 mpaka 0.

Tupandishe kundi la kufaulu maana huyu anajua kusoma na kuandika lakini hawezi kwenda sekondari. Lakini kama elimu ya msingi ya miaka saba maana yake ni kwamba kwa matatizo ya sasa hivi yakutokuwa na walimu na vifaa. Watoto hawapati dozi kamili ya darasa la kwanza, darasa la pili na kuendeleza mpaka darasa la saba. Kwa hiyo, mtoto anamaliza elimu ya msingi akiwa hana elimu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba tutazame upya suala hili, sijui kama lile wazo la *National Education Advisory Board* kama lilifutwa? Mawazo yale yaliyotolewa na Kamati ya Bunge, kwa kweli yangechambuliwa kwa kina na Bodi kama hiyo, kama ingeundwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ni watumishi wanaofanya kazi ya kulea Taifa hili. Ubora wa viongozi na raia wa kesho wa nchi hii utategemea elimu inayotolewa hivi sasa. Tukiparaganya mambo sasa basi ndiyo tumeparaganya misingi ya maisha ya baadaye ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikikumbuka kazi ngumu inayofanywa na walimu wa nchi hii, chini ya mazingira magumu wanayoisha walimu katika nchi hii, machozi huwa yananilengalenga. Kuna wakati nikiwa Waziri, nilikwenda Mkoa wa Manyara, wakati nikielekea kwenye hoteli, mwalimu mmoja alikuwa anaishi kwenye nyumba iliyo kama ghala la mahindi hivi (kihenge), alipoona gari linakuja akakimbia akidhani sisi ni majasusi kumbe nilikuwa Waziri wake. Basi nilisogea pale nikamwambia mwalimu asiwe na mashaka na sisi. Wakati nikiangalia ile nyumba aliyokuwa anaishi, mara mjusi alitoka pale na kwenda nje. Pale ndipo anapoishi mwalimu wetu!

Vile vile wakati wa kampeni nilikwenda kwenye vijiji fulani vya mbali na kulazwa katika nyumba ya Mwalimu Mkuu. Usiku panya alikuja kunishambulia na ikabidi nitoke mbio (Mgombea wa Ubunge) ndani ya nyumba ile. Hizi ndizo nyumba za walimu wanaolea watoto wetu. Mimi nadhani kuwa kipimo cha Taifa lolote linaloendelea ni ubora wa mahali wanapolelea na kuelimishia watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Taifa lolote linalopuuzia mahitaji muhimu ya watu wake hasa walimu, litashindwa kukidhi mahitaji ya nchi yake. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara ya Elimu na Utamaduni. Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake ya ufasaha kabisa katika hoja yake na sina sababu ya kuitakataa hoja hii, mimi naiunga mkono hoja hii moja kwa moja. Pia namshukuru sana na kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni ndugu yangu, Bujiku Sakila, kwa uhodari wake katika kazi pamoja na kwamba hatupo naye hapa, lakini tunamtakia kila la kheri, apone haraka ili aungane na wenzie waweze kuendelea kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nijadili matatizo zaidi kwa sababu mafanikio ni mengi siwezi kuyataja. Sasa haya matatizo yanaweza yakamsaidia Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake kurekebisha mambo ili yawe mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo la kwanza ni mishahara ya walimu dhidi ya gharama wanazotumia. Kwa walimu wote wa shule za msingi na wale wa shule za sekondari. Nataka kutoa mfano mfupi kwamba mshahara wa mwalimu labda tuchukulie ni shilingi 85,000/=. Sasa anza kutoa, katika kutoa anza kutoa kodi za kisheria mbalimbali, lakini pia kuna makato mbalimbali ya kisheria unayaondoa, pia lazima utoe gharama za mwalimu kufuata mshahara Wilayani na hawezi kukaa siku moja ni siku mbili, tatu, nne, ondoa hizo gharama, malazi, chakula nakadhalika. Sasa sana sana pale

mshahara wa mwalimu ni shilingi 35,000/= ndiyo anaopata mkononi na kurudi nao kijijini.

Kwa hiyo, lazima Serikali iwe macho iangalie hilo. Ndiyo maana hata hotuba ya Waziri Mkuu, nilisema hawa walimu wanastahili malipo ya kufanya kazi katika mazingira magumu. Kwa hiyo ni sehemu ya mazingira magumu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Serikali ijue utaratibu wa kuwatambua walimu ili ipandishe mishahara yao. Kwa sababu kazi ni ngumu na ni muhimu sana hawa walimu walipwe ili waweze kutoa elimu bora kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ambalo pia ni kubwa ni uchache wa nafasi za sekondari. Nilikuwa najaribu kuangalia hotuba yako, vijana waliokuwa darasa la saba, acha waliofanya mtihani, mwaka 2002 waliopata nafasi ya kwenda sekondari ni asilimia 22 tu na asilimia 78 wote wamerudi vijijini. Kwa hiyo, hali ni ngumu. Elimu ya msingi huko baadaye tunakokwenda itakuwa ni ya sekondari. Kwa hiyo, Serikali iwezeshe wananchi kujenga shule za sekondari za kutosha ili vijana wetu wengi waweze kuwa na elimu ya sekondari.

Nimefurahi kuona ile mipango uliyosema, lakini uharakishwe! Mimi nilifikiri kwamba utatolewa maelezo hapa, tukiondoka hapa ni kwenda kuchangamkia kazi, lakini wanasema tena bado unafanyiwa utafiti na kadhalika, labda tena mpaka mwakani. Tunazidi kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufanikiwa vile vile kama tunavyojua wananchi bado ni maskini sana. Hii ada ya shule za sekondari tuiondoe. Tuna vijana wengi sana wanashindwa kusoma elimu ya sekondari kwa sababu wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia ada. Sisi hapa ndiyo tunajitahidi kuwalipia watoto ada za shule nakadhalika, lakini wananchi wengine wote wanashindwa. Kwa hiyo, tunaomba hii ada iondolewe. Lakini vile vile wako wanafunzi wasichana katika shule za sekondari na za msingi wanaopata mimba wakiwa shuleni, imeelezwa humu kwenye hotuba. Mimi nataka nisome kitabu ambacho ni mwongozo nafikiri karibu Wizara zote wanacho kinaitwa Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Kuondoa Umaskini. Sasa sehemu ya elimu ukurasa 37, kipengele cha 5 kinasema wanafunzi wa kike wa shule za msingi na sekondari, wanaopata ujauzito wataruhusiwa kuendelea na masomo na kupata elimu ya malezi ya familia. Sasa kwa nini tunachelewa? Mwongozo huu umeshaelekeza kwa hiyo ni sera zetu. Kwa hiyo, tunataka nani aje afanye? Kwa nini tunachelewachelewa ni haki yao wasome hawa! Ni bahati mbaya tu wakapata mimba!. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tatu, ni ukosefu wa shule za ufundi stadi huko vijijini na mitaani. Shule za ufundi kwenye vituo vile vya ufundi stadi ni muhimu sana. Mimi nilifikiri katika Bajeti hii tungehimiza kwamba angalau kila kata basi iwe na kituo cha namna hiyo. Nadharia peke yake haitasaidia kuondoa umaskini haraka, lakini shule za ufundi zitachangia ajira, zitachangia kuondoa umaskini nchini.

Kwa hiyo, tunaomba hili suala lisiachwe maana limeanza kuachwa, hatutaki kuzungumza, tunazungumza kwa kifupi. Tunaomba sana katika hili lifuatiliwe. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kuikumbusha Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile katika kitabu hiki ukurasa wa 37, kifungu cha 4 kuna kipengele kinazungumzia habari ya sayansi na teknolojia, anasema: “Sayansi na Teknolojia zitapewa kipaumbele katika taasisi na vyuo vya mafunzo.” Kwa hiyo, lazima tubadili mwelekeo wetu tuutoe katika sayansi na ufundi na teknolojia ili tuweze kuharakisha maendeleo yetu kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nne ni kwamba shule za msingi na sekondari hazikaguliwi vizuri. Ni kweli tumepiga hatua lakini hazikaguliwi kwa sababu zifuatazo. Kwanza ukosefu wa magari. Ziko Wilaya hazina magari kabisa ya kukagulia, Wabunge ndiyo wanaosaidia kutoa magari, Halmashauri zinasaidia, lakini siku ambayo Halmashauri hawana gari, Wabunge hawana, basi wakaguzi hawaendi kukagua shule.

Kwa hiyo, Wizara inunue magari kwa ajili ya ukaguzi kwa kila Wilaya. Tena magari haya *Samarai* hayafai, *Land cruiser* ndiyo zinawafaa wakaguzi wengi ili waende wakakague shule. Kazi hii tunaiweza, kama tumepiga hatua hiyo, tunaweza kabisa kufanya hii. Shule haziwezi kuendelea bila kuwa na wakaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tano, nataka kuzungumzia Chuo cha Ualimu Kondoa. Chuo cha Ualimu Kondoa kina matatizo na kwa bahati nzuri nimefika Wizarani nimezungumza na Katibu Mkuu na ametoa ahadi atasaidia. Lakini lazima nibainishe niweke katika kumbukumbu. Matatizo hayo ni kama haya yafuatayo, Chuo kile walikuwa wanakarabati lakini hakijamaliziwa. Tunaomba fedha zitolewa tena ili kimaliziwe kukaratiwa.

Lakini pia uchache wa mabweni, wanachuo ni wengi, wanabanana sana katika bweni moja ambayo kiafya ni mbaya kabisa. Kwa hiyo, tunaomba tupewa hela, tujenge angalau bweni lingine ili wanachuo waliopo pale waweze kulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanachuo zaidi ya 300. Vile vile maktaba na maabara hakuna vitu ambavyo ni muhimu sana kwa wanafunzi wetu kwa sababu hata walimu wanaochukua mafunzo pale wanakwenda kimichepuo. Wapo wa mchepua wa sayansi, wapo wa mchupuo wa maarifa na nakadhalika. Kwa hiyo, tunaomba sana katika hili. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini tatizo lingine ni kwamba wana mashine ndogo ya kusukuma maji, lakini nayo sasa hivi imezidiwa kwa sababu ilikuwa inaweza kusukuma maji kwa wanafunzi wasiozidi 50, sasa hivi wapo zaidi ya 300 kwa hiyo, ile mashine imechoka inashindwa kupeleka maji kwenye chuo. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ifike iangalie. Namwomba Katibu Mkuu asiende Dar es Salaam kwanza, aende Kondoa aone namna gani atashirikiana na chuo kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

Vile vile wana magari mawili makuu kuu ya siku nyingi hayafanyi kazi tunaomba wapewe gari mpya katika utaratibu kwani nimeona hela ni nyingi tu chuo kinaweza kikapata gari mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine naomba niunganishe na Sekondari ya Wasichana Kondoa. Maana pamoja na kuzungumzia ya Kitaifa, vile vile nizungumzie na yale yanayogusa katika jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwilaya tulijitahidi sana. Wanafunzi wa Kondoa vile vile wana matatizo ya maji. Kiwilaya tulijitahidi sana kununua machine ndogo mpya kupitia *BSF machine* ile imesaidia lakini ndogo na shule ina wanafunzi wasiyopungua 500 kwa hiyo, nayo sasa imefeli kufanya kazi. Wanafunzi hao ni wasichana na kama unavyojua matatizo ya wasichana ni mengi zaidi kuliko ya wavulana.

Kwa hiyo, tunaomba Katibu Mkuu, atakapokwenda kule kwenye Chuo cha Ualimu, basi afike vile vile kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa ili aone tatizo hili la maji atalitatua namna gani. Ni muhimu sana. Sasa hivi ile shule imeanza kuwa na wanafunzi watoro kwa sababu ya ukosefu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie walimu wanafunzi wanaokaa mwaka mmoja katika chuo na mwaka mwingine wanakuja kumalizia kwenye mazoezi kwa maana shuleni. Nasikia wanalipwa asilimia 80 kwa hiyo, hawalipwi mshahara kamili.

Sasa mimi nasema tukifanya hivyo hatutaboresha elimu hata kidogo. Kwani kuna sababu gani ya kuwanyima kuwalipa mshahara mzima unaotakiwa? Walipwe mshahara mzima uliopangwa ndiyo tutawapima vizuri wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea kuwalipa sehemu ya mshahara watakuwa watembezi, wakimbizi wa kwenda kuhemea hemea, hawatatulia kufanya kazi shuleni. Tuwape mishahara, tuwapime vizuri, watakaoshindwa basi watajiondoa wenyewe. Lakini kwa utaratibu huu tutakwama. Waalimu wameshaajiriwa tangu mwezi wa sita, lakini wengi wanashindwa kuripoti kwa sababu wanajua hilo tatizo.

Kwa hiyo, naomba sana hilo lizingatiwa na Serikali na Waziri alione vizuri na wahusika wote walione vizuri ili tuweze kusaidia kuimarisha elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa hayo niliyosema, lakini naunga mkono hoja hii, naomba yale yote niliyosema hapa yazingatiwe na Katibu Mkuu aende Kondoa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuishie hapo kwa asubuhi. Isipokuwa ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja, kufuatana na Kanuni ya 49 (a) unayo saa nzima ya kujibu hoja hii katika kumalizia.

Mheshimiwa Waziri, kama utaitumia mwenyewe ni saa moja, kama utapenda kugawana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, naona na yeye amekaa

karibu, kama ungependa msaidiane kujibu hoja, basi mtagawana hiyo saa moja. Kwa hiyo, mjiandae kwa namna hiyo.

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6. 46 Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa wasaa wa kuweza kuchangia na nikiwa wa kwanza mchana huu. Kabla sijaanza kama ilivyo ada ningependa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliotuunga humu ndani baada ya kupata ushindi katika chaguzi ndogo za mwezi wa tano, wakaribie sana, lengo liwe ni moja la kujaribu kuishauri Serikali ili kuleta maendeleo kwa wananchi wetu kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wa Wizara na Wataalam wote kwa kazi nzuri kwa kweli wanayojaribu kuifanya, tuwaunge mkono na hatimaye kutayarisha hotuba ambayo wameitoa leo, yenye mwelekeo wa matumaini ya kuweza kutekelezeka katika Sekta ya Elimu kwa ngazi ya Msingi, Sekondari, Walimu na Elimu ya Watu Wazima. Kwa kweli hongera sana.

Pia nimefarijika kusikia kwamba Mheshimiwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, amerudi India. Hivyo ni mategemeo kwamba hali yake ni mzuri na huenda anaweza akaungana nasi labda katika kipindi hiki cha *Session* hii, Mungu amsaidie kupona haraka.

Baada ya utangulizi huo Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mchango wangu kwa ushauri. Lakini sehemu kubwa kwa masikitiko kwa sababu ushauri huu nimejaribu kuutoa tangu nilipoingia ndani ya Bunge hili mwaka 2000 hata 2001 si ndiyo Bajeti ilianza hapo. Lakini nasikitika utekelezaji wake mambo mengi bado kidogo yanasua sua. Ni hongera kwa Taifa kuanzisha au kufufua elimu ya *UPE* kwamba wote waweze kwenda shuleni na elimu ya msingi ndiyo msingi wa mengine yote. Huwezi ukaenda Chuo Kikuu bila msingi. Lakini inasikitisha kwamba watoto wenye ulemavu hasa viziwi, wasioona na watoto walemavu wa akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu hii tusipoiangalia wao hawatafaidika nayo. Kwa sababu pamoja na kufutwa ada, kwa elimu ya msingi, lakini bado kuna matatizo mengi, yanayowasibu watoto hawa kama ambavyo nitajaribu kurudia. Kwa kweli ninarudia na sijui nitumie mbinu ya kulia kama ambavyo Wabunge wengine walilia, basi wakatimiziwa.

Sasa sifahamu, lakini machozi ya haraka hivyo sina, ila kwa kweli ni kwamba nasikitika kwa sababu ninapozungumzia jambo miaka miwili mitatu, halafu matokeo yake ukaona kama vile hayapo. Inatia uchungu kidogo.

Ninalolirudia ni kwamba katika shule zilizotengwa au za mjumuisho maalum kwa watoto wenye ulemavu, hasa kwa wasioona, wale wenye ulemavu wa akili na viziwi, bado kuna tatizo la ukosefu wa walimu wa taaluma hii ya elimu maalum ambayo hao wanafundishwa jinsi ya kusaidia watoto hao. Kwa sababu si tu kufundisha darasani, lakini walimu hawa wanapaswa kuwasaidia watoto hawa kutokana na matatizo yao kwa njia moja au nyingine.

Kwa mfano, nilipokuwa ziarani hivi karibuni katika Mkoa wa Lindi, nilipata malalamiko katika shule maalum ya Nachingwea Mjini ambapo ni ya watoto wenye ulemavu wa akili, kuna mwalimu mmoja tu, anayehangaika na watoto 10. Yeye akaniambia Mheshimiwa Mbunge mimi ni moyo tu, vinginevyo ningekuwa na mapafu, kazi hii ningeiacha. Nikamsihi tu kwamba aendelee kuwa na moyo kwa sababu hawa nao wanapaswa kusaidiwa.

Kingine ni ukosefu wa vifaa. Nimeona humu katika Kitengo cha Elimu Maalum, kuna vifaa vitanunuliwa vya kufundishia labda tegemeo hilo hapo, lakini kwa watoto wasioona wanahitaji *tape recorder.* Mwalimu anapozungumza, anarekodiwa, yakishazungumzwa anahitaji *Braille Machine* kuyahamisha yale aliyoyasikia katika lugha yao ile ya madoti doti. Yale madoni doni na ile mashine inahitaji karatasi maalum kusudi mtoto huyo aweze kumudu hayo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kabisa mahitaji haya hayapo. Hayapo katika shule za msingi. Nimeona Masasi Maalum Mtandi, ambapo kuna walemavu wasioona. Nimepata taarifa kutoka Korogwe Sekondari, nimepata taarifa kutoka Ndanda Sekondari ambayo kuna Kitengo cha Walemavu wasioona hapo. Hizi ni Shule chache tu, lakini kwa ujumla wao suala hili huu ni mwaka wa tatu hakuna ambacho kinaendelea.

Tatizo lingine ni ukosefu wa vitabu vya maandishi makubwa. Ulemavu unapishana, Albino hawawezi kusoma maandishi madogo madogo, sijui kama hili linatiliwa maanani wakaweza kuandaliwa watoto hawa kuweza kumudu kwa sababu huwa hawaoni kutokana na mwanga. Kwa hiyo, maandishi yao ni makubwa makubwa.

Lingine, ni matumizi madogo kama sio hakuna ya lugha ya alama kwa watoto viziwi mashuleni. Nasikitika kusema kwamba wakati ninapotembelea watu wenye ulemavu, viziwi wanalalamika kwamba walimu hata kama wanafundisha, hawatumii lugha ya alama mashuleni. Kwa hiyo, watoto hawa huwa hawaelewi na wengine wanachanganywa na watoto wazima darasani. Sasa hebu niambie, huyu asiyesikia inakuwaje? Inakuwa baada ya darasa ampate mwanafunzi mwenzake kuweza kumweleza sijui kwa kuandika, sijui kwa lugha ambayo hata na mwanafunzi mwenzake haielewi ili aweze kumudu na kiziwi wanajiweza sana kwa masomo ya sayansi hasa yale ya vitendo. Lakini bila kuwasaidia kwa lugha hii inakuwa ngumu kuweza kufahamu.

Tatizo lingine ni ukosefu wa shule zenyewe hasa zile zinazoitwa maalum. Sasa hivi kuna *move* ya kuwa na elimu ya majumuisho. Sina uhakika kama elimu hii au mtindo huo wa kusomesha umeeleweka vipi kwa walimu na jamii kwa ujumla wake. Hata hivyo, zamani kulikuwa na shule maalum zilizotengwa kwa ajili ya watoto hawa.

Lakini nazo kwa upande wa Serikali ni chache, nyingi ziko chini ya Mashirika ya Dini na nyingi si rahisi kufikiwa na watoto wa aina ya ulemavu kwa mfano wasioona au viziwi. Mtoto atoke Mahenge aje asome Buguruni Shule ya Msingi. Kusafiri kutoka Mahenge mpaka Buguruni ni tatizo. Haya niliyaona na iliripotiwa wakati wa ziara zangu. Hilo ni tatizo kwa watoto wengi kuweza kumudu hii elimu ambayo ni lazima nao waipate kama watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwamba katika kujibu swali Mheshimiwa Waziri katika Mkutano wa kumi nililoliuliza kuhusu mazingira ya majengo na hata Kamati limezungumzia hilo kwamba basi ataangalia jinsi ya kujaribu kuzingatia mazingira mazuri au yanayofaa kwa majengo ya madarasa na vyoo ili hawa watoto katika awamu ya pili ya MMEM hayo yaweze kuzingatiwa, yaweze kuboreshwa. Kwa hiyo, ninasubiria kwa sababu moja ya tatizo ni *accessability* kwa watoto wenye ulemavu hasa wa viungo kwani wanapata taabu kama mimi wakati mwingine mnavyoshuhudia hapa ninavyohangaika na hizi ngazi. Lakini huna la kufanya kwa sababu mazingira ndivyo yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ningependa kuzungumzia kidogo kuhusu ajira ya walimu. Ni kweli Wizara ya Utumishi imetoa ruhusa ya ajira za Walimu na Walimu wengi kiasi wameajiriwa na wataendelea kuajiriwa. Lakini kuna kilichotokea kidogo ambacho nadhani wananchi wamekishangaa. Sasa sifahamu ni kuanzia wapi. Lakini kwa sababu ndiyo Wizara yenyewe kwamba Walimu waliomaliza shule au Vyuo walishapewa ruhusa ya kuajiriwa, waliajiriwa. Lakini baada ya muda mfupi zikaja taarifa au barua kwamba wale walioajiriwa ambao walikuwa tayari wamehitimu wasitishwe kidogo ili wachukuliwe hawa walimu wanafunzi, sijui ndiyo watarajali hawa wanaoitwa.

Sasa wananchi wanashangaa, itakuwaje wale waliohitimu wawekwe pembeni kidogo ili nafasi zao ziweze kujazwa na hawa wageni au hawa wapya au ambao wapo kwenye mafunzo. Mafunzo ambayo wengine tunayashangaa kwa sababu mwaka mmoja wa shule halafu wa pili wakafanyie mazoezi nje bila hata mwalimu wa kuwa-*access* kwenye *teaching practice* nayo vile vile inawashangaza wananchi na kwa kweli walikuwa wamesita au wameshangaa kwamba kwa nini walimu hao ambao hawajamaliza shule waweze kurudishwa chuoni. Hili pia nililikuta kwenye ziara zilizozifanya huko Kusini. Kwa hiyo,ufafanuzi zaidi uweze kutolewa.

Naipongeza Wizara kwa kuongeza fedha za kuweza kusomesha watoto wa kike wanaotoka kwenye matatizo au familia zenye matatizo. Lakini kama wenzangu walivyosema na wavulana pia wana matatizo. Kwa hiyo, hebu tujaribu kuangalia kurekebisha tatizo hilo.

Naipongeza Wizara kwa upande wa utamaduni kwamba mwaka 2002 nilizungumza humu ndani kuhusu tamasha la Bagamoyo. Nashukuru kwamba Wizara ilishirikisha watu wenye ulemavu na kweli walionyesha vipaji vyao kule. Ninaloliomba kwa sababu matamasha haya yanafanyika kila mwaka kwa upande wa Bagamoyo, nasema waendelee kushirikishwa, kuwe na utaratibu maalum wa kutafuta walemavu

wenye vipaji mbalimbali, sanaa na utamaduni, waweze kuendelezwa pale chuoni Bagamoyo.

Huko nyuma tulikuwa na Marehemu Mzee Morice Nyunyusa, alililetea Taifa hili sifa nzuri tu, alikwenda Japan. Kwa hiyo, hawa pia waweze kuendelezwa angalau wajisikie vizuri na wanaweza wakapata kipato kutokana na taaluma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya walimu, kama wengine walivyosema, kwa kweli yaangaliwe. Kwa sababu sasa hivi ni karne ya ajira ya soko huru. Walimu wanaweza wakashirikishwa, wakaenda kwenye shule za *private* ambako zinalipa vizuri. Halafu shule za Serikali zitaendelea kudoda pamoja na jitihada zote za kuongeza idadi lakini bila walimu hatuwezi kufika mahali popote. Walimu wana kazi nzito, wanapaswa kuangaliwa.

Kuhusu suala la kuinua hadhi ya walimu. *TSC* miaka ya nyuma ilianzisha mfuko wa kusaidia Walimu kununua magari. Walimu walipaswa kuchangia. Lakini mradi huu ulikufa kifo cha panzi hata sielewi. Sasa ikabidi walimu warudishiwe fedha zao. Walimu wa shule za sekondari wengi wao walirudishiwa zile fedha lakini wa shule za msingi mpaka leo wengi wao hawajarudishiwa, wanaloomba wanataka kujua hatima ya fedha zao na ikiwezekana fedha hizi zirejeshwe haraka iwezekanavyo. Sina hakika kama Bajeti imepanga au haijapanga. Lakini ni vema warudishiwe.

Baada ya kusema haya, kama nilivyosema, nimeyachangia haya kwa kurudia mara ya tano kama siyo ya sita. Mimi ninachokiomba ni utekelezaji kutokana na Bajeti hii hasa kuhusu watoto walemavu waweze kuelimika. Jamani bila elimu, hawa watakuwa omba omba milele na hali zao ni mbaya. Kwa kweli mnajua, mnawaona. Ahsante kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Elimu. Kwanza kabisa naomba niseme naunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu na Utamaduni. *(Makofi)*

Pili, naomba nichukue nafasi hii kutoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na tunashukuru kwamba Waziri amesema kwamba anaendelea vizuri na tunamwombea aweze kupona ili akaendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara hii chini ya usimamizi wa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wake wote na wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia elimu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unaanzia katika ukurasa wa 60. Naomba ninukuu, ambapo anasema kwamba: "Kufutwa kwa ada na michango ya wazazi peke yao katika shule za msingi," na akasema: "Nachukua fursa hii kusisitiza kwa mara

nyingine kuwa Serikali inakataza kabisa kuwachangisha wazazi wa wanafunzi wa shule za msingi peke yao kwa sababu yoyote.”

Sasa, tukiangalia yale maneno ambayo yamewekwa kwa msisitizo, ni kuwachangisha wazazi wa wanafunzi peke yao, kwa maana ya kwamba michango hii ipo na kwa maana hiyo, wale wanaotakiwa kuchangia pale kama Shule inahitaji mchango ni wananchi wanaoizunguka ile shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango huu uko hapo kwa maana ya kwamba hili agizo kwa kweli limekuwa halitekelezeki au ni gumu kutekeleza kwa sababu si rahisi sana kwa Mwalimu Mkuu kuweza kuitisha wananchi wanaoizunguka ile shule ili kuweza kupata mchango kwa ajili ya maendeleo ya shule ile. Nasema hivyo, kwa sababu inawezekana kabisa wazazi au wananchi wanaozunguka maeneo yale wengine hawana watoto wanaosoma katika shule ile. Kwa hiyo, si rahisi sana kukubali yeye aweze kuchangia katika ujenzi au matengenezo ya shule au inawezekana mwananchi mwingine watoto wake wako nje ya shule ile na kwa maana kule anakosomesha watoto wake nako wanahitaji mchango wa aina fulani au pengine anasomesha *International School* kama *International School* ina maana mchango wa kule ni mkubwa sana.

Kwa hivi inakuwa siyo rahisi sana kuweza mwananchi yule kuweza kuchangia katika shule ile ambayo anakaa karibu nayo. Kwa hivi ndiyo maana unakuta kwamba Mwalimu Mkuu anachoishia ni kwenda kumtuma mwanafunzi ili akamwite mzazi, kwa sababu huyu mzazi yeye, mwalimu anajua kabisa kwamba mzazi wa mwanafunzi aliyenaye ndiye aliye na uwezo wa kuweza kumwita ili kumwomba msaada kwa ajili ya matengenezo au kwa ajili ya kitu chochote ambacho shule imekuwa ikihitaji.

Kwa hiyo, nadhani kwamba hili agizo halitekelezeki na sisi wanasiasa kwa kweli tusingependa kugombana na wananchi tuwaambie kwamba mnatakiwa kuchangia, wakati tayari Serikali inasema kwamba hakuna kuchangia. Kwa hiyo, inakuwa si rahisi sana kuweza kushawishi wale wananchi wanaozunguka katika yale maeneo ya shule ili waweze kuchangia katika ujenzi wa shule.

Kwa hiyo, mimi hapa nilikuwa nadhani kwamba Serikali ichukue tahadhari nyingine au ichukue mkakati mwingine ili kuweza kuhakikisha kwamba Shule zote ambazo zinahitaji msaada wa kuchangiwa wanaweza kupata msaada wa kuchangiwa kwa kutumia fedha hizi ambazo Wizara ya Elimu na Utamaduni imekuwa ikitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha za *Capitation Grants* zimekuwa zikitolewa kwa shule kwa kutumia idadi ya wanafunzi kwa maana kwamba kama shule ina wanafunzi 1,000 basi ina maana hiyo shule itapata pesa nyingi sana. Lakini kama shule ina watoto 200 na hii nasemea kwa mfano kabisa kwamba katika Manispaa yangu ya Iringa, Jimbo langu la Iringa Mjini, unakuta kwamba kuna baadhi ya shule ambazo zimekaa pembeni kidogo. Majengo yao ni mabovu sana, yanahitaji msaada wa matengenezo. Lakini wanafunzi walioko pale ni wachache sana na kwa sababu pesa inayopatikana inakuja kutokana na idadi ya wanafunzi unakuta shule nyingine zinaishia

labda kupata 70,000; 60,000 au 90,000, wakati shule yenye watoto wengi inaweza ikapata hata milioni tatu.

Kwa maana hiyo, shule hiyo ambayo inahitaji msaada wa matengenezo inapata fedha kidogo na kwa maana ya matengenezo haiwezekani kufanyika. Kwa hiyo, shule ambayo ina wanafunzi wengi inapata fedha nyingi na matengenezo yake yamekuwa yakiendelea vizuri na kwa maana hiyo, kumekuwa na manung'uniko kwamba walimu wakuu wengine wanachukiwa na wazazi kwamba shule fulani wanatoza michango. shule nyingine hawatozi michango.

Hiyo ni kwa sababu ya *Capitation Grants* ambayo inatolewa kutokana na idadi ya wanafunzi. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, mimi naomba sana kwamba utaratibu ubadilike kwa kipindi cha mwaka huu, ili kusudi zile shule ambazo zina mahitaji halisi ya kuweza kujenga au kufanya matengenezo zipate pesa kutokana na mahitaji yake. Kwa sababu nachukua tu mfano pale Iringa unakuta kwamba shule nyingine ambazo sasa hivi zimeshafanya matengenezo ya kutosha na bahati nzuri zenye watoto wengi kwa sababu wazazi wamewakimbizia pale watoto kwa sababu wanajua majengo ni mazuri, wamepata pesa nyingi na matengenezo yale yameshakwisha.

Kwa maana hiyo, sasa hivi inawezekana pengine wameanza tu kujenga ukuta au anachora pengine ramani kwenye ukuta kwa sababu tayari kila kitu wameshajitosheleza au pengine anataka tu kuingiza sasa umeme. Lakini kuna shule nyingine ambayo akiingia mwanafunzi darasani anatumbukia kwa sababu sakafu imechakaa. Lakini mwalimu hana uwezo wa kutengeneza ile sakafu kwa sababu pesa anayopata ni kidogo.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba utaratibu kuanzia mwaka huu ubadilishwe ili pesa hii ya *Capitation Grants* na *Development* iende kutokana na mahitaji ya shule mahali ambapo ipo. La sivyo tutaendelea kuwataka wananchi wachangie kwa kweli hawatachangia na wazazi wale ambao wataambiwa kwamba wachangie hawatakubali kwa sababu wanajua kabisa kwamba Serikali imeshasema kwamba hakuna kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningependa kuchangia ni kuunga mkono yale ambayo wenzangu wameyasema kuhusu maslahi duni ya walimu. Kutokana kuwa na maslahi duni ya walimu kwa kweli hawana uwezo kwa namna yoyote ile hata kujijengea nyumba zao. Kwa hivi, pamoja na kwamba tunaweza tukapandisha mishahara pengine napo inaweza isiwasaidie sana lakini mishahara kwa kweli wapandishiwe. Lakini jambo la msingi ambalo mimi nashauri Serikali ni kwamba kuwe na mkakati maalum wa kuwasaidia hawa walimu ili wakaweze kuwa na nyumba zao.

Kwa mfano, sasa hivi unakuta *National Housing,* inajenga nyumba pale Dar es Salaam na sehemu nyingine. Lakini unakuta wanaopata kwa kweli ni wale wenye uwezo kwa sababu mwalimu kwa kweli hana uwezo wa kuweza kununua nyumba hata kwa bei ya chini kwa maana kwamba kama ni milioni 15 ya kuanzia, milioni 15 mwalimu anakuwa hana uwezo wa kuweza kuipata.

Kwa hiyo, kuwe na mkakati maalum wa kuwajengea walimu nyumba ambazo ni za bei ya chini lakini ambazo wao kutokana na mshahara wanaopata na hata kwa kuja

kutegemea malipo yao ya mwisho, kiinua mgongo basi wakaweze pia kukatwa ili kufidia wanapostaafu na wao wakawe na mahali pa kuishi kuliko hivi ilivyo sasa, mwalimu akishastaafu anarudi mahali ambapo kwa kweli imekuwa ni mahangaiko sana na anabaki anaangalia mwanafunzi wake kama hivi bahati nzuri nina walimu wangu hapa sasa hivi ni Wabunge angalau. Lakini unakuta mwalimu mwingine anamwambia mwanafunzi wake ndiyo Mbunge, na anapita na gari yeye ambaye alimfundisha kwa kweli yuko katika hali mbaya na anajiuliza kwamba hivi hapa *system* hii katika Tanzania ikoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwa upande wa elimu ya sekondari. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuweza kulipia wanafunzi wale ambao wazazi hawana uwezo kabisa lakini pia watoto yatima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado kuna tatizo kubwa kwa maana watoto hawa ni wengi sana ambao wamekuwa ni yatima. Hapa mimi nilipo nina faili zima kubwa ambalo linahusu wanafunzi ambao ni yatima na wazazi wengine hawana uwezo ambapo mtoto amemaliza *Form Four,* amepata bahati ya kuendelea na *Form Five,* lakini hana uwezo wa kuendelea kwa sababu hana uwezo wa kulipa ada na kwa kweli unakuta kwamba maelekezo ya *forms* ambazo walimu wanazitoa anakwambia kabisa kwamba kama huna pesa, basi huyo mtoto asithubutu kuja shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maelekezo kama yale kwa kweli yanatisha, yanamwogopesha hata mzazi au mlezi yule ambaye anakuwa anakaa na yule mtoto na katika hali hii ambapo watoto wengi ni yatima kwa kweli inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka huu tulikuwa tuna sherehe moja pale Mjini Iringa, tukawa tumeita baadhi ya wanafunzi ambao ni yatima lakini wakipata msaada kutoka shirika letu linaitwa *TAHEA.* Walimu walikuja na wanafunzi wachache ambao wanalipiwa na *TAHEA* lakini katika *introduction* kila mwalimu akawa anaeleza kwamba mimi nimekuja na watoto kama 10 lakini shuleni kwangu nina watoto labda 120 au 150 au mwingine anasema nina watoto 200 ambao ni yatima.

Kwa maana hiyo, *primary* atalipiwa na Serikali, sekondari anaweza akapata msaada wa Serikali. Lakini je, baada ya pale atakwenda wapi, kwa sababu hakuna mtu yeyote wa kuweza kumlipia. Ina maana atakapofikia *Form Four, Form Five* hataweza kuendelea na Chuo Kikuu hataweza kuendelea.

Kwa hiyo, njia rahisi na ya moja kwa moja ni kufuta ada katika shule za serikali na hata ikibidi hata Kidato cha Nne na cha Tano na cha Sita ili hawa watoto ambao ni yatima na ambao hawana uwezo kwa kweli wakaweza kusoma bure hadi watakapofikia kule Chuo Kikuu, basi wakaweze kupata ule mkopo ambapo tutategemea kwamba Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu italeta pengine Muswada hapa ili kusudi kuwezesha ule mfuko ambao Serikali ilishaahidi kwamba wataweza kupata mikopo ili wanafunzi wote bila kujali kama yuko Serikalini au upande wa *Private* ataweza kulipiwa. Kwa hiyo, bila hivyo haitawezekana watoto wetu tutakuja kustukia tuna watoto wengi ambao wameishia *Form Four* lakini wamekosa kuendelea na Elimu ya Sekondari kwa sababu uwezo wao wazazi hawana au walezi wanaokaa nao hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kurudia tena kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niwe mmoja wa wachangiaji jioni hii kuchangia hotuba hii ambayo iko mbele yetu hotuba ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kwa kweli hotuba hii ni safi kabisa na hakukuwa na mengi ya kuweza kuyanokoa nokoa kwa kuyasahihisha. Ila ni kawaida yetu kwamba lazima hapa na pale tuweze kujalizia jalizia, lakini liwe kamilifu mno. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, basi naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea hotuba ambayo ina upeo mkubwa sana na ni hotuba ambayo inatuelekeza au inatupa dira ya wapi tunakwenda katika miaka inayofuata na labda ni kwamba kama tutakuwa na hotuba safi kabisa kama hii katika miaka miwili mitatu ijayo watani zetu mwaka 2005 kwa heri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niwapongeze watendaji wa Wizara hii kuanzia Katibu Mkuu, Wakurugenzi, tujipongeze na sisi. Mimi hapa niliyesimama, nimo katika Kamati ya Huduma za Jamii ambayo *portfolio* yetu moja ya Wizara hii. Sisi tuwapongeze, kwa sababu kwa ushirikiano wao na kwa sababu ya kuwa karibu nasi, tumeweza kuleta kitu ambacho hata wachangiaji wa mekuwa kidogo sana. Tunawapongezeni sana. *(Makofi)*

Naomba nitoe pole kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, lakini tumefarijika kupata habari kwamba amerudi matibabuni India na si muda mrefu labda ataungana na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii vile vile kuwapa pole ndugu zetu wa Mwanza kwa *accident* iliyotokea ambapo kwa mujibu wa vyombo vya habari kuna watu kama 17 wamekufa na zaidi ya 50 wamejeruhiwa. Tunawapa pole sana, Mungu awape subira kwa haya yaliyotokea na *inshallah* na sisi atupe salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu ambayo nataka kujaliza, pamoja na uzuri wa hotuba hii, kuna suala ambalo tumelizungumza au nimelizungumza katika vikao viwili, vitatu vilivyopita
na leo nataka kuongezea, nachukua nafasi hii kuliongelea tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitalia, lakini nitaendelea kulizungumzia suala hili mpaka pale litakaposikika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lenyewe ni kwamba tungeomba Serikali ikaondoa kero hii inayotukabili mbele yetu ambayo nasema kwamba limebakia ni hili suala la kupandisha kiwango cha elimu ya msingi kutoka darasa la saba angalau kufikia mpaka darasa la kumi.

Suala hili tumelizungumzia ndani ya Kamati, tumelizungumzia wakati mwingine katika vikao na katika akili ya kawaida haliingii wala sioni kwamba kuna mantiki ya kwamba mtoto anaanza darasa la kwanza akiwa na umri wa miaka saba, anamaliza darasa la saba ana umri wa miaka 13 au 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunazungumza kwamba mtoto huyu hawezi kuajiriwa, wakati akiwa na umri wa miaka 13 anakuwa ameshamaliza elimu ya msingi yaani darasa la saba, wakati huo huo unasema sasa hivi nenda kwa jamii, huyu mtoto aende akafanye nini kwa jamii? Hapa tunaunda kundi la vijana ambalo lina nguvu na baadaye hatutoweza kulidhibiti na kulizuia na kwa maana hii hakuna mantiki ya kusema kwamba umaskini utaondoka wakati elimu au wakati vyombo vinavyoshikamana na elimu vinatuambia ya kwamba ili umaskini uondoke basi ni lazima kiwango cha elimu kiwe kimezidi. Hawa wakiishia darasa la saba na kuingia mitaani hawajisaidii wao wenyewe na pia wala hawawezi kuwasaidia wazee wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwamba kuna mambo mawili makubwa sana ambayo yamefanyika. La kwanza, ni kuondoa ada zile za shilingi 2,000/= wakati mtoto anapoingia darasa la kwanza na pili, kama hilo halitoshi ni kuondoa hii kodi ya maendeleo. Hili lililobakia na ili wenzetu watusindikize katika hili basi hili la darasa la saba kwamba kiwango cha elimu ya msingi kumalizika, nadhani hili nalo Mheshimiwa Waziri mimi kama nilivyosema mwanzo ningeomba nalo lifanyiwe kazi na lionekane kwamba angalau basi tuwe tuna muda maalum, tunapanga kwamba elimu ya msingi inatoka darasa la saba wanakwenda darasa la kumi au kidato cha pili. Ikifika muda huo utakuta huyu mtoto atakuwa na umri kati ya miaka 17 na 18, huyu mtoto atakuwa tayari kufanya jambo lolote lile la maana kuliko tukamwacha katika umri wa miaka 13 au 14 akaingia mitaani na anakuwa hana la kufanya. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, kuna suala hili la kufanyiwa *repetition* watoto wanaofika darasa la nne ikiwa hakufaulu alama 45, kitu kama hicho pamoja na kupasi somo la hesabu. Mimi sipingani nalo lakini ningependa kutoa rai kwamba Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Watendaji mkaliangalia hili, kwa nini hawa watoto tusingelianza kuwachuja kutoka darasa la kwanza, toka anapoanza?

Kwa hiyo, tunaanza darasa la kwanza akifeli tunamrudisha, darasa la pili hakuweza kupasi maksi zinazotakiwa tunamrudisha kwa sababu hawa wakifika darasa la nne inakuwa hawezi kuendelea kwa sababu anakuwa amefeli. Ilifika wakati fulani tukamwuliza Mheshimiwa Waziri kama anakumbuka sawa sawa ilikuwa kidogo tulicheka sote, tukamwambia Mheshimiwa, kama darasa hili la nne wote hawakupasi ni kitu gani kitakachotokea? Akatuambia tutabadilisha kile kibao cha darasa la tano tutaweka kibao cha darasa la nne. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui tutakuwa tunabadilisha vibao vingapi kutoka darasa la tano tunaweka kibao cha darasa la nne kwa maana ya kwamba hawakupasi hisabati kwa mujibu wa maksi zinazotakiwa au alama zinazotakiwa. Kwa hiyo, kama tungelianza mwanzo kuwachuja, tungefika mahala tusingekuwa na kazi ya kiasi hicho ya kuwachuja kuwaambia kwamba darasa zima haliendi na huku tunakwenda na darasa lile

limekufa na umri wao unakwenda na kila kitu.  Kwa hiyo, hili nalo ningeomba liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwamba kulikuwa kuna suala la vijana inawezekana sio Wizara yake lakini umaskini na elimu.  Najua kuna Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kuna Wizara ya!  Si umaskini *as such* lakini najua kwamba na elimu, lakini hapa nataka kuunganisha kitu gani?  Huyu kijana anayekuwa amemaliza kidato cha pili, hapa ninachotaka kueleza ni kwamba hao vijana wanaokuwa wamemaliza kidato cha pili ambao watakuwa ni wengi tuna Jeshi hili la Kujenga Taifa, tuna mpango huu wa kuhimiza kilimo na wale ambao watakuwa wanashindwa kuendelea na kidato cha tatu kwa maana ya kwamba kama mpango huu ungelifuatwa, ni kusema kwamba hawa tuwapeleke katika Jeshi la Kujenga Taifa au tuwapeleke katika hizi Shule za *VETA* ya kwamba hawa upande mmoja watatusaidia kwamba ajira tumewapa kwa hiyo tutakuwa tumepunguza upungufu wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili vile vile watakuwa wanajifunza kilimo. Baada ya muda fulani wakimaliza, watakuwa wakulima bora zaidi lakini wakati huo sisi kilimo tutakuwa tunakiendeleza na tunaondosha tatizo la ajira katika nchi yetu.  Tatizo la ajira na vijana ni *timing bomb* wakati wowote likilipuka tutakuwa hatuwezi kulizuia na mahala pa kuanzia hili na kuondoa suala hili ni kuzingatia humu mahala tunapozungumza, amemaliza kidato cha pili au amemaliza kidato cha nne waende katika JKT ama waende *VETA* kwa maana ya kwamba kujifunza kazi na amani.  Nadhani hilo litakuwa limeeleweka.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni kutoa shukrani za dhati, najua siyo Wizara yake lakini ni kusema kwamba *TASAF* hasa kwa upande wa Zanzibar wametusaidia sana katika kuinua ujenzi hasa mashule.  Wenzetu huku Dar es Salaam au Tanzania Bara mnayo hii MMEM.  Ilikuwa tumwulize Mheshimiwa Waziri lakini nimepata ushauri na wenzangu tumesema hapana, tumvute Mheshimiwa Waziri chemba ili tumwulize hii MMEM na Zanzibar iko vipi tusiilete hapa.  *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri itafika wakati tuje kukuuliza utuambie MMEM hii iko vipi kwa Zanzibar ili isije kama ilivyokuwa imekuja *TASAF*.  *TASAF* ni chombo ambacho kinatusaidia kwa hali ya juu hasa sisi Waheshimiwa Wabunge katika ujenzi wa mashule, ujenzi wa hospitali na mambo ya maji inatusaidia sana. Sasa tulipoikuta *TASAF* na tunavyoisikia MMEM inavyochakalika huko mitaani tukasema hebu na hii nayo tuisikilize kama kuna uwezekano wa kuifanyia kazi basi tuifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.  *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa kutuletea hotuba nzuri yenye kusheheni takwimu na hali halisi ya elimu hapa nchi. Hongereni sana, ni kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa madarasa katika Mpango huu wa MMEM aliokuwa anausema mwenzangu wa Zanzibar hapa, umeonyesha kabisa kwamba palipo na nia na usimamizi mzuri kazi nzuri inaweza kufanyika na kwa kweli imeonyesha kwamba kama tungekuwa tunaweka usimamizi mzuri kwa kiasi hicho kati ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama ulivyowekwa hapa, mimi nadhani nchi hii ingeondoka kwenye matatizo mengi ambayo tunayaona maana fedha siyo kidogo. Tatizo la nchi yetu ni usimamizi mbovu wa miradi na wakati wa kutekeleza shughuli zetu.

Kwa hiyo, napenda sana niwape hongera wenzetu hawa ambao kwa kweli wameonyesha njia na tungependa Wizara nyingine na Idara za Serikali zingefuata na kuiga mfano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata ongezeko kubwa la kuandikisha watoto wa shule za msingi tangu mwaka jana kuanzia huko nyuma 800,000 hadi kufikia 1,600,400 hivi. Haya ni maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haya maendeleo lazima yapimwe na kuwa watoto hawa watakapokuwa wamemaliza shule za msingi watakwenda wapi. Kwa sababu hali yetu ya shule za sekondari nchini sasa, ni ya kusikitisha kabisa. Kwa sababu ukilinganisha na majirani zetu, Mheshimiwa Waziri ametueleza katika hotuba yake hii nzuri kwamba sasa tunao watoto kama 344,000 ambao wapo katika shule za sekondari. Mimi ninaamini kabisa kwamba hawa ni watoto walioko kwenye *register* tu lakini ukienda shuleni watoto hawa hawapo wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kitu cha ku-*test* vizuri ni watoto wanapomaliza *form four.* Mwaka 2002 waliofanya mtihani na kuhitimu walikuwa 39,000 hivi ukizidisha mara nne unaweza kujua hali yetu huko kwenye sekondari iko namna gani. Lakini ukilinganisha 344,000 tulizoambiwa leo na 1,300,000 kwa majirani zetu wa Kenya pia unajua kwamba tuko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu za Mashirika kama *UNESCO,* Tanzania ni ya mwisho duniani katika kutoa elimu ya vijana wa umri kati ya miaka 13 na 18. Sasa sisi hapa tumepata takwimu kwamba watoto walioko sekondari ni asilimia 12 lakini unaelewa kabisa kwamba mwaka 2002 tuliwaandikisha watoto 1,600,000 na huko nyuma mwaka uliopita tuliandikisha watoto 800,000. Sasa hawa watoto 800,000 ambao walikosa elimu ya msingi hapa hawakuwa *factored* katika hii *percent* 12 ambayo tumepewa katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na pia watoto hawa ambao wanakosa shule kwa *drop out* za aina mbalimbali hawako katika namba hii. Namba ambayo tumepewa ya asilimia 12 inalenga wale watoto walioko ndani ya *register.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watoto ambao wanaondoka shuleni, wanaondoka kwa sababu gani?

Karibu asilimia 40 mpaka 50 ya watoto hawaendi shule kwa sababu ya ada. Kumpeleka mtoto darasa la tisa ni kikwazo kikubwa mno kwa sababu mzazi huyu aliyeshindwa kulipwa shilingi 2,700/= katika elimu ya msingi ndiyo huyo huyo anayetakiwa kumpeleka mtoto alipe ada ya shilingi 40,000/=, adaiwe majengo shilingi 20,000/=, adaiwe dawati la shilingi 15,000/=, chakula cha mchana shilingi 20,000/=, tahadhari ya shilingi 10,000/= na nguo shilingi 15,000/=, ukizijumlisha kwa pamoja ukaongeza kwamba lazima anunue viatu sasa maana huwezi kwenda sekondari huku unapekua, basi utakuta kumpeleka mtoto darasa la tisa ni lazima utafute shilingi 120,000/= mpaka shilingi 135,000/=. Sasa mtu ambaye hawezi kupata shilingi 2,700/=, shilingi 120,000/= atazipata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata kama hali ya uchumi haiwezi kuendelea mbele, haiwezi kuwa nzuri, ni lazima tuangalie jinsi gani tutawapeleka watoto wetu *form one.* Katika eneo hili maana baada ya *form one* wale watoto ambao wameweza kwenda *form one* wanaendelea kwa sababu wamebakiza ada na chakula peke yake.

Kwa hiyo, tufikirie jinsi ya kupunguza gharama kwa *form one. At least* tuseme ada isilipwe mtu akiwa *form one,* tuseme na labda wasidaiwe majengo na madawati, mimi sijui tufanyeje, lakini lazima tutafute shilingi bilioni 20 zinazotakiwa kutekeleza hili. Haiwezekani tuwe wa mwisho duniani halafu hatuna jawabu, haiwezekani. Lazima tutafute jawabu la kujiondoa wa mwisho duniani, hatuwezi kuwa wa mwisho zaidi ya Niger na Ivory Coast, hatuwezi kuwa chini ya nchi hizi ambazo hazina chochote lakini zinawapeleka watoto shule. Kwa hiyo, lazima tutafute njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli napendekeza kwa dhati kabisa kwamba ada hii ya shilingi 40,000/= mtoto akiwa *form one* asilipe na pia mtoto akiwa *form one* asilipe shilingi 20,000/= hizi za majengo aachwe alipe akiwa *form two* maana wakiishaingia gharama zinakuwa ndogo, lakini hatua hii ya kuingia *form one* ni ngumu sana na hii lazima tuitafutie jawabu lake. Mimi nadhani katika Bajeti yote ya shilingi trilioni 2.4 tunaweza kupata shilingi bilioni 20 za kuweza kutafuta jawabu hili, kupanga ni kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo linakuja kuja hapa na maswali yanapoulizwa hapa Bungeni unaona. Kwa kweli kiu ya elimu imekuwa kubwa sana na watu wenye njaa ambao ni wa mwisho duniani katika kutoa elimu ya sekondari kwa watoto wake unaweza kuelewa kwa nini wanaanza kunyoosheana vidole kwamba wewe unapata zaidi na sisi tunapata kidogo.

Kwa kweli ni vema Serikali ikaangalia sera iliyoko sasa ya kuwaambia wananchi kwamba ni jukumu lenu kujenga shule za sekondari na Serikali itawasaidia kwa njia yoyote ile. Ikaenda ikatafuta hivi ni kwa nini katika Wilaya nyingine shule hizi

hazikujengwa? Pamoja na kusukuma kwamba zijengwe lazima tutafute hivi ni kwa nini katika Wilaya ya Mtwara wamejenga shule mbili tu, hili lazima tutafute. Tukishapata ni sababu gani tutafute jawabu, tusipotafuta jawabu tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu kwa sababu maendeleo hayawezi kuja kwa watu ambao hawakusoma. Ni lazima tuweke uwiano huu uwe mzuri na tujaribu jamani tufikie asilimia 50 yaani kuwapeleka watoto asilimia 50 katika shule za sekondari.

Kama tulivyopanga ukiangalia katika mipango yetu yote *poverty, strategy paper, poverty removal* na mambo mengine mengi haya ambayo tunasema mazuri mazuri lazima tuanze sasa. Huwezi kuwa na shule ya sekondari za kutosha mwaka 2007 kama hukuanza kuzijenga leo na kama unajenga na wanavijiji lazima uanze sasa.

Pia ninataka niseme kitu kidogo juu ya mtazamo wa Wizara kuhusu kufikia hilo lengo la kuwapeleka watoto asilimia 50 katika shule za sekondari mwaka 2007. Nilikaa na wenzangu katika Wilaya yangu tukaangalia ni jinsi gani tunavyoweza kuwapeleka watoto wetu asilimia 50 itakapofika mwaka 2007, tukaona ni lazima tuwe na shule za ziada za wananchi shule nyingine sita. Kwa sasa tunazo shule nane. Sasa ili tuweze kufikia kiwango cha asilimia 50 na tuweze kufikia malengo na maelekezo ya Wizara, ni lazima shule zilizopo tuzifikishe madarasa manne manne au mikondo minne halafu tujenge na shule nyingine sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi maelezo niliyoyapata kutoka Wizarani hayakuniridhisha kwa sababu Wizara inaangalia zile shule za Jumuiya pamoja na shule za watu binafsi na za mashirika, wanasema ninyi tayari mna shule hapo hizo ndiyo zitakazowapeleka watoto asilimia 50, hiyo haiwezekani.

Tunazo shule 12 za watu binafsi na za mashirika kule Wilayani Mwanga lakini katika watoto 5,400 wanaosoma katika shule hizo watoto wa Mwanga wako 400 peke yake. Watoto wanaosoma pale ni watoto wa Tanzania na mimi nadhani ni kitu kizuri lakini huwezi kuwaambia watu wa Mwanga kwamba msijenge shule za kutwa kwa sababu hizo zinazowachukua watoto kutoka Dar es Salaam ziko kwenu, haiwezekani. Watoto wa Mwanga wale wanaokaa nyumbani na ambao hawana pesa ya kulipa shilingi 300,000/= au shilingi 400,000/= zinazokuwa *charged* kwenye shule zile wanahitaji kwenda shule hata kama kuna shule za private ziko katika Jimbo langu mimi.

Kwa hiyo, maombi yetu ya wana Mwanga yako pale pale kwamba ili tufikie kiwango cha asilimia 50 kwa watoto wanaoingia sekondari ni lazima tujenge shule mpya na tunaiomba Serikali ituunge mkono. Mimi ninaiomba Serikali pia iangalie mipango ya Wilaya zote bila kujali shule za *private* ziko ngapi katika Wilaya hizo, iwasaidie wananchi na pale inapobidi ambapo wananchi hawajengi kabisa, Serikali itumie *Budget otherwise* tutakuwa na kitu ambacho hatuwezi kukisahihisha huko mbele. Hapa tulipo tunaweza kufanya masahihisho tukaleta uwiano mzuri kati ya Wilaya na Wilaya na kati ya Mkoa na Mkoa lakini tutakapokwenda mbele bila kuleta uwiano huo tutakuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mwisho, napenda na mimi niongee leo kuhusu mishahara ya walimu. Walimu ndio wanaolifundisha Taifa hili na ndio wanaohakikisha kwamba Taifa linakwenda mbele au haliendi mbele. Mataifa ya Ulaya ya Kaskazini kama Scandinavia, *the best people go to education they go to become teachers* na nchi zile zinawalipa ili wawe walimu na kufundisha Taifa ambalo linasonga mbele. Hapa kwetu *messenger* wa shirika la kukusanya kodi analipwa zaidi ya mwalimu, sasa unajua *what message we send?* Tunapeleka ujumbe gani kwa walimu kwamba mwalimu na *messenger* wa *TRA, messenger* wa *TRA* ni muhimu zaidi. *(Makofi)*

Mimi nadhani wakati umefika ni lazima tuangalie mdomo wetu uko wapi, tuwalipe walimu vizuri, *we must pay.* Kwenye Jimbo langu kule nina shule yangu mmoja inaitwa Emangulai kule Kirya, walimu hawakai kule kwa sababu wako mbali na Mjini, hakuna usafiri wa gari na pia hakuna huduma zingine. Hivyo lazima wapewe *incentive* ya kukaa kule. Lazima tuangalie mazingira wanapofanya kazi walimu na tuyatengeneze vizuri ili watoto wetu wawe na elimu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuweze kuwa na watu ambao wanafanya kazi nyingine na wapende kwenda kwenye ualimu. Mwaka huu zaidi ya watoto 7,000 walio-*qualify* kuingia *form five* katika nchi yetu hawakwenda kwa sababu hatuna walimu wa kufundisha *A-Level.* Kwa nini tukose walimu wa kufundisha *A-Level* na tunawafundisha walimu kwenye Vyuo Vikuu kila siku? Ni kwa sababu hatuwalipi walimu hawa. Unampeleka mwalimu *Mwenge Secondary School,* unamwacha pale bila *incentive.* Anaondoka *Mwenge Secondary School* atakwenda Dar es Salaam apate pesa nzuri zaidi halafu aishi maisha mazuri zaidi. Kwa hiyo, ni lazima tuwaangalie walimu wetu na tuangalie mazingira wanapofanya kazi na tuyarekebishe mazingira hayo, hatuwezi kusema hatuwezi, tutaweza nini Watanzania, tutaweza kitu gani? Kupanga ni kuchagua, lazima tuchague mambo yatakayotuletea maendeleo. Mambo ya kesho na kesho kutwa hatuwezi kuangalia mambo ya jana tu, jana imekwisha na kesho hata kama mtu ungekufa wewe mwenyewe, kesho itakuja tu na lazima tujitayarishe kupambana na kesho. Na Taifa hili lazima lijitayarishe kupambana na kesho haliwezi kuongea na kuishi kwa *glory* ya jana peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimeona hapa katika mgawanyo wa madarasa kwamba katika mgawanyo huu utakaopeleka fedha mwezi Julai, Jimbo langu litapewa madarasa saba. Sasa nilikuwa na maombi rasmi kabisa kwamba ninajenga shule tatu za wafugaji, ningependa nipewe madarasa tisa ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara hii. Kabla sijaanza napenda niungane na mchangiaji aliyemaliza sasa hivi kwamba Wizara iwe makini sana kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge na maoni ya wananchi juu ya suala zima la walimu. *(Makofi)*

Mimi maeneo mawili ndio naona muhimu sana katika nchi yetu na katika dunia, suala la walimu na waandishi wa habari. Hatuwezi kuwapata walimu kama hawakuwapata walimu mwanzo wa kuweza kuwafundisha. Pia waandishi wa habari, nchi yetu kama itakuwa na waandishi wa habari wazuri kwa kweli mambo mengi yanaweza yakaisaidia jamii kwa muda mfupi sana. Kwa hiyo, naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameeleza majukumu ya Wizara na ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwamba, Wizara hii ndiyo itakayoleta maendeleo makubwa katika Taifa letu hili la Tanzania. Tunataka wafahamu hivyo kwa sababu uchumi wowote wa nchi yoyote duniani unategemea elimu. Sayansi na teknolojia ndiyo msingi mkuu wa uchumi kwa nchi yoyote ile duniani. Bila ya elimu ya kiwango cha juu kutoka msingi wa chini kabisa tukaja katikati tukafikia juu, mimi naamini hatuwezi kufikia pale ambapo tumekusudia. Hata Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu anategemea msingi ambao utakuwa umejengwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni kutoka huku chini, hawezi kuchukua watu kwenda Vyuo Vikuu kama watakuwa hawana elimu ya kutosha kutoka huku chini. Kwa hiyo, nataka wajifahamu kwamba wao ndio msingi mkubwa wa kuweza kulitoa Taifa hili katika umaskini mkubwa huko mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameelezea majukumu saba hapa ambayo Wizara yake imeyasimamia kuanzia mwaka 2002 mpaka mwaka 2003 na watayaendeleza mwaka 2003/2004. Nataka ninukuu majukumu matano katika hayo. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba la kwanza, ni elimu ya msingi na ya awali, ndiyo ile ambayo niliigusia mwanzo. Lakini kuna sehemu ya pili, ni juu ya elimu ya sekondari ya kawaida, kidato cha kwanza mpaka cha nne na elimu ya sekondari ya juu kidato cha tano mpaka cha sita.

Vile vile Mheshimiwa Waziri aligusia juu ya elimu maalum *(special education)* itolewayo kwa wenye ulemavu kama vile wasioona, viziwi na wenye ulemavu wa akili na kadhalika. Nataka hapa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu ninafarijika kila nikija kwenye Bunge, kipindi cha mwanzo Bunge linapoanza huwa kuna wale nafikiri watakuwa ni viziwi, tuna kunywa nao chai asubuhi pale, huwa wanaudhuria Bunge na wanakuwa na mawasiliano ya elimu yao ambayo wanayo, huwa nafarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika maeneo haya ni lazima tuwaunganishe Watanzania wenzetu ambapo kutakuwa na mapungufu fulani ili waweze kuwa na mawasiliano ambayo ni ya kuweza kuwasiliana ambacho kimoja ni kitu cha elimu. Kwa hiyo, eneo hili napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri hata tukiangalia kwenye *ITV* wanatoa kutokana zile *signal* kwa wale wanaozungumza kama viziwi. Kwa hiyo, elimu ni kitu cha msingi kwa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikiendelea kwenye Na. 4 kwamba elimu ya watu wazima *(Adult Education)* ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya msingi na sekondari kwa mfumo usio rasmi kwa watoto na watu wazima walioikosa. Sasa hapa kidogo ni ipi elimu isiyo rasmi, tunachopendekeza kwamba walioikosa au vipi?

Tusifanye kitu ambacho kina kasoro, tuifanye elimu kamili. Hapa kidogo nimeshtuka naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha aseme ni ipi. Malengo ni mazuri kama kuna watoto waliokosa elimu lakini tumewaandalia mazingira kwamba wapate elimu lakini kuna eneo lingine wanasema isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ni juu ya utamaduni wa Taifa ikiwemo lugha, sana, mila na desturi na ukaguzi huu wa elimu. Mimi nataka nije kwenye lugha. Tanzania lugha yetu kuu ni lugha ya kiswahili na niwatake viongozi wa Serikali waitumie lugha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza Kiongozi wa Kitaifa au Mheshimiwa Waziri anazungumza katika *function* yoyote anashindwa kuitumia lugha ya kiswahili. Nilifarijika sana hivi karibuni nilipomkuta Balozi wa *EU* anazungumza kiswahili kupitia *television* na pia Mheshimiwa Rais Joseph Kabila, juzi amezungumza kuhusu Serikali, amezungumza kiswahili, sasa Tanzania unamkuta Mheshimiwa Waziri katika *function* anazungumza kiingereza, mnatupeleka wapi? Kama leo tunaambiwa kwamba katika nyumba ya Malkia kiswahili wanakitafuta na halafu sasa hivi Japan wana-*train* katika Chuo Kikuu. Kwa hiyo, katika hili mimi nataka Wizara hii isimamie kwamba lugha ya kiswahili ndiyo lugha yetu ya Taifa na viongozi wa Serikali waitumie. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa tatu namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuzungumzia dira na malengo maalum ya Wizara yake. Nchi yoyote ili ifanikiwe kufika ni lazima kuwe na dira ambayo itaifikisha pale na dira yoyote ya nchi au ya Wizara inategemea wasomi na wataalam wanaotokea katika nchi ile.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba wataalam na wasomi walioko katika Wizara hii pamoja na walioko Serikalini watashirikiana kuangalia matatizo wanayopata wananchi wetu juu ya suala zima la elimu. Kwa hiyo, hili ni jukumu lingine nataka niliachie Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimnukuu Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kutokana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania *(Tanzania Development Vision 2025),* Wizara imeandaa dira *(vision)* na dhima *(mission)* yake, hongereni sana kwa sababu bila kuwa na maandalizi, mipango hufiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sisi Bunge linatuandalia kutoka Majimboni, Dar es Salaam mpaka Dodoma na hata tukitaka kuondoka hapa tunapangiwa hivyo hivyo, maandalizi ya safari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri isiwe umeweka katika kitabu tu tunataka dira hii ifanye kazi na moja ni kuhakikisha kwamba vijana wetu wa Tanzania wamepata elimu ya kiwango cha juu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niende ukurasa wa 17 ambao unazungumzia juu ya Idara ya Elimu ya Sekondari. Ameeleza mafanikio yaliyopatikana mwaka 2002/2003 na akainisha kwamba mwaka 2002 tulipata mafanikio asilimia sita kwenye idadi ya wanafunzi 1,024 mwaka 2003 tumepata mafanikio ya wanafunzi 1,083. Nataka

nijue mafanikio hayo ni pamoja na Zanzibar? Kwa sababu Zanzibar inafanya mtihani wa Taifa na walikuwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 18 anasema wanafunzi wa Kidato cha I - IV waliongezeka kwa asilimia nane kufikia 319,487. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, lakini isiwe kufikia tu ni kuhakikisha kwamba wanatoka na elimu ya kiwango cha juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 19, ametoa kielelezo Na.14.1(b) ambacho kinasema kinahusu Jumla ya Wanafunzi wa Kidato cha I-IV, idadi ya vijana wa umri wa miaka 14-17 mwaka 1999-2003 nafikiri watakuwa ndio hawa wanaomaliza shule na kama vijana wote wanamaliza shule kwa umri huu, tunaliambia nini Taifa? Vile vile nataka wataalam wa Wizara hii wafanye utafiti kwa sababu miaka 17 hajafikia hata umri wa kubalehe wa miaka 18 akaanza kujitegemea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kitu cha muhimu ni kuangalia athari kama kijana atakuwa amemaliza *Form IV* na umri wake ukiwa ni huu tunamfikiria vipi kwa maisha ya baadaye? Ndio maana Waheshimiwa Wabunge wakapendekeza shule ya msingi mpaka sekondari iwe elimu ya bure na hili tusilifanyie ubishi, ni elimu tu ndio itakayosaidia kuondokana na matatizo yetu sio jambo lingine, tunazungumzia kupambana na umaskini ni elimu tu itakayotusaidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nataka ulione hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda ukurasa wa 44, Mheshimiwa Waziri ameelezea juu ya Baraza la Mitihani (BAMITA) amesema kwamba katika mwaka 2002/2003 mitihani ya Kitaifa ya kumaliza Elimu ya Msingi ya Darasa la Saba Tanzania Bara, tunataka mpaangalie hapo vijana wetu wakimaliza Darasa la Saba lakini twende Elimu ya Sekondari ya Kidato cha Nne, Elimu ya Kidato cha Sita pamoja na Mitihani ya Ualimu Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ndio pale nilitaka kujua katika ile idadi ya wanafunzi je Zanzibar imo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar inafanya mtihani wa Taifa, nataka nijue je *syllabus* kutoka *Form I - IV* ni moja Tanzania nzima? Kwa sababu isije tokea wanafunzi wetu wa Zanzibar wakaonekana wako nyuma kielimu kutokana pengine na mfumo mzima wa elimu ya Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwenzangu alifanya woga juu ya ile ya MMEM lakini mimi nasema Mheshimiwa Waziri tunaona choyo unapotoa matumizi na mgao wa fedha kwa Wabunge wenzetu walioko Bara sisi ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara ya Elimu iko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba Serikali ifikirie tena suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni katika ukurasa wa 57 ambapo anasema Baraza la Kiswahili la Taifa litatekeleza majukumu matatu ya kukuza Kiswahili. Katika majukumu hayo ni kuhakikisha kwamba viongozi wote walioko Serikali hata katika Umoja wa Mataifa wanazungumza lugha yetu ya Taifa ili asilimia 80 ya wananchi

waweze kuwasiliana na kiongozi wa nchi moja kwa moja kama ambavyo amefanya Mheshimiwa Rais alipotoa hotuba yake ya kila mwezi kupitia kwenye redioa alipokuwa *Poland* na wananchi wakaipata moja kwa moja. Wenzetu Waarabu tunamwona Waziri Mkuu wa Israel anazungumza lugha ya Kiarabu kwa hiyo na sisi tusiwe waoga kuzungumza lugha yetu kuhofia kwamba labda tutaonekana tuna mapungufu fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni juu ya suala la UKIMWI. Mheshimiwa Waziri na wataalam, inasemeka kwamba Walimu wengi wanaathirika kwa UKIMWI, tunaomba mlifanyie kazi suala hili, ni aibu. Kama kuna Walimu labda wanasumbuka sana wamekaa muda mrefu sana hawajaoa wapeni uwezo waoe ili waepukane na janga kama hili. Ni aibu kwa binadamu kuambiwa kwamba ana matatizo ya UKIMWI. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alichukue hili atakapokuja kuwasilisha bajeti ya Wizara yake anisaidie, zile mashine za kukata nywele kwa sisi wengine tunaokata nywele haziwezi kusababisha kupata UKIMWI. Kwa sababu tunaogopa ile hit ya umeme kwamba haifiki kule na hatuamini kwamba spirit inaua wale virus wa UKIMWI, kwa kweli hili nina hofu nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina woga tarehe 25/6/2003 nimepima sina kitu, cheti hiki hapa, sina *sugar,* sina chochote na Waheshimiwa Wabunge msigope, hiki hapa. Kwa hiyo, Walimu wasiwe waoga tuwawezeshe kumiliki nyumba zao ili kuwaepusha na matatizo haya. (*Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka niliongezee, kwa kweli nakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutupa taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri sisi wengine tulikuwa tunasumbuka sana, tunakupongeza sana. Lingine ni juu ya kupunguza muda wa kuanza Kidato cha Tano na Kidato cha Sita kutoka mwezi Julai kuanza mwanzo wa mwaka, tunakupongeza sana. Kwa maeneo mengine yote mpaka Vyuo Vikuu tunaomba Serikali iliangalie hili kwa sababu tunakuwa na hofu kuna vijana wanawezakuwa wame-*pass* lakini hapa katikati kutoka Januari mpaka Mei wakajiajiri akaona tabu kujiunga na shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia mafanikio Mheshimiwa Waziri, Wizara na Serikali kwa jumla na napenda kuwaambia kwamba mkombozi wa Taifa hili kutoka katika umaskini ni elimu ya kiwango cha juu kwa vijana wetu katika Taifa letu hili la Tanzania na mhimili wetu mkuu ni Wizara ya Elimu na Utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kujadili hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja, mimi ni mjumbe wa Kamati, nakiri kabisa kwamba Wizara hii inafanya mambo mengi mazuri sana na ni

Wizara kubwa. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwanza Waziri mwenyewe na viongozi wa Wizara hii ambao ni Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na wasaidizi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwape pole kwa Naibu Waziri, Ndugu yetu Mheshimiwa Sakila, tumefarijika sana tulipopewa taarifa leo kwamba amerudi kutoka India tuna imani ataungana nasi. Tunaomba Mungu azidi kumsaidia aje, tuna hamu naye sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara ya Elimu na Utamaduni ni Wizara ambayo kama wenzangu walivyokwishasema ndio mhimili mkubwa wa maendeleo katika nchi. Wote tulioko katika jengo hili hakuna mtu ambaye anaweza kukana kwamba hakupitia katika mikono ya Mwalimu hata Waandishi wa Habari bila Mwalimu kufanya yake vizuri nadhani wasingekuwa pale, hata wale wapiga picha, hata wavumbuzi wa kamera, hata wajenzi, hata watu wote wa *TRA* hakuna ambaye hakupitia mkononi mwa Mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninasononeka sana ninapoanza kuona kwamba watu wanasema kazi ya Ualimu ni wito, ni kujitolea na haki asifikifikirie, kwa kweli inasonenesha sana. Nafikiri kuna haja ya kumfikiria sana huyu Mwalimu. Kumlinganisha Mwalimu na watu wengine nadhani tunamnyima haki ni sawasawa na kulisha pua ukasahau mdomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, naanza na kuzungumzia maslahi ya Walimu. Kwa kweli naomba Serikali, mimi ni mwanakamati nilizungumza na mwaka jana nilizungumza, muda sasa umefika wa kuangalia maslahi ya Walimu na kuwapa haki zao wanapodai au wanazostahili. Inasikitisha sana unapoona Mwalimu anakwenda likizo hapewi haki zake. Anahamishwa kwa mkataba mpaka anahamishwa tena bado hajalipwa, Mwalimu kakosa nini jamani? Hizo ni haki zake za msingi anatakiwa apewe ukiacha mambo ya kumwongezea mshahara, kwa nini lakini hapewi. Anafanya kazi ya ziada halipwi sidhani kama kuna Mwalimu yeyote amewahi kulipwa kwa kazi ya ziada kama yupo Wizara iniambie kwamba yupo sana sana atasema Mwalimu ni kama Mbunge hapewi hela ya ziada ni kama Waziri ni kama nani lakini ukweli ni kwamba naye anastahili kupewa hizo haki. Kwa hiyo, mimi binafsi bado naona kuna haja ya Serikali sasa hivi kuchukua hatua kuangalia maslahi ya Mwalimu. Mwalimu anaishi katika mazingira magumu. Kuna Walimu ambao ukienda kwenye nyumba wanazoishi sehemu za kwangu katika Wilaya ya Geita utakuta katika nyumba kama ni usiku kama ana koroboi ndani unachungulia umwona alivyolala, mazingira yao kwa kweli ni magumu naomba tuwasaidie Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata vyeo vyeo kwa kweli havieleweki. Headmaster wa Shule kubwa na ndogo utakuta wote wanaenda sawa tu na ikiwezekana unakuta Headmaster anazidiwa na Mwalimu wa Darasani. Hakuna mshahara wa Afisa Taaluma, hakuna mshahara wa *Dean of Students,* au marupurupu kidogo ya kuongeza pale, hakuna marupurupu ya Mwalimu wa Darasa hata ukimwondoa kwenye Ualimu wa Darasa anaona afadhali umeniondolea mzigo. Sasa kwa nini tusiwapangepange hawa fedha za *allowance?*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kabisa kama walivyosema wenzangu Serikali inaweza kuweka vitu hivyo. Tunasema tunawapa *TRA* ni kazi gani kubwa *TRA* wanayofanya ana muda wa kusoma kwamba ajiandae Mwalimu muda wote anasoma hawezi kwenda kufundisha hivi hivi bila kurudia kusoma lakini *TRA* anazunguka kwenye duka, amtie makashikashi nyingine anapata anaweka pembeni tunampa mshahara mkubwa. Mimi kwa kweli naomba tujaribu kuwangalia hawa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri suala hili tumekuwa tukizungumza sana naomba isiwe kama wimbo, tulifanyie kazi Serikali iwaangalie Walimu. Kwa nini wasilipwe haki zao wanapokwenda likizo, arrears zimerundikana kwa nini?

Kwa kweli naomba suala hili Mheshimiwa Waziri utupe majibu mazuri, kwa nini? Tunalipa madeni ya nje, unawapa watu wa nje lakini kuna watu wako wananyong'onyea hapa, tuwamegulia basi tupunguze madeni. Kama kuna *DEO* hataki kulipa madeni ya Walimu basi aeleze wazi hizo fedha kama anapewa? Kwa nini fedha za likizo zisipelekwe moja kwa moja kwa ma-*Headmasters* badala ya kusubiri kutoka Wizarani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa kuwa naomba, ngoja nizungumze polepole. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna Mpango wa Sekondari Kuimarisha Elimu ya Sekondari (MMES), naomba waangalie kwanza Wilaya ambazo zimesahaulika hazina Sekondari za Serikali hata moja. Kwa mfano Geita inaongoza katika nchi isipokuwa nafikiri inazidiwa na Temeke ina wanafunzi 145,000 lakini haina hata Sekondari moja ya Serikali ina shule sita inauzidi Mkoa wa Lindi ambao una jumla ya wanafunzi 127,000 inakaribia Mkoa wa Pwani. Sasa anza kuangalia vinginevyo sisi labda tumeandaliwa kuwa vibarua wa sehemu nyingine ukienda sekondari hawapo, ukienda Chuo Kikuu hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba sana katika maandalizi haya jaribu kusaidia sio muwaambie wananchi endeleeni wakati kuna wananchi wale waliokuwa wanachangia kodi zikajengwa Sekondari Dar es Salaam, Moshi, Mbeya katika baadhi ya Wilaya sasa wale wamepumzika sasa hawa wanaambia vuteni soksi, endeleeni, jiunge wakati dhahabu yote inakwenda, tunagawana wote, tuachiene basi dhahabu sisi tujenge muone kama tutashindwa! Aah, nilijisahau nilikuwa naomba nimekuwa mkali lakini naomba tuanze kufikiriwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *BTP,* muundo wa *BTP* ulivyo sasa hivi unanitia wasiwasi. Nia ni nzuri ni kupata Walimu wengi kwa wakati lakini tuangalie tusije tukapata *bogus teachers. Teaching practice* ninavyoamini ndio Ualimu wenyewe kwa sababu ndio kazi anayotakiwa kwenda kuifanya Mwalimu lakini tumewapeleka kule vijijini, nilipewa na mtaalam siku ile tunakutana nikaisoma lakini nikaona bado kuna tatizo, hao Waratibu wameandaliwa kuwa-*assess,* Ma-*DEO* wameandaliwa kuwa-*assess* maana yake wanawashangaa wanakwenda kule?

Je, fedha hizi ziko tayari za kwenda kuwapelekea watu wale, wakufunzi wataweza kufika kule, wameshaanza kwenda, maana yake muda unakwenda? Nadhani kuna haja labda wakitoka kule wapewe *course* kwa ajili ya kwenda kufanya kazi. Naomba waliangalie upya suala hili lengo ni zuri lakini utekelezaji wake ni mgumu. Anayeweza kufanya hivi ni yule ambaye haielewi mtandao wa Tanzania ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Isima ni kijiji kiko pembeni sana Geita huko lakini ule Mto ukifurika hakuna anayekwenda kule wanabaki Walimu na wanakijiji sasa huyu atayekwenda kule ku-*assess* sijui itakuwaje na hizo *record* zitakuwa na usahihi wa namna gani? Mimi nafikiri hili suala la *teaching practice* hebu liangalieni tusije tukapata Walimu ambao kwa kweli hafifu afadhali watumie mwaka mmoja lakini *teaching practice* iwe labda wiki nne wabaki pale pale Chuoni vinginevyo tutakuwa tunajenga kitu cha ajabu. Waratibu wenyewe walishakuwa hoi, Walimu wenyewe wa kuwaa-*assess* na wenyewe wako hoi kule sasa mnawapeleka hawa nao wakajifunze uhoi wa wale watu, ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie inahusu Baraza la Mitihani. Kuna hoja imeletwa na vijana wa Chuo Kikuu ya matriculation. Kijana anapomaliza *Form VI* amepata *Division I* au *II* anaenda kufanya *matriculation* na inafanyika kwa wote unakuta mtu wa *Division* wa *I* au *II* ameachwa. Kuna karatasi hapa nitampa Mheshimiwa Waziri aiangalie lakini sisi tunaamini Baraza la Mitihani nalo linafanya kazi hiyo hiyo huyu amekuwa *screened* vizuri na Baraza la Mitihani kama kuna wizi hiyo ni hoja nyingine kwa sababu hata Chuo Kikuu wizi upo, sisi tumepita pale tunajua kuna maksi sijui za nini, sijui za chupi, za nini sasa watakuwaje wao waaminifu? *(Kicheko)*

Halafu unakuja kumpa mtihani mtu amekaa nyumbani miezi sita huwezi kujua kwamba kuna *validity and reliability* ya mtihani, unajua kwamba huyo amekaa nyumbani inawezekana amekwenda huko kwenye vitocho huko Nyarugusu anaingia kwenye machimbo ya dhahabu kutafuta hela unakuja kumpa *matriculation* akili imesha-*confuse* unamnyima nafasi ya kwenda Chuo Kikuu, wote hawatoki kwenye mazingira ya aina moja. Hiyo *matriculation* tunaweza tukafanya hapa Maprofesa wakashindwa mimi ambaye sio Profesa nikapata, ndivyo ilivyo, twende tukafanye, si ni kutumia akili haraka haraka! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna kuwanyima haki watu wa *Division I* afadhali fanyia basi *Division III* umwangalie kama anaweza. Mimi nafikiri watupe jibu kama haiwezekani basi tuondoe Baraza la Mtihani hakuna haja ya kuwa nalo. Mimi naona hapa tunachanganyana kama ni kutafuta fedha hazitafutwi hivyo. Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie hilo na naingoja Wizara ya Elimu wa Juu kwa kweli kwa hili asipotueleza vizuri taabu ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo napenda nizungumzie ukaguzi. Wakaguzi wanafanya kazi nzuri lakini kuna tatizo moja ambalo nafikiri kuna haja ya kuliangalia. Nadhani sijui kama limesahihishwa bado tunahitaji kuangalia ukubwa wa Wilaya, idadi ya wanafunzi, ndio tuweze kupeleka huduma ya Wakaguzi. Nilikuwa natoa mfano wa

Wilaya ya Geita, Geita ina wanafunzi zaidi ya 145,000 na shule ni nyingi, Mkoa wa Lindi una wanafunzi 127,000 kama ni utaratibu huo wa Wakaguzi watano watano au sita sita Mkoa wa Lindi utakuwa na Wakaguzi 30, Geita itakuwa na Wakaguzi saba au watano tukisaidiwa sasa hivi nimeambiwa ni tisa hata maslahi yataenda hivyo hivyo kwa idadi ya Wakaguzi, nafikiri kuna haja ya kuangalia upya suala hili.

Geita ni Wilaya ni kubwa sehemu nyingine nashindwa kufika Jimbo langu lenyewe ni Wilaya kwa sababu nina zaidi ya watu 300,000 na tuko Wabunge watatu Wakaguzi wanashindwa kufanya kazi zao. Mheshimiwa Waziri niliomba gari tena 110 ukileta nyingine hizi zitakwisha njiani kila siku utakuta wako njiani wanahangaika. Mimi wamekuja kuniomba gari nimekataa ukimpelekea Mkaguzi nakosa kura mimi kwa hiyo wanahangaika sana wapeni Wakaguzi wa Geita gari. Tunaomba katika mpango wako hela ipo naona unayo nyingi sana hapa wasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimwombe Waziri ajitahidi kutafuta namna anafanya vizuri sana lakini ajitahidi kutafuta namna ya kuboresha vijana wenye vipaji katika fani mbalimbali Kitaifa.

Kwa mfano michezo, ni namna gani kwenye *level* ya Kitaifa watajulikana waweze kupata ajira maana yake tumewaacha kule wataishia kwenye Kata, Wilaya wakiunganaungana wengine wamekata tamaa michezo kule juu hakuna namna ya kuwapata wachezaji wazuri na ndio maana tunasema *Taifa Stars* inakufa sasa si tunachagua walevi wachezaji wazuri wako shuleni. Mnasema *Taifa Stars* hakuna wachezaji sasa mnachukua watu hoi mitaani machinga ameshachoka ndio anakuwa mchezaji bora, atacheza wapi? Vijana wenye damu wako shuleni, wako sekondari na tunawanyima nafasi ya kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wafadhiliwa walianza kusema wawaendeleze hiyo fedha imekufa. Sasa tafuteni namna ya kufanya sio lazima wakati vipindi tufanye kama Kenya wakati wa likizo na wakati wa Bunge watu wanafanya vijana wanajulikana. Michezo ni muhimu msiangalie tu wale *bookworms* tu kwamba ndio wanaosoma lazima kuwe na *social activities.* Ndio maana wakati wa *graduation* ukiwanyima *disco* watu wanabondwa mawe kwa sababu ni mchezo kuwe na michezo, shule ipendeze. Sasa hivi ukienda kwenye shule unakuta Walimu wamenuna, wanafunzi wamenuna kila mmoja amebeba kabegi kwenda nyumbani *no activities* zinazowapa uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba michezo inavuruga vipindi lakini kipangwe vizuri haitavuruga vipindi tuangalie Kenya, Nigeria, Uganda wanafanyaje? Juzi tulikuwa na vijana wanamichezo kutoka Uganda wengine wametoka shuleni tayari wameshapata ajira sasa wa kwetu ndio hivyo kwa kweli tunajenga Taifa la watu walionuna hatutafika. Kama *generation* iliyobaki nyuma kama ni *antisocial* ikija huku Bungeni ni ngumu tupu hakuna cha kufikiria kwamba mnaweza mka-*make any joke.* Mtapigana ngumu hapa Wabunge wanaofuata sisi tutakuwa tumeshajiondokea lakini itakuwa ni taabu na ngumi zitalia sijui. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna Idara ya Michezo, sikuizungumza Mkurugenzi wa Michezo, Mkurugenzi omba sasa wewe unafanya nini pale omba upewe na wewe kazi, unafanya nini pale kama haiwezekani nenda ukafundishe lakini Walimu hawana maslahi sijui utafundishaje maisha ni magumu kwa Walimu. Michezo ni elimu, urafiki na afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kujenga misingi ya elimu ya nchi yetu, nawapongeza sana.

Vile vile nawapongeza kwa kuweza kusimamia mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi katika nchi yetu ambao tumeuanzisha na tumeanza kuona matokeo mazuri kwa sababu elimu ya msingi imeanza kuboreka. Nawapa hongera nyingi sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea mambo matatu zaidi kwenye elimu ya msingi, sekondari na mazingira ya kazi ya Mwalimu. Elimu ya msingi ndio msingi mkubwa wa elimu nyingine yoyote iwe ya Sekondari, Chuo Kikuu, Udaktari, Uhasibu.

Kama mwanafunzi hakuwa amepata elimu nzuri ya msingi basi na hiyo elimu nyingine ya juu haitamfaa wala haitakuwa ya maana. Kwa hiyo, elimu ya msingi ndio msingi mkubwa wa kumpatia mtu yeyote msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wa elimu ambao nao wameamini hivyo, naomba kunukuu maneno ya Hayati Mwalimu Nyerere wakati anatunukiwa Shahada ya *Doctorate* katika Chuo Kikuu cha *Open University* cha Dar es Salaam alisema hivi: *"Our education should be of good quality. Primary education in particular should be excellent. Therefore this is the only formal education that most Tanzanians are likely to receive. At present, the quality of Primary School Education is appalling.*

*We must do something about it as a matter of National Agency. A part from the fact that it is the Education of the vast majority , the citizens of Tanzania it is also the foundation of the whole of the education system.* Ndiyo elimu ya msingi, *if it is poor the rest of education system is bound to suffer". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukiipuuza elimu ya msingi hatutafika popote. Kweli Wizara na Serikali imefanya juhudi kubwa sana kuhakikisha wanatimiza maneno ya Hayati Baba wa Taifa lakini nafikiri katika safari yetu tunaweza kupoteza malengo kwa sababu shuleni hasa katika shule za msingi ni mahali pa kumpatia mtoto stadi za elimu na malezi.

Stadi za elimu watoto wanapata, wengi wanamaliza shule wakiwa wadogo miaka 13-14 wanarudi nyumbani kama wametoka chekechea hawawezi kufanya chochote. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu lazima iangalie upya mfumo wetu wa Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani wakati tunasoma *Middle School* tukitoka pale tulikuwa tunaweza kuajiriwa ni watu wazima lakini watoto wanaomaliza darasa la saba sasa hivi hawana uwezo kabisa. Anarudi nyumbani hajui hata kufuga mbuzi, hajui hata kukamua ng'ombe, hajui hata kulima na huyu amemaliza elimu ya msingi ikamsaidie nini nyumbani kwake?

Wizara ya Elimu inatakiwa ianze ku-*address* tatizo hili kwa kubadilisha mfumo wa elimu. Ninafikiri tungerudisha darasa la tisa na la kumi katika Shule za Msingi tukawa na system ya miaka tisa, mitatu, mitatu ingeweza kusaidia misingi yetu ya elimu ya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwenda ku-*overhaul* mitaala yetu. Sasa hivi dunia nzima imebadilika kuna *globalization* imeingia na sio kwamba iko hewani iko ndani ya watu na watoto wetu hao wanaosoma watapambana na hii *globalization* kwa njia moja au nyingine.

Kwa hiyo, kuna kila sababu ya kubadilisha *curriculum* ili iwe ya kumpa mtoto *skills* za kuweza kuishi maisha ambayo ataweza kuwa katika hali ya ushindani na vijana wengine katika Taifa ama Mataifa mengine. Tatu ni elimu ya kujitegemea *(education for self-reliance)* siku hizi haiongelewi imewekwa kwenye *shelf* Hayati Baba wa Taifa ameandika vizuri sana *what is wrong with* elimu ya kujitegemea?

Sisi wote tulioko hapa tumekuja kwa misingi hiyo ya elimu ya kujitegemea. Sasa hata Wizara ya Elimu ime-*abandon* elimu ya kujitegemea, watoto wanatakiwa wajue dhana ya elimu ya kujitegemea wakimaliza elimu yao ya msingi hiyo ya miaka tisa niliyopendekeza wakirudi katika maisha yao kijijini wataweza kuchangia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, katika elimu ya msingi pamoja na elimu nyingine kama vile sekondari na wapi ni michezo ambayo imezungumziwa na Mheshimiwa aliyepita. Vijana wana nguvu sana na hizi nguvu zisipokuwa utilized vizuri watajiingiza katika vitendo vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana moja ya malezi ni kuwapa vijana shughuli kuanzia asubuhi mpaka jioni ikifika jioni kamechoka kanalala.

Lakini kama hakakucheza, hakakufanya kazi za mikono ikifika jioni bado kanafikiria mambo ya utundu utundu tu ndio maana watoto wa shule za msingi wameingia katika masuala mengi ambayo sio ya rika lao. Wanaanza kujifunza picha za ajabu, picha za *phonograph,* wanaanza kufahamu vitu vya namna hii kwa sababu vijana muda wao haujatumika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wacheze kwa muda wote waingie katika mashindano na ili michezo inoge lazima kuwe na mashindano ya watoto kwa watoto, wanafunzi kwa wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema kama akili inakaa tu bila kufanya *activity* nyingine, yaani kazi yake ni kusoma tu, inaishia kuwa ni *copycat,* siyo akili ya kuweza kufikiri na kubuni kitu. Sasa ili akili ya mwanadamu iweze kubuni kitu inahitaji kufanya *activities* zingine na ma-*genius* wote duniani wanafanya mambo mengi sana, hawafanyi kitu kimoja. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri hilo aliangalie katika mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwenye elimu ya sekondari. Wazazi wengi hawawezi kulipa na watoto wengi hawaendi shule kuna *drop out* kubwa. Sasa hivi shule unakuta darasa moja lina wanafunzi kumi na tano, ishirini au thelathini badala ya wanafunzi arobaini kwa sababu wazazi wengi wameshindwa. Karo ya shule ya kutwa hizi tulizojenga za wananchi ni shilingi 140,000/= au 150,000/=. Sasa na mahitaji mengine madogo madogo inafika karibu shilingi 200,000/=, wazazi wengi hawawezi. Wizara ifikirie na kuishawishi Serikali. Kama Serikali imeweza kufuta kodi ya maendeleo basi inaweza kufuta na karo ya shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama pia Serikali yetu hiyo hiyo imetamka ikafuta karo ya shule za msingi inaweza vile vile ikaamua kufuta karo ya shule za sekondari. Tunaomba Serikali ilifikirie hili kwa uzito mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika hizi shule zinazoitwa za wananchi, maana yake zinajengwa kwa nguvu za wananchi, ni *Community School,* lakini *how much* Wizara inaweka sera ya kuishirikisha *community* katika ujenzi wa ile shule? Ni kitu ambacho ni *questionable.* Shule ile inajengwa na wananchi katika Kata ama katika Tarafa, lakini viongozi ambao wanawakilisha wananchi katika Tarafa au Kata hawahusishwi na uendeshaji wa shule. Wananchi hawajui shule inavyoendeshwa wala mahitaji ya shule, kwa hiyo shule inakuwa kama inategemea uongozi wa *one man show off.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo Mheshimiwa Waziri ningeomba aliangalie ni kuhusu shule za kutwa ambazo zilianzishwa katika shule za bweni kwa mikondo ya kutwa. Kule kwangu najua kuna shule moja na kule Umbwe ipo moja. Same Sekondari walikuwa na shule ya kutwa, waliruhusiwa na Wizara kwa kibali chenye Kumb. Na. EDS/A1/63/VOL II/233 cha tarehe 23/8/1993 waanzishe shule ya kutwa. Wananchi wakachanga fedha zao, akina mama wakabeba mchanga kwa vichwa vyao, akina baba wakakusanya mawe, wakajenga vyumba nane vya madarasa, jengo moja la maabara na chumba kimoja cha ofisi ya walimu. Pia wakachangia kwa fedha zao madawati mia moja na sitini. Mwaka huu wakaambiwa ndiyo mwisho watoto wenu wasisome hapa, watafute mahali pengine. Sawa ni sera ya Serikali kwamba huwezi kuchukua watoto wanaopishana kwa alama, kimisingi ya ualimu ni kweli, lakini Wizara hiyo hiyo ndiyo iliyowaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa kukubali kwamba atawafidia wananchi lakini how fast? Ndiyo maana imebidi niliongee leo kwa sababu wananchi kule wanalalamika sana kwamba wao wamechangia majengo hayo na Wizara imeahidi itarejesha hayo majengo kwao. Sasa wameshapata eneo la kujenga shule yao, tunaomba Wizara iwafidie. Isiwe hiyo shule ya Same sekondari na Umbwe peke yake na kote kwingineko kama Arusha na kadhalika warejeshewe, vinginevyo tutaleta mgogoro na wananchi. Naomba Wizara ilizingatie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu kabla muda haujanitupa mkono, ni kuhusu hizi shule za wananchi za mashirika ambazo ni za binafsi kama zile za wazazi. Zamani walikuwa wanakwenda kwa wafadhili na mashirika mengi mengi ambayo Mheshimiwa Waziri ameyashukuru hapa. Siku hizi wanasema pesa zote za misaada na maendeleo tumepeleka Serikalini, kwa hiyo mkaombe Wizara ya Elimu. Lakini katika bajeti ya Wizara sijaona sehemu ambapo ametaja mahali ambapo Serikali inatoa ruzuku kwa hizi shule za wananchi na za watu binafsi, ni kwa sababu gani? Watoto wanaosoma katika hizo shule ni watoto wa Taifa hili hili la Tanzania. Sasa Serikali inapochukua misaada ya nje ikapeleka upande mmoja tu, ni kuwafanyia vibaya watoto ambao nao wana haki hiyo hiyo. Tunaomba Wizara ibadilishe sera yake hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu walimu. Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu kweli. Mwalimu anampa Waziri elimu, anampa daktari elimu na pia anampa Mhandisi elimu, halafu yeye anabaki hohehahe, hii si halali. Sasa tunataka walimu wakaangaliwe kwa upande mwingine, ukimkuta mhasibu mzuri kafundishwa na mwalimu au aliyetengeneza hiki kiti kafundishwa na mwalimu. Sasa huyu mwalimu kwa nini hapewi nafasi yake anayostahili. Juzi Serikali imeuza nyumba, walimu wanauliza hizi nyumba zimeuzwa kwa nini hata mwalimu mmoja hakuuziwa? Sasa labda walimu hawana maana katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakasema zile nyumba zipo katika mazingira ya shule, hata hizo zilizouzwa za Serikali zilikuwa katika mazingira ya Serikali. Mimi naishauri Serikali itafute njia ya kutafuta chombo cha kuwakopesha walimu fedha wakajenge nyumba. Walimu wakifikia muda wa kustaafu wasistaafu bila kuwa na mahali pa kukaa. Awe ni mwalimu wa kufundisha darasani, awe ni mwalimu wa kupiga siasa kama mimi ama kufanya kazi ya utendaji ofisini, basi apate mkopo wa nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu mishahara. Mishahara ya walimu kwa kweli ni midogo. Mimi nasema walimu wanapunjwa, *Karl Marx* alikuwa anasema *they are paid less than the necessary labour time.* Mwalimu anafanya kazi wakati wote, sisi tunafanya kazi masaa saba kwa siku kwa sheria ya nchi, baada ya hapo tunarudi nyumbani. Mwalimu akitoka shuleni anakwenda kusahihisha na kutayarisha somo la kesho, muda wake wa kupumzika ni mdogo na kwa sababu walimu wamejua kwamba wanapunjwa na wenyewe wameamua kuipunja Serikali. Kwa hiyo, wanauza vitumbua, wanashona vitambaa, wanafanya miradi yao, wanalima bustani, kwa hiyo watoto wetu hawafundishwi vizuri. Kama tunawapunja nao wanatupunja, kwa hiyo tutafikia kubaya. Tuangalie kwamba walimu wanatumia muda mwingi katika kazi za kuwasomesha watoto wetu ili watoto wetu waweze kupata elimu nzuri na hatimaye tuwe na Taifa zuri ambalo litakuwa na watu wenye elimu ya maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo hatima yake thamani na ubora wa elimu utashuka mno, siku moja tutakuwa na Rais aliyechoka kwenye akili. Kulikuwa na baba mmoja ananiambia, mwanangu, kheri ukakosa elimu ya vitabu kwa asilimia arobaini lakini usije ukakosa elimu ya malezi. Kwa sababu elimu ya malezi ndiyo msingi mkubwa. Ukimtafuta Rais mzuri lazima tuangalie ana matashi gani, Mbunge mzuri lazima tukaangalie, Mkuu wa Mkoa lazima tukaangalie. Kwa hiyo, ili walimu wafanye kazi zote mbili ya kutoa elimu ya vitabuni na elimu ya malezi *they need enough time and good pay.* Huwezi kumtengeneza mtu akawa na tabia kama za Hayati Baba wa Taifa kienyeji tu, hapatikani hivi hivi, anatayarishwa na kujengwa na kama tunataka hivyo basi tuwape hiyo haki yao walimu.

Mwisho ni kuhusu *terminal benefits* za walimu. *Terminal benefits* za walimu zimetajwa katika taratibu zao za ajira. Sasa walimu hao wanapostaafu na kurudi nyumbani wakapewa ile *package* yao wanapewa wakati wameshachoka. Hata kutumia hiyo fedha yake vizuri hawezi, amechoka. Tungefikiri Serikali ingeweka utaratibu mpya wa kufikia umri fulani apewe, halafu akimaliza apewe, iwe mikupuo miwili. Kama umri ni miaka thelathini ya utumishi, basi akifanya nusu miaka kumi na mitano apewe. Naambiwa hapa sitini ni mingi sana na umri umeshashuka mpaka arobaini na tisa kwa sababu ya haya matatizo ya magonjwa sugu. Kwa hiyo, walimu wengi watapoteza fedha zao, kwa hiyo anapokuwa na nusu ya umri wa utumishi apewe na anapomaliza apewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nampongeza Waziri na naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ili kuzungumzia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa nitamke wazi kwamba naiunga mkono hoja hii.

Ni hoja ambayo imeandikwa vizuri, imeonyesha takwimu za kutosha na imetoa malengo ambayo kwa hali yoyote kadri uchumi wa nchi yetu unavyoendelea ni malengo ambayo yanatekelezeka. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuliongoza hili jahazi akisaidiwa na wasaidizi wake Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye tunamwombea afya njema haraka inavyowezekana, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wengine. Ni kweli kabisa kwamba katika Wizara ambazo zimeonyesha uwezo wa Uaskari wa Miavuli basi na Wizara ya Elimu nayo imeweza kutuonyesha kwamba inaweza kitu katika kipindi hiki cha miaka mitano. Pamoja na yote hayo kwa uwezo uliopo napenda kusema kwamba huu ni mwanzo na mengi yalipo mbele yetu kuweza kufanya elimu iboreke. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wanayo nafasi ya kusikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge hapa, walimu wenyewe waliopo huko Vijijini wanaofanya kazi na umma ambao unawazaa watoto wao ili waweze kuelimika na baadaye kuwa viongozi wa baadaye kwa nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumzie tatizo la nyumba kwa ngazi zote za elimu; elimu ya msingi na elimu ya sekondari, sielewi sana kuhusu Vyuo Vikuu, hali

ya makazi ya walimu ni mbaya sana. Walimu sehemu zote hawana nyumba. Tumejaribu kuboresha kujenga madarasa na vyoo lakini upo uwezekano mkubwa wa wastani wa shule ya msingi kuwa na walimu wanane, lakini hakuna nyumba ya mwalimu hata moja. Mwalimu huyu analazimika asafiri kilomita tano, sita, saba, nane au tisa.

Namkaribisha Mheshimiwa Waziri aje Ngara nitampeleka kwenye shule moja inaitwa Kigina ambako mwalimu wake mmoja anatembea kilomita kumi na tatu kwenda kufundisha na kurudi nyumbani kwa sababu hakuna nyumba. Kwa hiyo, katika kuboresha elimu na kwa kuwa elimu ya msingi kama lilivyo neno msingi ndiyo chanzo cha elimu nyingine zinazofuata, ni dhahiri kwamba wito wa kujenga nyumba kwa sababu ya walimu lazima uwe mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wanaokaa Vijijini wanayajua maisha ya walimu. Unaweza ukafika shuleni, ukamtafuta mwalimu katikati ya wanafunzi mahali pengine ukakuta kwamba mwanafunzi ana hali nzuri kiusafi kuliko mwalimu. Walimu viatu vinawaishia haraka haraka kwa sababu ya kuchuja umande katika safari ndefu. Walimu nguo ni chafu kiasi cha kwamba ni vigumu kumwambia mwanafunzi akafue nguo, walimu wana hali mbaya kwa sababu wanatoka katika mazingira ambayo ni mazito. Mahali pengine wanakodi nyumba ambazo kwa kweli si sawa na za wakimbizi wa Rwanda na Burundi waliopo katika Wilaya ya Ngara. Kwa hiyo mimi nasema suala hili ni zito na linawakatisha tamaa walimu, walimu wengine wanazikataa *transfer* kwa sababu hawana mahali pa kukaa na shule nyingine zinakosa walimu wa kutosha kwa sababu hakuna mahali ambapo wanaweza wakakaa. Walimu walio na unafuu kidogo ni walimu walio katika maeneo ambayo ni karibu na Miji wanaweza wakakodi vijumba vijumba katika Miji na vitu kama hivyo, lakini mahali pengine kwa kweli walimu wana shida kubwa sana. Kwa hiyo mimi naomba Wizara itazame kwa sababi hiki ni chanzo kikubwa cha kushuka kwa elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa sekondari. Mimi sielewi, hivi kweli Serikali ya nchi hii, Serikali ya CCM, inaridhika kuona kuna Wilaya moja ina sekondari ishirini lakini nyingine haina hata moja? Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa maelezo aliambie Bunge hili kwa nini? Tunalipa kodi wote, wakati wa mkoloni tulikuwa tukilipa kodi wote, tunachangia Mfuko wa mapato ya Taifa kwa pamoja. Leo Wilaya moja ina shule ishirini au thelathini za sekondari lakini kuna Wilaya haina hata shule moja ya sekondari. Kama ni kukombolewa basi inakombolewa na shule za watu binafsi na shule hizi gharama zake tunazijua, wenzangu wamejaribu kusema. Mkulima wa kawaida wa Kijijini anayeshindwa kulipa kodi ya maendeleo ambayo imelazimika kufutwa kwa sababu imekuwa ni kero, atawezaje kumwingiza mtoto wake katika shule ya namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba sasa utoke utaratibu mahususi wa kugawa elimu ya Sekondari tuache utaratibu huu wa sasa, hii ni historia ya wakoloni. Wakoloni walikuwa wanajenga shule za sekondari karibu na Makao Makuu ya Mkoa, Wamisionari waliokuja walikuwa wanajenga shule mahali pale ambapo wameona kwamba ni pazuri. Kwa kuwa inafuatana na historia ya uvumbuzi utakuta sasa hivi maendeleo kielimu ndiyo maendeleo hata kiuchumi na hata kiustaarabu. Katika nchi yetu haya yameanzia Kaskazini, yakafika sehemu za Pwani, yakakata yakafuata barabara kuu yako Kusini Milimani, sehemu nyingine zimesahaulika kabisa. Unakwenda katika

Wilaya unakuta hakuna sekondari hata moja, leo! Mimi naomba Serikali ibadilishe sera hii sasa, ni Serikali ya CCM, ni Serikali iliyochaguliwa na watu na ni Serikali iliyo na lugha moja tu ya Kiswahili katika kuwaendeleza wananchi wake wote. Ninafahamu Wilaya ambazo katika mitihani ya kumaliza darasa la saba mtoto aliye na alama chini ya hamsini kwa sababu ya sekondari nyingi anaweza kwenda sekondari. Pia nafahamu kabisa Wilaya ambazo mtoto aliye na alama zaidi ya mia moja anashinda lakini anakosa mahali pa kwenda, kwa hiyo anabaki Kijijini. *(Makofi)*

Nitoe mfano, mwaka jana mwaka wa 2002 Wilaya ya Ngara ilikuwa na watahiniwa 1,622. Watahiniwa 1,406 walishinda kuanzia alama sitini kwenda mpaka 130, waliochaguliwa ni 318, waliobaki ni 1,088 ambao wapo Kijijini kwa sababu hakuna sekondari. Katika uboreshaji wa majengo ya *Primary school* sasa hivi kama kuna watu wamepata shida kuweza kuhamasisha wazazi kujenga, nashukuru wamejenga, ni Wilaya ya Ngara. Viongozi tunapita mahali tunataka kutupiwa mawe kwa sababu ya watoto 1,088 ambao wapo Vijijini. Watoto hawa kuna wenye alama mpaka 115 juu ya 150, hawa ni ma-*genius* na wapo Kijijini, hawa ndiyo watatengeneza bunduki kutumaliza maana wamekosa mahali pa kwenda. Pia ndiyo watakaoanza sasa kuvuta bangi kwa sababu wamekosa mahali pa kwenda. Wazazi wanakata tamaa, viongozi wanakata tamaa, watoto wanalia, Serikali inasemaje au inafanya nini kuondoa adha hii kubwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiomba Serikali ilitazame hili. Ifanye utafiti wa kutosha kuona Wilaya ambazo hazina sekondari zipewe sekondari. Wilaya ya Ngara ina sekondari moja ambayo sasa inaonekana kuwa inafanya kazi. Zipo mbili ambazo ndiyo zinaanza kujengwa na zipo nyingine zinapangwa lakini zipo nyingine ambazo ni za watu binafsi na gharama yake ni kuanzia shilingi 300,000/= kwenda juu. Hakuna mtoto wa mkubwa anayeingia pale. Wwanaosoma ni wanaotoka nje wenye uwezo wa uchumi. Mzigo huu ni mzito sana na Serikali inapaswa itazame kwamba sasa umefika wakati pato la Taifa tugawane. Marehemu Baba wa Taifa alitamka akasema: “Maskini hugawana umaskini wao wanapokuwa wakiendeleza ujamaa wao”. Sisi Watanzania tuendeleze huo ujamaa wetu kwa kugawana pato linalopatikana ili wote tuweze kulingana. Jambo hili ni zito sana na linasumbua, kwa kweli linaleta matatizo, na umma wa Tanzania hawaridhiki na mgawanyo huo. Pili ni tatizo kubwa sana ambalo sasa linajitokeza katika shughuli zetu baada ya wingi wa sekondari ambalo ni ada. Mimi naomba Serikali ifikirie kwamba njia mbili hizi zitafutiwe dawa, kwanza ni shule za binafsi zifikiriwe kupewa ruzuku kama vile tunavyofanya katika Wizara ya Afya na mahali pengine na miongozo ionyeshe kwamba kwa kuwa zile shule za binafsi zipo katika maeneo fulani ambako hakuna shule za wananchi wala za Serikali basi wale ambao wamepata alama za kutosha kuwaingiza sekondari wanaweza kupata nafasi ya kusoma pale. Hapa naomba kuishukuru Serikali na Wizara iliyoweza kutoa ushauri huo wa Serikali kwa hizi bilioni moja nukta moja zilizotoka kwenda kuwasaidia wale walioshinda lakini wakashindwa kujiunga na sekondari, imesaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa mwaka unaokuja akifanyakiasi cha msaada huo mara mbili au tatu kiasi cha idadi ya wanafunzi ambao wamebaki vijijini ambao nimewaeleza kwa mfano Ngara mimi

naamini kwamba inaweza ikasaidia. Katika 1,088 watoto waliofanikiwa kupata nafasi ni 32 tu. Kwa hiyo, 1,056 bado wapo nyumbani na wanalalamika. Kwa hiyo, huu Mfuko mimi naomba kabisa uongezwe na bado hili suala la kutoa ruzuku kwa shule za watu binafsi ambao wanafanya kazi nzuri sana liweze kufikiriwa kusudi watoto wetu wasome. Lingine linalodidimiza elimu wengi wamelizungumzia ni mishahara. Walimu wetu wanapata matatizo makubwa sana. Walimu wetu hawana hata uwezo wa kuweza kujiwekea akiba katika mabenki yetu yaliyopo. Wengine wanashindwa hata kuingia katika nafasi hizi za Vyama vya Kuweka na Kukopa kwa sababu mshahara ni mdogo sana. Walimu wetu wengi kama wananchi wote wa Tanzania walivyo, familia zao ni kubwa. Unamkuta mtu anatoka katika familia ya watu kumi na tano au ishirini badala ya kuita kwamba ni jamii inakuwa ni jamaa, wote wanamtazama yeye. Sasa Mheshimiwa Naibu Spika, mwalimu amefanya kazi kwa miaka ishirini au ishirini na mitano, bado anapata shilingi 72,000/= ni kitu cha kutisha sana. Hivi tunafikiri atafanya kazi gani? Mwalimu huyo ana watoto wawili au watatu wapo sekondari na watoto wawili wapo *primary,* ana mama ni mzee, ana baba ni mzee na pia ana ndugu wanaomtegemea, matokeo yake unamkuta anaanza kutumbukia katika kula madeni. Mwishoni mwa mwezi unakuta anabadili duka ambako alikuwa akikopa chakula anakwenda duka lingine. Walimu wetu wanapata shida sana. Mimi naomba Serikali ifikirie kuongeza mishahara na kuongeza mishahara kweli kwa sababu ya watu hawa ili mradi pato la Taifa limekuwa basi nafikiri lianzie kwa hawa ambao watatupa nafasi ya kuendelea kulikuza zaidi kwa kutumia teknolojia ambayo tutakuwa tumeipata kutoka kwao. Umaskini utafutika nchini, walimu wakiridhika na kufanya kazi vizuri wakiwa wametulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie kuhusu ujenzi wa mabweni katika sehemu ambazo shule za sekondari ni chache. Ujenzi wa mabweni katika maeneo ambapo wakazi wake ni watu wa kuhamahama, unaleta shida kwa kweli.

Katika maeneo ambapo shule za sekondari ni chache kama nilivyokuwa nimetangulia kusema. Watoto wanahangaika, wanatembea masafa marefu mno, wanalala popote pale wanapofika na wanaoathirika zaidi ni watoto wa kike. Watoto wa kike sasa wanapata mimba ovyo ovyo kila mahali. Watoto wa kike wanateseka, imefikia mahali wanaacha masomo. Watoto wa kiume masomo yao hawayakamilishi kwa sababu *syllabus* hawawezi kuzi-*cover,* wakati mwingine mtoto anafika shuleni saa tatu au nne vipindi viwili au vitatu vimekwisha kwa sababu ametembea safari ndefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano, kwa mfano Wilayani Ngara kuna sekondari moja ya Muyanzi inasimamia Tarafa mbili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri na pia namtakia maendeleo mazuri ya afya yake Naibu Waziri Mheshimiwa Sakila. Ningependa kuchangia kwenye maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kwanza ni minong'ono ambayo niliisikia wakati fulani kwamba Serikali inatazamia kufanya baadhi ya Vyuo vya Elimu kuwa *Associated Universities* kwa mfano Chuo cha Chang'ombe na vinginevyo. Nimepitia kwenye hiki kitabu cha hotuba sijaona lolote ambalo limezungumziwa kuhusu suala hilo. Ningependa kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri hili ni kweli na kama ndivyo suala hilo lingetazamiwa kutokea wakati gani? Kwa sababu kwenye Bajeti hii naona kabisa suala hilo halipo. Pili na linalofanana nalo ni Chuo ambacho kipo kwenye Jimbo langu Chuo cha Patandi cha *Special Education* kwa ndugu ambao pia ni maalum. Chuo cha Patandi ni Chuo ambacho kidogo ni *unique* lakini kwa bahati mbaya kimesahaulika kwa muda mrefu kwa kupata *allocation* za Bajeti ambazo hazitoshelezi, kwa hiyo kina matatizo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kina tatizo sugu la majengo. Majengo hayatoshelezi mara nyingi wanachukua wanafunzi wachache kuliko ambavyo wangestahili kuchukua au wangependelea kuchukua na wanatumia, kwa mfano sasa hivi, wanatumia jengo ambalo ni la vyombo vya useremala na ndilo wanalotumia pia kwa kufundishia kwa kweli inawapa matatizo. Wanatumia Maktaba kwa kufundishia na pia kwa shughuli za Maktaba. Majengo mengine wanayatumia kiajabu ajabu lakini ni kwa ajili ya ukosefu wa majengo.

Pili, *Operating Budget* yao na hasa kwa ajili ya shughuli za *field attachment* imekuwa ndogo kwa muda mrefu. Nakumbuka mara nyingi wanatuita tuwasaidie kufanya harambee ili wanafunzi wao wanapofikia kipindi cha kwenda kwenye *field attachment* waweze kujipatia fedha kidogo ya kwenda kujimudu kwenye *field attachment.* Lakini kwa bahati mbaya Wizara haionyeshi kwamba inawajali sana. Tatu, Chuo chenyewe kimezungukwa na soko kubwa, soko la Tengeru na pia jamii. Kuna eneo la shule ya msingi, jamii iliyozunguka hicho Chuo haina *fencing,* inahitaji hiyo *fencing* kwa muda mrefu, bahati mbaya hawajaweza kupata bajeti ya kuweza ku-fence eneo la Chuo ili kulinda mali ya Chuo na mali ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Wizara tungependa tuwaombe mzingatie hayo mahitaji ya hicho Chuo ambacho kipo kwenye Jimbo langu. Nipende tu kuwapa sifa kwamba ni watu ambao wanashirikiana vizuri sana na jamii inayowazunguka, wanapendwa na watu, tunawapenda, ni washirikishi na tunapenda kuwashirikisha pia kwenye maendeleo ya Arumeru Mashariki na Arumeru nzima.

Kwa hiyo, tungependa Serikali iwajali kuwasaidia kutatua matatizo ambayo wanayo na yanayowakwamisha kwenye kuendeleza Taifa letu kwenye hii fani ya elimu kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Elimu ya Sekondari. Hili nadhani limeishazungumziwa kwa kiasi kikubwa na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia. Na suala kubwa ni gharama ya Elimu ya Sekondari na hasa katika

Sekondari za Jamii. Kama ilivyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia na mmoja akatoa uchambuzi mzuri sana sina haja ya kuurudia. Lakini kwenye Jimbo langu kwa mfano, gharama zilizotolewa za 120,000/= kwangu zinakaribia 220,000/=. Ombi langu kwa Wizara ni kwamba watembelee hizi Sekondari wakaone *structure* ya hizi gharama. Shida kubwa watu wanacholia siyo hizi shilingi 40,000/= kwa zile Sekondari ambazo ni za kutwa,shida siyo hiyo. Shida ni hizi gharama za ziada ambazo zinakaribia 100,000/= kwa mwaka na kuendelea. Kwa mfano, ukiwa katika Kata ambayo haina Sekondari na kwa hiyo lazima uende Sekondari ambayo ipo Kata ya jirani, unalipa ziada eti kwa vile Sekondari haipo kwenye Kata yako. Huo ni mpango ambao jamii imejiwekea si mbaya kwa kweli ambao unatoa hamasa kwa Kata ambayo lazima itafute elimu kwenye Kata nyingine ili nao pia watafute Sekondari yao. Lakini inaongeza gharama na kwa kweli hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye *drop out* za wale ambao wanachaguliwa kuingia *form one,* lakini baada ya mwaka mmoja hawajiwezi tena kuendelea kumudu hizo gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sera ambayo imekuwepo kwamba kila Kata iwe na Sekondari, nimeona kwenye maandishi fulani fulani na kwenye makabrasha fulani fulani ya Wizara kwamba kuanzia sasa vigezo vya Wizara vitafuatwa *to the letter* na nina imani inazungumziwa pia kwamba wale ambao wameishaanzisha na zikapita kwenye utaratibu wa urasimu wa Wizara huenda isiwe tena rahisi. Tunafahamu waziwazi kwamba ni Ilani ya CCM kwamba kila Kata lazima iwe na Sekondari na wengi wanafanya jitihada kwa njia zote ili wapate Shule ya Sekondari, na wanajitahidi kujijengea Sekondari kwa ajili ya watoto wao na kwa ajili ya Taifa. Vigezo vingi ambavyo vinahitajika ili Shule ya Sekondari iweze kuandikishwa kama shule ya Sekondari, kwa mfano, kuwa na nyumba saba za walimu na vigezo vingine ambavyo ni majengo yanayohitajika katika shule ya sekondari ili iandikishwe kama shule ya Sekondari kwa kweli ni jamii ndogo ndogo ambazo zitaweza kumudu hizo gharama.

Mheshimiwa Spika, lakini nashukuru kwamba MMES huenda ita-*address* hili suala. Tunaomba pia Wizara itusaidie kwenye hili itazame kila jamii *on a case by case basis.* Kuna sehemu nyingine ambapo kwa kweli ukiwa *strict* sana, na tunaomba tuwashukuru sana Wizara kwamba wamejitahidi kwa kiasi kikubwa kutazama hili suala *on a case by case basis.*

Vinginevyo kwa kweli ukiwa *strict* sana itakuwa vigumu kwa sehemu zingine kuweza kupata shule ya sekondari. Tunaomba muendelee kutuvumilia kama vile nasi tunavyowavumilia kwenye maeneo mengi. Mtuvumilie na mtusaidie tuweze kuvuka vigezo ambavyo tusingeweza vinginevyo kama isingekuwa kwa huruma yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye malengo tuliojiwekea ambayo yametokea kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 3 na wa 4 . Ukurasa wa 4 kwenye malengo maalum ya Elimu ya Sekondari lengo la tatu linalozungumzia ni kuboresha Elimu ya Sekondari kwa kuongeza asilimia ya wanaofaulu mitihani ya Kitaifa ya Kidato cha nne na cha Sita katika madaraja moja, mbili tatu, kutoka asilimia 25 mwaka 2001 hadi zaidi ya asilimia 50 ifikapo mwaka 2003, hapo nina imani una maana ya mwaka 2005, mimi nadhani ni lengo nzuri. Lakini kwa muda huu uliobakia mimi inanipa wasiwasi kwamba hili kidogo litafikiwa kwa miaka mingine miwili ijayo. Na kwa sasa

hivi liko kwenye asilimia 36.2. Lakini ni vizuri kuwa na lengo hili ili tuweze ku-*struggle* kulifikia. Mimi naipongeza Wizara maana yake kwa kweli wanaweka malengo na wanayafikia. Kwa hiyo, nina imani huenda tutalifikia japo kidogo linaonekana ni ambitious. Lakini najiuliza tukifikia hilo lengo la asilimia 50. Linanifanya nijiulize pia swali lingine kwamba *capacity* ya *form fiv*e na *form six* ikoje, na sijaiona kwenye takwimu ambazo tumepewa. Sijaona *capacity* ikoje je, itatosheleza hii, ipo ya kupokea hii ziada inayoweza ikajitokeza na kufikiwa kwa hili lengo la asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo inanipa basi kupendekeza yafuatayo kwenye Mpango wa Kuendeleza Elimu ya Sekondari kama ambavyo huenda ikatokea na tungependa itokee. Kutazama maeneo mawili. Eneo la kwanza, ni kutazama eneo la kujenga mabweni katika shule za sekondari ambazo zipo na zimejengwa kwa maana ya kuwa sekondari za kutwa, na hasa kuna njia mbili kwenye hili. Kwanza, kujenga shule ya sekondari moja kwa moja kwa wanafunzi waweze kuwa na hosteli capacity katika *secondary schools* ambazo ni za kutwa. Pili, kupanua *capacity* ya *High School* yaani darasa la 13 na darasa la 14 katika sekondari ambazo ziko tayari yaani ku-*expand* kuanzia *form four* na kuendelea, hiyo itatusaidia sana. Kwa sababu kwenye *drop out rate* japo haijazungumzwa sana suala la *drop out rate* kwenye *secondary school level,* nina imani kwamba ni kubwa na ni kubwa kwa sababu tatu kubwa. Kwanza, malipo, pili watu kwenda katika sehemu za migodi, kwa mfano kwenye Jimbo langu, tatu ni umbali wa shule za kutwa kutoka nyumbani kwa wanafunzi, wengine husafiri wastani kilomita 9 mpaka 15 kwenda na kurudi kutoka shuleni ni shule za kutwa hizo. Na hasa kwa wanafunzi wa kike kwenda na kurudi umbali huo unawafanya wakati mwingine wanakata tamaa na ku-*drop out* kabla ya kumalizia masomo yao. Kwa hiyo, tungeomba Wizara itazama hilo suala kwa kutusaidia pia kupunguza *drop out rate* katika *secondary school level* kwa kujenga hosteli *capacity* na kupanua kutoka *O- level* kwenda kwenye *High level. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kama nina dakika moja pale ni kuhusu makato ya mishahara ya walimu. Wakati mwingine inatokea kwenye ngazi zetu za Halmashauri na wakati mwingine inatokea kwenye ngazi nyingine. Lakini naona hili na wiki iliyopita nilipita mahali nikaona *notice* tu kwamba "mtakatwa Shilingi" kadhaa kwa ajili ya shughuli fulani kwa mfano, Mwenge. Lakini makato ya bila ridhaa ya mtu, ridhaa ya muajiriwa limekuwa ni jambo la kawaida. Walimu wengi wamekuwa wakinijia Jimboni kulalamika juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi nichangie. Awali ya yote kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba kama Kaimu Katibu Mkuu wa *UDP* na Mbunge Viti Maalum kupitia Chama hicho hicho nampongeza Mheshimiwa Isaac Cheyo kwa kushinda kesi yake leo, na nawaambia waliokuwa wanakitani kiti hicho walie tu. *(Makofi)*

Vile vile napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa yote aliyoyasema leo. Kwa kweli amesema vitu vya uhakika. Lakini kuna watu ambao tunahitaji kuelimishwa vile vile kwa sababu tumesoma, lakini hatujaelimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuelimika maana yake ni kutumia elimu uliyoipata kwa vitendo. Utakuta wote tunachanganya hapa tuna tunafikiri kwamba sisi wote ni watawala eti kwa sababu wanatoka kwenye Chama kinachotuongoza. Kwa kweli elimu hiyo naiomba Wizara ya Elimu na Utamaduni itusaidie kutuelimisha zaidi tofauti ya utawala na watawaliwa, tofauti ya wawakilishi ambao sisi Wabunge ili tujue tunaowawakilisha wananchi humu ndani ya Bunge na si watawala. Watawala ni Mawaziri crime ya Wabunge.

Vilevile katika Kanuni na Katiba kuna *Shadow Ministers* ambao na wenyewe Kanuni inawatambua na Katiba inawatambua wanatakiwa kupewa muda zaidi wa kuzungumza hapa ndani ya Bunge kwa utaratibu uliowekwa na Sheria. Sasa lazima tuheshimiane tunapozungumza, tusidharauliane, tukaambiana kwamba watu hawakusoma Katiba, hawakusoma sijui habari zilizopita juzi, labda *last week, last year* wamekuja hapa wapya. La hasha.! Wamesoma na wanaelewa wanachofanya. Tusipate nafasi ya kuzungumza huku ndani ili mradi kusema tu usikilizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie katika habari yenyewe. Mimi nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu elimu. Elimu ni haki ya mtoto kama ukiangalia vizuri nimekuwa Waziri ninaye subiri kwa Wizara hii kwa muda wa miaka 7. Nimezungumzia masuala ya haki ya mtoto na elimu na mpaka nikaomba sizungumzii ugoro, unaweza ukasoma *hansard* ukaona, kwa nini tutwange maji kwenye kinu na hali haki ipo pale nendeni mkasome *hansard* mtaona ninayozungumza ni ya kweli. Ndiyo maana nimesem tunahitaji sisi wenyewe elimu kwanza na elimu ni kuelimika. Kwa hiyo, mnaweza kusoma *hansard* mtaona niliyoyazungumza katika miaka 7 iliyopita, na ninachokizungumza hapa ni cha kweli tupu sina sababu ya ubabaishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni haki ya mtoto na tumeishatoa elimu bure kwa shule ya msingi hapo naweka vyema kwa Mheshimiwa Waziri na kwa Wizara ya Elimu na Utamadini naweka vyema. Sisi kazi yetu kama Wapinzani ni kusema yale yanayotakiwa kusemwa kwa niaba ya wananchi, na ndiyo maana sisi hatujichanganyi kwenye uongozi tunakwenda kama wawakilishi wa nchi kwa ajili ya kutetea maslahi ya wananchi, na mengine yanayozungumzwa yakitendeka lazima tusifu kwa hiyo hapo naweka vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda New York, kwenye Mkutano wa Haki ya Mtoto. Nikazungumzia kwamba tunapotoa elimu ya bure kwenye shule za msingi na tuacha walimu wanaposomea ualimu vyuoni walipe ada tunashindwa kutimiza wajibu wa haki ya mtoto. Na baada ya hapo sizungumzi ugoro nimesema, mnaweza kwenda kwenye Umoja wa Mataifa mtakuta hiyo message ipo. Baada ya kurudi walimu wanasoma bure kwenye vyuo vya ualimu kwa hiyo naweka vyema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka jana nilizungumzia shule za sekondari wanafunzi wasome bure kwa sababu hawa watoto wa shule za sekondari ni watoto wa wazazi wale wale walalahoi. Watoto wale wazazi wao ni walalahoi, unapompa elimu ya shule ya msingi bure, halafu unamnyima elimu ya sekondari bure, unakuja kumpa kozi ya ualimu bure inakuwa haiwezekani. Akimaliza darasa la saba atarukaje ili aweze kwenda kwenye kozi ya ualimu ili aweze kwenda kuwafundishe mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa misingi hiyo naendelea kusisitiza kwamba elimu ya sekondari nayo itolewe bure ili kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata haki sawa, na elimu ni haki ya msingi ya watoto. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni naamini ni msikivu, kwa hiyo, mwaka kesho nitamwekea vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo basi, nampongeza kwa yale aliyosikiliza na kuyatekeleza. Hapa hatubishani tunazungumzia maendeleo na haki ya mtoto ni elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye utamaduni. Kwanza sijamalizia hapo kwenye elimu ya sekondari, kwa sababu tukiacha watoto hawa wasisome tutakuwa tunajenga tabaka la maskini na matajiri. Kwa sababu wazazi walio matajiri wanaweza kusomesha watoto wao nje ya nchi au kwenye *International school.* Lakini wazazi walio wengi ambao ni walalahoi hawawezi kusomesha watoto wao. Kwa hiyo, utakuta huko mbele ya safari yaani *future* utakuta watoto wa walalahoi wataendelea kuwa watoto wa walalahoi na watoto wa matajiri wataendelea kusoma, na tujua umaskini unatoka hasa kwenye elimu. Kwa hiyo naomba basi, tusiweke tabaka hili la watoto wa walalahoi ambao wamezaliwa bila kutaka wameshtukia tu wamezaliwa kwa wazazi maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba basi Wizara ya Elimu na Utamaduni ihakikishe kwamba elimu inatolewa bure kutoka darasa la kwanza mpaka *form four* na kwenye Vyuo vya Ualimu. Na hao walimu vilevile kwa kuwa ni wachache na watoto ni wengi, inaonekana mwalimu mmoja anaweza kufundisha watoto 100. Kwa hiyo, nashauri Wizara ya Elimu na Utamaduni ifanye utaratibu wa kufundisha *audio visual centers* za kuonyesha katika Televisheni ili watoto wapate mwalimu mmoja na waweze kupata faida ya elimu hiyo kwa watoto hata 1,000 katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani kulikuwa na mambo ya Redio, watu tulikuwa tunakwenda kwenye Redio Tanzania kusikiliza Kiingereza kinavyofundishwa na mwalimu mmoja nafikiri nchi nzima. Lakini sasa hivi tuko kwenye karne ya Sayansi na Teknolojia, kwa hiyo mimi nashauri mwalimu mmoja akae katika *centers* aidha, za kanda au za Mkoa, lakini watoto wamuangalie kwenye kipindi hicho maalum afundishe ili watoto wetu wote wapate elimu bora na *standard* sawa bila wengine kuwa wanajua na wengine wapo wapo tu. Naamini hilo litatendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye utamaduni. Utamaduni kuna mambo mengi, kuna ngoma na mavazi na vitu kama hivyo. Mimi nataka kuzungumzia mambo ya kale. Ukiangalia kwa haraka haraka Mambo ya Kale na majengo ya zamani unaona kwamba hakuna fedha. Lakini pale tunaweza kutengeneza fedha ila tunafikiria tu kwamba tumeshakuwa sisi wenyewe siyo wabunifu tunaachia mpaka mgeni aje afanye hiyo shughuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kigoma ukaangalia Livingstone Tembe ile ya Kigoma unakuta hakuna kitu chochote. Kuna mfanyakazi mmoja tu pale, ana-*cram* kila kitu. Mwaka huu Livingstone alikutana na Spiki hapa akafanya hivi, wakakutana kwenye mti, akikosea neno moja lazima ali-*rewind* ili aweze kwenda sawa sawa kwa muda wa saa nzima akiwa anazungumza. Sasa hii ni karne ya Sayansi na Teknolojia na vile vile ukienda kwenye Kaole Bagamoyo unakuta hadithi hiyo hiyo. Wafanyakazi wa pale wanakupitisha hapa sijui ilikuwa nyumba ya nani, ilikwendaje, hapa kuna maji ya Sheikh na vitu kama hivyo. Ambapo sasa tukikumbuka kwamba ni wakati wa Sayansi na Teknolojia na vilevile tunahitaji kufanya haya majengo yatuletee fedha ndiyo tuweze kuangalia utamaduni wetu na kuuona kwamba unafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi wote naamini hata Wizara ya Elimu na Utamaduni wanaoshughulika na mambo ya utamaduni wamesafiri nje ya nchi kuona wenzetu wanafanya nini katika nchi hizo. Kwa haraka haraka naweza kutoa mfano wa Haiderabad India kule kuna magofu kama haya ninayozungumza ya Kaole. Lakini watu wanakwenda siku za weekend wanalipa fedha kwa ajili ya kuangalia nyumba zile za magofu na kando kando kuna maduka ya kitalii wanauza tisheti na vitu vingine, shanga na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sijui kwa nini sisi tusifuate watu wa India mifano yake au watu wa China ambako nilikwenda vilevile unakuta hawana haja ya mtu mmoja ambaye ana-cram na hatuna mkataba na Mwenyezi Mungu kwamba mtu huyo ataendelea kuwapo mpaka gani, wameishaweka message hiyo kwenye tape.

Kwa hiyo, wewe unapofika pale unaulizwa tu wewe ni lugha gani unataka kusikiliza, kama ni ya Kiingereza unapewa tape ya Kiingereza, kama ni ya Kifaransa unapewa *tape* ya Kifaransa, unatembea mwenyewe kwa kusikiliza kanda. Wanakwambia nenda hatua tano, ukifika hapo katika jengo hilo utakuta ndiyo alikuwa anakaa Mfalme wetu, ukienda hatua tano kushoto utakuta nyumba na humo ndani ya chumba utakuta kuna kitanda ambacho alikuwa analalia Mfalme wetu na kadhalika. Sasa sisi tutafika lini huko na hali tuko katika Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja sasa hivi kubadilika na sisi kufanya hivyo. Maelezo tunayoyapata kule Kaole na maelezo ambayo tunayapata kule Livingstone Kigoma Tembe yawekwe kwenye tape ili watu wanapofika pale wanalipa fedha na wanaweza kuzunguka wakaonyeshwa kila kitu bila mtu kuwako pale akieleza kama ame-*cram*. Vilevile wangeweka vibanda vya kunywa soda au vya kupumzikia. Kwa hiyo hapo tunaingiza fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kitu cha kushangaza sana Watanzania tunazitafuta fedha, lakini ikionekana njia ya kutafuta fedha kama hii nyeupe hatutaki kuichukua fedha. Tunangojea mpaka mgeni aje abuni aweke hivyo vitu na tumlipe kulikoni! Kwa hiyo, naomba Wizara na Elimu na Utamaduni iwe bunifu wafikirie zaidi ya hii niliyowapa mwanya wenyewe waendeleze ili tuweze kupata fedha kutokana na utamaduni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utamaduni huo huo naomba kuzungumzia mambo ya *Dar es Salaam Internationa Airport.* Ni jambo la kusikitisha hapa juzi nilikuwa natoka *South Africa* mimi nikakuta wimbo unaoimbwa pale *Airport* ni wa Kihindi. Wimbo wa Kihindi kama tunaingia Mumbai na sisi tuko Dar es Salaam ambapo ni Tanzania. Kuna nyimbo nyingi sana za Kitanzania za Kinyamwezi, za Kihehe, za Kigoni, za Kigogo na kadhalika. Hizo ni nyimbo nzuri sana kwa nini tuweke nyimbo za Kihindi na tuache kuweka nyimbo za kwetu za kibantu ili kueleza utamaduni wetu. *We should be proud of our culture. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona nimalizie hapo yamenitosha kwa leo, na mengine yote yaliyotangulia. Nitaunga mkono yote yakifanikiwa hasa la elimu ya *Secondary School.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kumalizia ngwe ya jioni hii. Kuna mambo mengine pengine sisi wazungu wanasema *we are aiming high* tunatazamia vitu vya juu sana ambavyo inawezekana tusivipate vikabaki ni fikra tu.

Kwanza, mafunzo ya ualimu ya mwaka mmoja au miwili ya kutazamiwa, hivi kweli tutapata walimu bora. Walimu kusoma mwaka mmoja, mimi ni mwalimu nimechukua kozi ya ualimu kwa muda wa miaka mitatu. Kwa nini tusiweke kozi ya ualimu ikawa miaka tatu ili hawa kweli wawe ni walimu wameiva. Tutapeleka walimu ambao hawajaiva hakuna watakachofundisha tutarudi tena hapa na matatizo yale yale ya *UPE,* tatutakwenda mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunasema hisabati haipendwi na watoto si kwamba haipendwi, lakini ni nani tuliowaweka kufundisha hawa watoto somo la hisabati. Leo hawa walimu unawapa mafunzo ya mwaka mmoja je, vyuo vinavyofundisha hawa walimu vina walimu *competent* ambao wanajua hisabati na wanawafundisha walimu hawa waende kufundisha wanafunzi inavyotakiwa. Tusije tukafikiri shule mafanikio ni majengo tu. Tumefanikiwa kupata majengo ndiyo ya shule za msingi lakini upande wa elimu hatujafanikiwa bado. Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekiri kuna shule kama 40 hawakufaulu wanafunzi kwa muda mrefu. Sasa hii utasema umefanikisha pamoja na majengo yaliyojengwa, hakuna kitu na hatuwezi kwenda mahali hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tujali utaalam huo. Ukienda kwenye Vyuo vyetu vya Ualimu hata maabara zenyewe hakuna na vifaa hakuna, wanafundishwa walimu pale watakwendaje kufundisha sayansi huko shuleni, na dunia ya leo bila sayansi hakuna ugunduzi wowote tutabaki ni watu wa kusukumwa na kuswagwasagwa tu. Huwezi kufundisha ualimu kama wanavyofundishwa ualimu ya Katekisiti haiwezekani maana wale hawana suala la kutafuta ukweli ni kusema hakuna wa kukubishia. Lakini watoto lazima wafike mahali wafundishwe na wajifunze waulize, wapinge waonyeshwe ukweli ndipo wataelimika na ndiyo watajua na kutuelekezwa wapi tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba sana Wizara ya Elimu na Utamaduni ivikarabati Vyuo vya Ualimu na iweke vifaa vya kutosha na walimu wenye uwezo na walimu wanaokaa katika Vyuo vya Ualimu wawe ni wale ambao ni wenye ushindani mkubwa na wa Chuo Kikuu hapo ndipo tutapata hali halisi ya elimu tunayoitazamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, na vilevile walimu waheshimiwe. Walimu wenyewe hawaheshimiwi hawa ikifika wakati wa kustaafu wakifuatilia pensheni zao ukienda pale Wizara ya Fedha wanavyohangaika wale walimu utafikiri wamefiwa. Wana matatizo makubwa sana hata ile Tume ya Utumishi ya Ualimu hata wale watu waliofiwa wakienda pale kufuatilia mirathi yao wana matatizo makubwa. Kuna walimu waliokufa miaka ya 90 mpaka leo hawajalipwa haki zao na familia zao zina matatizo makubwa.

Lakini sasa walimu ni watu wenye huruma na wenye ari ya kujali utu. Unapofika hapo unajiuliza hivi huu ni ualimu tunaoufikiri huu. Lazima kwa kweli tuliangalie hilo na tulirekebishe ili kwa kweli walimu hao angalau wapate ahueni ya kuweza kuona kwamba wanaheshimika na wanatambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kuanzishwe utaratibu wa kuaandaa watoto hawa hivi mtoto wa 13 unampeleka wapi. Kama kweli hatuna nia ya kuvuruga tu kizazi hiki, Watoto wenye umri miaka 13 wakimaliza shule waende wapi kijijini, tunaandaa chokora wa nchi hii, hapana. Maana watoto hawa wakishamaliza darasa la saba hawana la kufanya hawawezi hata kulima bustani na hawawezi hata kuchuga ng’ombe. Sasa leo unawapeleka kijijini wakafanye nini. Sasa mimi nadhani hili kwa kweli lazima tukubali kuliona hili, hatuna sababu ya kuogopa. Ni afadhali tubaki maskini, lakini tuwaandalie watoto wetu hali nzuri itakayowapa matumaini ya kuishi ndiyo itakayotujengea heshima na utu wetu tuliopo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani watoto walikuwa na shughuli za ufundi ufundi hivi na elimu ya kujitegemea na mwenzangu amesema hapa lakini leo kuna nini. Leo hata kilimo hakuna, leo kuna shule hapa Mheshimiwa Waziri ameonyesha kwamba zitakazopewa chakula cha mchana. Shule ziko kwenye Jimbo langu watoto wanatoka kilomita 10 kuja kusoma shule, sasa hawa hawana chakula cha mchana watasomaje? Halafu mnasema wawe watoto wa miaka 6 au 7, mtoto mwenye umri wa miaka 7 hata kuvumilia njaa hawezi atasomaje huyu. Kama ni suala la kutoa chakula cha mchana tuangalie katika sehemu zote. Mimi nakubaliana kama mlivyoorodhesha Dodoma na

nini kwa sababu ya njaa sawa. Lakini watoto wote wanahitaji kupata chakula cha mchana ili waweze kufuatilia masomo yao sawa sawa. Kwa hili suala tusije tukaanza kuchagua tu vitu halafu tunaacha vitu vingine vibaki katika hali ya kushangaza na kushtua hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu lugha. Mimi nilikwenda Japan wakasema wao walikuwa hawana lugha ya maandishi ya Kijapani, wakamua kuchukua Kichina. Wametumia lugha hiyo ndiyo lugha yao na mambo yao yote ya elimu wanatumia Lugha hiyo. Mambo ya Kiingereza na nini yanabaki kwenye sehemu ya mambo ya nje huko na shughuli zingine za biashara. Lakini sisi tumeg'ang'ania Kiingereza. Hivi kweli Kiswahili hakifundishiki sasa! Hivi kweli vijarida vyote vilivyotolewa na Chuo Kikuu havifai kutusaidia kufundisha Kiswahili. Aaah jamani hii nadhani ni majivuno ambayo hayana msaada wowote huko tunakokwenda. Lazima tujivunia lugha yetu. Mimi nimezungumza na walimu wa Kiswahili pale Chuo Kikuu wanasema wana uwezo kabisa na hakuna mashaka yoyote. Leo tunasema eti tufundishe Kiingereza wako vijana wetu sasa elimu hii wanayoipata kwenye shule za msingi haina utaratibu kwa sababu hawakielewi Kiingereza ni balaa kwako na wanashindwa mitihani kwa sababu hawaelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafundishe lugha hii, kama ni tatizo wabandike na yale ya Kiingereza, ya Kilatini ndivyo watu wanavyokwenda na lugha inakwenda hivyo. Siyo suala la kusema utapata tafsiri zote za Kiswahili, utazipata wapi. Hata Kigiriki nacho kina maneno ya kuazima kwa nini sisi tuziazime. Kwa kweli kusema eti watu hawawezi kuelewa, hivi leo watoto wanatoka huko wa Kimasai wanaingia shule wanaanza Kiswahili tu ndiyo hawajasikia Kiswahili tangu wazaliwe wanajifunza wanaelewa. Chukua Wagogo hawajui hata Kiswahili huko vijijini lakini wakijifunza wanaelewa, Wanyakyusa, Kiswahili hawajui lakini wakifundishwa wanaelewa. Hivi tatizo ni nini linalotufanya tuone Kiswahili si lugha nzuri. Hii nadhani tunajirudisha nyuma na tunajicheleweshe bure. Hili kwa kweli Wizara ya Elimu na Utamaduni iamue na Wizara yetu ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu nayo ilizingatie hili, watoe uamuzi utakaojenga heshima ya nchi hii. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani tunalo tatizo ama la kufikiria vitu ambavyo havina utaratibu. Tunasema michezo haifai. Lakini ukisikiliza Redio sasa juu ya timu hii iliyokwenda Sudan vurugu kabisa. Kila mtu anataka michezo, nadhani hata Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni naye yumo katika mawazo hayo iliposhinda Simba watu walikwenda mpaka uwanjani na ni watu wazito kabisa. Lakini ukisema jamani na michezo ifundishwe, hivi mchezo wa mpira unadhani ni suala sawa na kuswaga ng'ombe wa Wasukuma tu, unapiga na mawe. Lakini kuwe na utaratibu na watu wajifunze mbinu za michezo na taratibu za michezo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa michezo ni ajira watu wanaajiriwa na watu wanaleta uchumi wa fedha za kigeni wakienda kucheza huko nje. Leo sisi tunasema eti michezo hapana. Nadhani tunalo tatizo la kuzaliwa nalo sisi. Michezo ndiyo utamaduni, Msukuma akienda Ulaya akaimba Kisukuma watu watauliza hivi huyu anayeimba anatoka nchi gani ndiyo wanaijua Tanzania kumbe Wasukuma wako huko. Siku moja

nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Pius Ng'wandu akaniambia Wasukuma bwana wako Zaire, kuna nyimbo wanaimba Wazaire sukuma, sukuma kumbe ni kweli wapo Wasukuma kule. Sasa hii inawapa moyo hata ukienda Zaire Msukuma una moyo wa kusema wapo wenzangu huko. Lakini sasa tumejibana tu hapa hapa ndiyo maana hawa ndugu zangu hawa Wahutu nao wamezuia kule pembeni, sasa utamaduni hawana kule, hatuna tunachoonyesha sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani ni vizuri tukaangalie juu ya suala hili. Michezo inaburudisha, michezo inafanya hali ya afya na miili ya watoto ijengeke kutosheleza elimu na kujenga akili ya kuamua mambo haraka haraka. Mtu unayeona anapiga chenga kwa kuzubaazubaa ujue hata mawazo yake ni ya kuzubaazubaa tu. Kwa hiyo, sasa ni vyema kwa kweli suala la michezo hili wala tusilifanyie mchezo tuamue michezo shuleni iwepo na watoto washindane. Vipindi vya kusoma wasome hatutaki michezo iingilie vipindi vya masomo. Hata wakisema Jumamosi waende shule wafanye shughuli za michezo waende.

Kulikuwa zamani wakati wa Mkoloni na Kwata yote hii ni michezo ya kuwajenga watoto wawe na mawazo ya kubadilika haraka na kujihami haraka. Sasa sisi tunasema watoto wasome tu, watasoma mpaka wapi haitawezekana lazima waweze kuijenga miili yao kwa ajili ya kujitetea na kujiweka sawa kwa namna yoyote ile ya ushindani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Na nawashukuru wote kwa kusikiliza, na naunga mkono hoja ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Naomba basi na sisi atusikilize kwa kubadili kuonyesha kuwa ametuelewa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani dakika zilizobaki hazitoshi kwa mchangiaji mwingine. Kama nilivyosema asubuhi wote walioomba watapata nafasi ya kuchangia. Wizara hii imepewa siku mbili, kwa hiyo wale waliobaki majina yenu yapo kesho mtapata nafasi ya kuchangia. Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 9 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*